Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Sita – Tarehe 18 Juni, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 47

**Mpasuko wa Kisiasa Tanzania Zanzibar**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwenye hotuba yake ya kulifungua Bunge aliyoitoa tarehe 30/12/2005 aliliambia Bunge kuwa anasononeshwa sana na mpasuko wa kisiasa ulioko huko Tanzania Zanzibar na kuahidi kwamba atautafutia ufumbuzi wa kudumu:-

Je, ni hatua gani zimefikiwa katika kutekeleza ahadi hiyo muhimu kama ilivyoahidiwa mbele ya Bunge na kwa Watanzania wote kwa ujumla?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA NA URATIBU** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya awali ya utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwea Rais ilikuwa ni kwa vyama husika kuunda kamati chini ya uenyekiti wa Makatibu Wakuu wa Vyama hivyo ili kukutana na kufanya mazungumzo kwa lengo la kufikia makubaliano ambayo yangezaa muafaka. Pendekezo hilo lilitekelezwa kikamilifu

na wawakilishi wa CCM na *CUF* chini ya uenyeviti wa Makatibu Wakuu wa Vyama hivi viwili. Hadi Mwezi Aprili, 2008 wawakilishi hao walikuwa wameishakutana na kufanya mazungumzo yaliyohusikasha agenda muhimu kwa takribani miezi kumi na nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya mazungumzo hayo ilikuwa ni kupata muafaka baada ya vyama husika kuwasilisha kwenye vikao vya maamuzi katika vyama vyao mapendekezo kuhusu makubaliano yaliyofikiwa. Hata hivyo, kama mnavyofahamu kwamba hatima ya mazungumzo yale hayajafikiwa kwa sababu ambazo sote tunazifahamu.

Mheshimiwa Rais ameendelea kusihi kwamba wakutane kama ilivyokubaliwa awali ili kutathmini maazimio na mapendekezo yaliyofikiwa baada ya kila upande kuwasilisha taarifa ya awali katika vyama vyao kuhusu makubaliano yaliyofikiwa na Kamati ya Muafaka. Azma ya Mheshimiwa Rais katika utatuzi wa suala hili ni thabiti na kwamba hakutokuwa na njia ya mkato katika ufumbuzi wa mpasuko uliopo zaidi ya hatua iliyokwishachukuliwa na Serikali katika kuwezesha kukutana kwa Kamati hiyo na kufanya vikao mbali mbali. Kupitia Bunge hili, tunashauri kuwa ni vyema ombi lililotolewa na Mheshimiwa Rais kuhusu kurejea kwenye meza ya mazungumzo likatekelezwa haraka iwezekanavyo ili kutokwamisha juhudi zilizokwishaanza na kufikia hatua nzuri ya maafikiano. Hatima ya majaliwa kisiasa ya wananchi wa Tanzania inategemea sana busara zetu kama viongozi katika kufikia suluhisho la kudumu kwa manufaa ya sasa na vizazi vijavyo.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kuwa suala hili limekuwa la muda mrefu na suala hili kutokukamilika linaitia aibu Tanzania ndani ya nchi pamoja na nje ya nchi, na ndiyo maana Rais wetu kila anapotembea anaulizwa swali hili; na kwa sababu kumetokea matatizo katika nchi za jirani na amekwenda kusasidia na ameyaklamilisha, lakini hili la Zanzibar limekuwa gumu, halimaliziki?

Swali la pili; kwa kuwa Mheshimiwa Rais suala hili alianza kulizungumza hapa Bungeni, pamoja na maelezo aliyosema Mheshimiwa Waziri. Je, Bunge hili litamsaidia vipi Mheshimiwa Rais kuhakikisha kuwa suala hili linamalizika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kabla sijajibu maswali hayo mawili, ningependa kuliaridu Bunge kwamba mara ya kwanza tulipopata swali hili, tulifikiria kulirejesha kwa Mheshimiwa Mbunge kwa kushauriana na uongozi wa Bunge kwa sababu suala lenyewe bado liko ngazi ya vyama husika na Mbunge aliyeuliza swali hili ni mmojawapo wa viongozi wa ngazi ya juu wa chama kimojawapo. Kwa hiyo, tulidhani alikuwa anafahamu hatua iliyokwishafikiwa katika kutafuta muafaka. Sasa, kuhusu swali lake la kwanza kwamba imechukua muda mrefu kwa tatizo hili kutatuliwa. Bado msimamo wa Serikali ni kwamba wale ambao wamejitoa kwenye mazungumzo, warejee kwenye meza ya mazungumzo kwa sababu hakuna njia mbadala. Pili; katika hatua tuliyonayo sasa,

suala hili halijafika kwenye ngazi ya Bunge. Suala hili liko kwenye ngazi ya vyama husika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimwona Mheshimiwa John Cheyo, halafu muulizaji wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Selelii katika swali hili.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Ahsante sana. Kwa kuwa hili jambo sasa linazungumzwa Bungeni na halizungumzwi tu katika vyama vinavyohusika; na kwa kuwa inavyoonekana Serikali inalipia hata haya mazungumzo. Kwa hiyo, ni jambo ambalo ni la kitaifa; hawaoni kwamba labda mazungumzo haya yasingekuwa ya vyama viwili na kwamba mazungumzo haya kama kweli tunataka kutafuta njia ya kuziba mpasuko kwa kudumu, yawe ni mazungumzo ambayo ni mapana zaidi na vyama vyote ambayo vinahusika katika nchi hii viweze kuhusishwa ili tupate jibu la kudumu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA NA URATIBU:** Kwanza, nirejee yale niliyosema hapo punde kwamba tungependa kulirejesha suala hili kwa Mbunge aliyelileta. Lakini kwa dhamira ya kutaka kuwaarifu wananchi hatua iliyofikiwa katika mjadala huu, ndiyo maana tumelifikisha hapa. Na hatua hii ni hatua ambapo kuna ajenda moja ambayo haijafikiwa, lakini upande mmoja ulikuwa umejitoa. Kwa hiyo, tulidhani hatua hizi zingekamilika na baadaye vyama husika vikafanya maamuzi na hatimaye maamuzi yale kama yanahitaji utatuzi wa kesheria au kuletwa Bungeni, basi tungeanza mjadala huo ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kupanua wigo wa mazungumzo, mimi nadhani mahala pake siyo hapa. Vyama vyetu vina utaratibu wa kukutana na utaratibu huo ahaujaainishwa katika sheria ya vyama vya siasa wala taratibu zetu za kanuni za Bunge na hata Katiba ya nchi. Kwa hiyo, pamoja na kuwa ni wazo zuri kupanua wigo wa mazungumzo haya, kwa vile yanagharimiwa na Serikali. Kwa vile hatima ya mazungumzo haya ni kurejesha mahusiano mema katika nchi yetu, tungependa wigo wa mazungumzo upanuke, lakini mahala pa kujadili na kufanya maamuzi siyo ndani ya Bunge, ni ndani ya vyama vya siasa.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED – KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali moja la nyongeza. Ikiwa yeye Waziri anao ushahidi wa wazi kwamba chama kimoja kimejitoa kwenye mazungumzo na kama ushahidi huo anao, anaweza akasema kwamba Bunge hili hakuliarifu taarifa sahihi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la msingi hapa siyo ushahidi, la msingi ni ombi la Mheshimiwa Rais kuomba pande zote mbili kurejea mezani kujadili hatima ya muafaka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na swali linalofuata. Ninaomba kuwapa taarifa. Kwa mujibu wa Kanuni zetu, anaposimama Kiongozi wa Upinzani Bungeni, kwa mujibu wa Kanuni, ni lazima apewe nafasi ya kuzungumza. Na

mara tu suala lolote linapotokea, atakaposimama Mheshimiwa Waziri Mkuu saa na wakati wowote, ni lazima apewe nafasi ya kuzungumza. Kwa hiyo, ninaomba nitoe hiyo taarifa ili muelewe utaratibu wa kuendesha shughuli ndani ya Bunge. Kwa hiyo, tunaendelea na swali linalofuata. *(Makofi)*

Na. 48

**Uwakilishi wa Wabunge kwenye Halmashauri**

**MHE. ALI SAID SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa Wabunge ndio wawakilishi wa wananchi; na kwa kuwa Wabunge wa Zanzibar si wajumbe wa Halmashauri wanazotoka:-

Je, Serikali haioni kuwa huo ni upungufu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA NA URATIBU** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, muundo wa utawala nchini Tanzania kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ni wa Serikali mbili, yaani Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Wabunge tumepewa dhamana ya uwakilishi wa wananchi kwa mujibu ya Katiba hiyo. Uwakilishi huo ni kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano na Baraza la Wawakilishi, ambako sheria mbali mbali hutungwa na kuweka taratibu za uanzishwaji wa vyombo mbali mbali vya utoaji maamuzi katika ngazi ya utawala, hususan Serikali za Mitaa pamoja na sheria na Kanuni zinazosimamia mamlaka hizo. Majukumu ya vyombo husika hutegemea malengo na madhumuni ya kuundwa kwake kwa mujibu wa sheria. Kwa kuzingatia muundo na majukumu ya vyombo hivyo vya uwakilishi wa wananchi kwa upande wa Tanzania Zanzibar. Ni vyema Mheshimiwa Mbunge akawasilisha swali hilo au ushauri huu kwenye Baraza la Wawakilishi Zanzibar au katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili liweze kufanyiwa kazi.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Waziri, ni kwamba shughuli hizi zinahusu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Sasa, je, kuna uhalali gani wa kuchukua fedha za kujenga ofisi za Wabunge ambao Wabunge wenyewe hawawajibiki SMZ, zikapelekwa katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar? Hilo, swali la kwanza. *(Makofi)*

Swali la pili; sasa kwa kuwa imeonekana kwamba ni dhahiri kwamba, utaratibu huo si sahihi. Je, Serikali hii sasa itafanya utaratibu gani kuhakikisha kwamba fedha hizo hazifikii SMZ ila kwa njia hiyo zinafikia njia nyingine? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mantiki ya majibu yangu katika swali la msingi ni kwamba jambo hili au suala hili kwa mujibu wa Katiba yetu siyo suala la Muungano. Ndiyo tafsiri na mantiki ya jibu la swali la msingi na ndiyo pia jibu la swali la pili la Mheshimiwa Mbunge kwamba utaratibu huu ni sahihi, kwa sababu eneo la Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Katiba yetu siyo eneo la Muungano.

Kuhusu swali lake la kwanza; madhumuni ya ofisi zetu, hasa ile ofisi ya Zanzibar, ni kuwahudumia Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa upande ule na ndiyo maana ili huduma iwafikie Kwa karibu zaidi. Pia tunafikiria kujenga ofisi nyingine Pemba. Ofisi hizi hazina uhusiano na taratibu za Serikali za Mitaa ambazo siyo eneo la Muungano.

Na. 49

**Kuhamishwa kwa Wafanyabiashara Ndogondogo**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwepo na taratibu za kuwahamisha wafanyabiashara ndogondogo katika maeneo ya mitaa ya miji yetu kama vile Dar es salaam, Arusha, Mwanza na kadhalika; na kwa kuwa mara nyingi zoezi hilo hufanywa na Askari Mgambo ambao huonekana wakipora mali za wafanyabiashara hao na pengine kuziharibu kabisa:-

(a) Je, zoezi hilo hufanywa kwa mujibu wa sheria, na kama ndivyo, ni sheria gani hiyo?

(b) Kama Serikali inahimiza wananchi kufanya kazi kwa bidii ili kujikomboa na umaskini. Je, inaionaje hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi sasa katika miji yetu kumekuwepo na hatua mbali mbali za kuwahamisha wafanyabiashara wadogo wadogo kutoka katika maeneo yasiyo rasmi. Aidha, tunafahamu kuwa liko ongezeko kubwa la watu kutoka vijijini kwenda mijini ambao wamekuwa wakitafuta ajira ili kuweza kukabiliana na maisha ya kila siku. Kutokana na

hali hii, vijana wengi wanajihusisha na biashara ndogo ndogo kama njia ya kujipatia ajira.

Hata hivyo, wafanyabiashara hao wanakuwa wakiendesha biashara zao kinyume na sheria kwa kuvamia maeneo yasiyo rasmi na yasiyoridhisha. Hali hii inasababisha kuwepo na matatizo kama vile:-

§ Kupungua kwa usalama wa raia na mali zao.

§ Msongamano wa watu katika eneo moja na uchafuzi na uharibifu wa wa mazingira.

§ Kuziba barabara na njia za waenda kwa miguu.

§ Kuharibu miundombinu mbali mbali ikiwa ni pamoja na mandhari ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kuwaondoa wafanyabiashara ndogondogo katika maeneo ya miji wanayofanyia biashara linafanyika kisheria. Baadhi ya Sheria hizo ni hizi zifuatazo:-

(i) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Miji) Sura ya 288 (awali Sheria Na. 8/1982) Kifungu Na. 66(1), (n) na (o); na

(ii) Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya mwaka 2007 *(Urban Planning Act, No. 8/2007)* Kifungu cha 7(5)(b), (s) na (u).

Sheria hizi kwa pamoja zinazipa Mamlaka za Miji madaraka ya kupanga na kusimamia matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza madaraka hayo, mamlaka za Serikali za Mitaa zimepewa uwezo wa kupanga matumizi mbali mbali ya ardhi, yakiwemo:-

Biashara, makazi, huduma za jamii na maeneo ya wazi. Kwa mujibu wa sheria hizo, mwananchi atakayekiuka utaratibu wa mipango ya matumizi bora ya ardhi iliyowekwa na Halmashauri husika, atakuwa anakiuka sheria.

Aidha, Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara Na. 14/2007 *(The Business Activities Registration Act. No. 14/2007)* kifungu cha 16(a) – (f), kinaelekeza mambo ya kuzingatiwa na wafanyabiashara wote ikiwa ni pamoja na kuzingatia masharti ya mipango miji, hifadhi ya mazingira na kanuni za afya.

Hata hivyo, katika kutekeleza sheria hizo, tunakubali kuwa unatokea upungufu. Kwa mfano, uharibifu wa mali za wahusika. Lakini, pale inapothibitika kuwa mali hizo zimeharibiwa kwa makusudi au kuporwa na Askari Mgambo waliohusika na zoezi hilo, litakuwa ni kosa la jinai na sheria itafuata mkondo wake.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwepo kwa wafanyabiashara ndogondogo na umuhimu wao katika kuchangia kuwepo kwa ajira. Huongeza kipato kwa anayejishughulisha na biashara na jamii inayomtegemea na kuchangia katika kuongezeka kwa pato la taifa. Serikali inalo jukumu la kuwashirikisha wananchi wote kwa njia ya uwezeshaji katika ujenzi wa uchumi na kutokomeza umaskini. Aidha, Serikali inahimiza wananchi kufanya kazi kwa bidii ili kujikomboa na umaskini. Lakini, kwa kufanya hivyo, hawatakiwi kuvunja sheria na taratibu zilizowekwa. Kwa sababu hiyo, Serikali kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa imejitahidi kuchukua hatua za kuwatambua wafanyabiashara hao katika maeneo mbali mbali nchini na kuwatengea maeneo yenye huduma mbali mbali ikiwa ni pamoja na barabara, usafiri, vyoo, huduma za afya, maji na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, utekelezaji wa zoezi hili ni endelevu kwa kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini zinaendelea kuweka mikakati mbali mbali ya muda mfupi na muda mrefu na kuitekeleza.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru tu kwa majibu mazuri aliyoyatoa Naibu Waziri.

Lakini, mimi niseme tu kwamba kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri anakiri kwamba Serikali inahimiza wananchi wake kufanya shughuli mbali mbali za kibiashara na shughuli mbali mbali za maendeleo ili kujikomboa na umaskini; na kwa kuwa katika utekelezaji wa sheria hizo kwa maana ya kuzisimamia, upungufu ni mkubwa mno na ukiona namna ambavyo wale askari mgambo wanavyonyang'anya mali za wale hasa vijana, na ukiona namna ambavyo zinaharibiwa, utasikitika kwa sababu nao wale wamekopa kutoka kwenye mabenki na wanahitaji kurejesha.

Je, Serikali haioni kwamba ni busara ikatoa agizo la kutekeleza sheria hizo au kuzisimamia sheria hizo kwa utaratibu mzuri na siyo kwa kuharibu mali maana yake mali hazina matatizo yoyote? *(Makofi)*

Hilo la kwanza. Lakini, la pili. Je, Serikali iko tayari kuagiza Halmashauri zote na hasa Halmashauri za Majiji na Miji, kuweka vibao au alama zinazozuia watu kuendesha shughuli fulani katika maeneo husika, badala ya kuweka kama mtego wa kuwanasa ikiwa ni pamoja na zile sehemu wanazozuia kupaki magari ambazo ahazina vibao vyovyote wala alama yoyote inayozuia kufanya hivyo na inakuwa kama mtego na watu wamekaa pale wanasubiri unaswe kwenye mtego ule?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Majibu! Tunaomba majibu yawe mafupi!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekiri hapa kwamba katika utekelezaji wa utaratibu huu na sheria hizi, tumekuwa na matatizo ya hapa na pale na upungufu umejitokeza. Nakiri kabisa kwamba katika hali hii ya kwamba unataka sasa

uwasogeze vijana kutoka katika maeneo hayo wanayopita, tunawapeleka katika maeneo ambayo yameandaliwa, kumetokea huo upungufu. Mheshimiwa Simbachawene anataka kuona kama tunaweza kutoa tamko hapa kuhusu wale wanaofanya hivyo. Msimamo! Utaratibu unataka tufanye mambo yote katika nchi hii kwa kufuata sheria na Katiba. Ni marufuku kwa kiongozi yetote yule na ni marufuku hata vijana wetu wa mgambo wale kumsumbua kijana anayefanya biashara yake pale eti tu kwa sababu amefanya katika eneo ambalo haliruhusiwi. Anachotakiwa kufanya pale ni kumpa maelezo na kumpa amri ya kwamba sasa unachukuliwa na unapelekwa kwenye kituo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri pia tukakumbuka kwamba wakati inapofanyika hivyo, kurupushani za hapa na pale zinaweza zikatokea, na hivyo nguvu ikaweza kutumika pale. Kwa hiyo, kwa msingi huo, utaona kwamba hilo analozungumza Mheshimiwa Simbachawene linaweza likajitokeza pale. Lakini, maelekezo tunayotoa hapa ni kwamba tufuate sheria, tufuate taratibu, vijana hawa wana mchango mkubwa, lakini tunachosema wawepo katika utaratibu unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; Mheshimiwa Simbachawene anazungumzia utaratibu wa kuweka vibao ili kuweza kuonyesha kwamba eneo hili haliruhusiwi kupaki gari, eneo hili haliruhusiwi kuweka biashara na vitu vingine vya namna hiyo. *(Makofi)*

Naomba kwa niaba ya Waziri Mkuu nichukue fursa hii kutoa maelekezo kwamba Halmashauri zetu zote nchini zihakikishe kwamba zinaweka vibao katika maeneo ambayo hayaruhusiwi kufanya biashara ndogo ndogo na waelekeze waende katika maeneo wanayotakiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majibu yamekuwa marefu sana. Ninaomba tuendelee na swali linalofuata.

Na. 50

**Mchango wa Serikali ya Muungano katika Kusukuma Maendeleo ya Zanzibar**

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALFAN** aliuliza:-

Kwa kuwa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 pamoja na mambo mengine imebainisha ahadi ya kuwepo kwa ongezeko la mchango wa Serikali ya Muungano katika kusukuma maendeleo ya Zanzibar:-

Je, ahadi hiyo hadi sasa imeishatekelezwa kwa kiasi gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, Mbunge wa Tumbe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 hakuna kipengele hata kimoja kinachoelezea moja kwa moja ahadi ya kuwapo ongezeko la mchango wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kusukuma Maendeleo ya Zanzibar. Hata hivyo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayo wajibu wa kusaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada mbalimbali zimekuwa zikiendelea kufanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zikiwa ni mchango wake katika kusukuma Maendeleo kwa upande wa Tanzania Zanzibar.

Mfano mzuri ni kupitia Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania ambapo pande zote mbili za Muungano zimeshirikiana ipasavyo na hatimaye kuweza kupata wafadhili wa miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na *TASAF, SELF, MACEMP, PADEP, ASDP* na *MCC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ongezeko la misaada, mikopo na faida ya Benki Kuu ya Tanzania, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweza kupata ongezeko katika gawio lake, yaani kutoka shilingi bilioni 18.65 kwa mwaka 2005/2006 hadi shilingi bilioni 23.02 kwa mwaka 2006/2007 na hadi shilingi bilioni 28 kwa mwaka 2007/2008. Aidha, katika mwaka huo wa 2007/2008 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliipatia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar shilingi bilioni 1.9 (hizi zikiwa ni ziada ya ule mgao wa 4.5%) ili kuchangia ujenzi wa Ofisi za Baraza la Wawakilishi, Zanzibar.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hakuna swali la nyongeza. Kwa hiyo, tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa, nafikiri utumie mic ya jirani yako kama hiyo ya kwako haifanyi kazi!

Na. 51

**Ajira za JWTZ Zinazotolewa kwa Upendeleo**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa JWTZ ni Jeshi la Muungano la Wananchi wote wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, ambapo hata nafsi za ajira jeshini hutolewa kwa uwiano maalum kwa pande zote mbili za Muungano; na kwa kuwa imebainika kuwa kuna nafasi zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya Tanzania Zanzibar zilitolewa kwa watu wa Tanzania Bara:-

(a) Je, hii ni haki kwa chombo nyeti kama hiki?

(b) Je, nini mantiki na sababu za gawio ndani ya Jeshi hilo?

(c) Je, yako makubaliano gani kwenye ajira zinazotolewa na Jeshi la Muungano?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, JWTZ limekuwa likiajiri vijana kutoka Mikoa yote 26 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzingatia kukidhi vigezo vya sifa zilizowekwa. Baadhi ya sifa hizo ni:-

§ Awe raia wa Tanzania;
§ Umri kuanzia miaka 18 – 23;
§ Elimu ya kidato cha nne na kuendelea;
§ Awe na akili timamu;
§ Asiwe ameoa au kuolewa na asiwe na mtu yeyote anayemtegemea;
§ Awe tayari kufuata sheria zote za Jeshi zitakazokuwa juu yake;
§ Awe na tabia na mwenendo mzuri; na
§ Awe hajatumikia Jeshi la Polisi au Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kwamba tunaziba mianya yote ya upendeleao na kupata vijana wanaoandaliwa vizuri katika mafunzo ya awali ya kijeshi, JWTZ limebadili utaratibu wa awali wa kuchukua vijana. Hivyo, kuanzia Julai Mosi, 2008, JWTZ litaajiri vijana waliopitia JKT na JKU.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Kwa kuwa uajiri wa Jeshi linakuja gawio Tanzania Zanzibar, na kwa kila Wilaya hutokeza kwamba hugawiwa vijana idadi maalum.

Lakini kwa kuwa imebainika kwamba uongozi unatoka kutoka sehemu moja ya Muungano na kuleta vijana wao ili zile nafasi za Zanzibar kuchukua wao.

Je, huoni kwamba kitendo hiki kinawatoa imani vijana wa Zanzibar? Pili, kwa kuwa suala hili kwa uhakika limefanyika; na kwamba vijana hawa wametokwa na imani kutokana na kitendo hicho; na kwa kuwa mafunzo hayo yako hapa Dodoma sehemu ya Makutopora.

Je, Serikali itakuwa tayari kufuatana na kuhakikisha kwamba wale vijana walioingizwa kinyume na taratibu kutolewa ili kuwa visomo kwa kitendo hiki kisitokee tena?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, naomba nilihakikishie Bunge lako kwamba hatuna utaratibu wa kugawa askari wetu kwa misingi ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nilihakikishie Bunge lako kwamba utaratibu tunaotumia ni wa kuangalia sifa za wanaohusika. Kwa sasa wanafunzi wetu wote wa kijeshi walioko kwenye mafunzo wanazo sifa nilizozitaja katika jibu la msingi.

Na. 52

**Wanajeshi wa JWTZ Waliokwenda Comoro**

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA** aliuliza:-

Kwa kuwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania lilikuwa miongoni mwa Jeshi la Umoja wa Afrika waliokwenda Comoro kwa ajili ya kuikomboa Anjuoani mwaka 2008 na kupata mafanikio yaliyokusudiwa:-

(a) Je, Serikali imetumia kiasi gani cha fedha katika kukamilisha kazi hiyo?

(b) Je, Umoja wa Afrika pamoja na nchi marafiki nao wanasaidia kiasi gani katika kukamilisha operesheni hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Wete lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetumia Tsh. 7,123,000,000 kwa ajili ya kukamilisha kazi hiyo. Fedha hizo zilitumika kuwandaa wanajeshi, kulipa posho, kuwasafirisha, kuendesha operesheni na kuwarejesha baadhi yao nyumbani baada ya operesheni kumalizika. Wafadhili walitoa kiasi cha dola za kimarekani 6,000,000 kufidia matumizi hayo ya Serikali yetu.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Pamoja na kazi zote ambazo zimefanywa na wanajeshi wetu kule Anjuoani ambazo zinapigiwa mfano, ninataka kujua fedha hii ya Serikali bilioni 7.1 imetoka kasma gani na kama fedha hii haikuathiri mwenendo mzima wa bajeti ya Jeshi? Kwa kuwa jirani zetu wa Uganda kwa muda mrefu walikuwa wanasumbuliwa na waasi kule Kaskazini mwa nchi kiasi ambacho maisha ya wananchi yanapotea kwa wingi. Je, Serikali iko tayari kwenda kuwasaidia wanajeshi wa Uganda kwenda kuondoa uasi ule?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, fedha zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya kugharimia shughuli za Comoro zilitoka katika Mfuko wa Serikali Kuu na zilitoka kwa maelezo

rasmi kwamba zitarejeshwa na wafadhili na *AU* na tayari zimeisharejeshwa. Pili, kuhusu waasi wa Uganda, Serikali ya Tanzania haijapewa maombi rasmi ya kusaidia kuondoa waasi hao, ila tunaunga mkono mazungumzo yanayoendelea katika nchi hiyo, kati ya Serikali na waasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nitoe utaratibu; Linapoulizwa swali la msingi, wakati Mheshimiwa Waziri anapomaliza kujibu swali la msingi, ninapotoa nafasi ya maswali ya nyongeza; mwenye nia ya kuuliza swali la nyongeza, ndiye anatakiwa asimame wakati huo. Sasa, nimegundua kwamba kuna baadhi ya Wabunge wamekuwa wakisikiliza majibu na majibu ya nyongeza, halafu wanajisikia hamu ya kuuliza, ndio wanasimama. Sasa, naomba niseme huu si utaratibu. Tunaendelea na swali linalofuata. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 53

**Mradi wa Maji wa *World Bank***

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa wananachi wa vijiji vya Chamanda, Simai, Igoji Kusini (Salaza) na Igoji Kaskazini, katika Kata ya Mima Wilayani Mpwapwa wana matatizo makubwa ya kudumu ya maji; na kwa kuwa mradi wa maji wa vijiji vya Chamanda na Igoji Kusini uliofadhiliwa na Benki ya Dunia kwa thamani ya shilingi milioni 200, ulikamilika na kuanza kutoa huduma ya maji kwenye vijiji hivyo:-

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba vijiji hivyo havina huduma ya maji baada ya baadhi ya mabomba kusombwa na maji?

(b) Kama Serikali inafahamu hilo; Je, ni lini ukarabati utafanyika ili wananchi wa vijiji hivyo waendelee kupata huduma hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Igoji Kusini ambapo pia kuna vitongoji vya Chamanda na Simai kilipata mradi wa maji ya mtiririko uliojengwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia. Ujenzi wa Mradi huo uligharimu shilingi 150,648,675, ulikamilika mwezi Julai, 2004. Hata hivyo, mwezi Desemba, 2004 wakati mradi upo kwenye kipindi cha matazamio *(retention period),* mvua kubwa ilinyesha na kusomba baadhi ya mabomba. Mkandarasi aliyepewa kazi ya ujenzi alielekezwa kurekebisha kasoro hiyo. Baada ya marekebisho hayo, wananchi wa kijiji cha Igoji Kusini waliendelea kupata huduma ya maji hadi mwezi Machi, 2006 wakati huduma hiyo

iliposimama tena kutokana na baadhi ya mabomba yenye urefu wa mita 859 kusombwa tena na maji ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kijiji cha Igoji Kaskazini kuna mradi wa kisima kirefu kinachotumia pampu inayoendeshwa na injini ya dizeli. Mradi huo uliojengwa mwaka 1974 ndio unatoa huduma ya maji katika kijiji hicho.

Mheshimiwa baada ya maelezo hayo mafupi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, lenye sehemu (a) na (b) yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafahamu kwamba kijiji cha Igoji Kusini ambacho pia kina vitongoji vya Chamanda na Simai hakipati huduma ya maji kutoka mwezi Machi, 2006 baada ya baadhi ya mabomba kusombwa na maji ya mvua. Kwa kuwa uharibifu huo ulitokea ndani ya kipindi cha matazamio ya mkandarasi wa ujenzi tarehe 13 Machi, 2006, Halamashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ilimwelekeza Mkandarasi wa ujenzi wa mradi huo akarabati sehemu ambayo mabomba yaliyosombwa na maji. Halmashauri ilimwandikia Mkandarasi barua tarehe 12 Mei, 2008 na kumuagiza awe ameanza kazi hiyo kabla ya tarehe 13 Juni, 2008. Kwa kuwa Mkandarasi hakutekeleza maelekezo yaliyotolewa, Halmashauri inaandaa utaratibu mwingine wa kukarabati eneo hilo kwa kutumia fedha za Mkandarasi za *retention*. Kazi hiyo itafanyika kabla ya mwezi Septemba, 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumanne, tarehe 16 Juni, 2008, Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji alifanya ziara ya siku moja katika Wilaya ya Mpwapwa ili kujionea mwenyewe na kupata taarifa ya hali ya maji katika Wilaya ya Mpwapwa. Mheshimiwa Waziri alitembelea vyanzo vya maji katika eneo la Kikombo, Miradi ya Maji ya Ving'awe, Mazae na kuzungumza na wananchi katika kijiji cha Chunyu. Nawashukuru Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe na Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa kwa kushiriki kikamilifu katika ziara hiyo. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, nina maswali ya nyongeza:- Kwanza kabisa, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa, nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa kufanya ziara ya Wilaya ya Mpwapwa kwa siku moja na kutoa maelezo ya matatizo ya maji katika Wilaya yetu ya Mpwapwea. Sasa, maswali;- Kwa kuwa fedha iliyobaki ya kukamilisha mradi ule wa maji kiji cha Chamanda na Igoji Kusini ni shilingi milioni 14; na kwa kuwa fedha hizi hazitoshi, mradi ule ili uweze kufanya kazi, unahitaji milioni 45.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ana maelezo gani kuhusu upatikanaji wa fedha zilizobaki ili mradi ule uweze kukamika na wananchi wa Chamanda, Simai na Igoji Kusini waweze kupata maji? Swali la pili, Je Mheshimiwa Naibu Waziri, anayo taarifa kwamba kijiji cha Igoji Kaskazini, hivi sasa kisima kile hakifanyi kazi baada ya mashine

yao kuharibika na wanapata maji toka kijiji cha Sazima, Je, Mheshimiwa Waziri atatusaidiaje ili wananchi hao waweze kupata huduma ya maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kiji cha Kigoji, sasa hivi ndio napata taarifa hii kwamba kijiji kile sasa maji hayatoki. Lakini, ninachoweza kusema ni kwamba wataalam watakwenda katika kijiji kile ili wafanye assessment ya ni kiwango gani cha uharibifu uliotokea ili tuweze kuchukua hatua mwafaka za kurekebisha. Kuhusu fedha zilizobaki kwa ajili ya kutengeneza miradi ambayo iliharibiwa, Mheshimiwa Lubeleje amesema inahitaji milioni 14 tu. Na mimi nasema fedha hizo zipo tayari kwa sababu Wizara ya Maji na Umwagiliaji, katika mwaka wa 2008/2009, nimfahamishe Mheshimiwa Lubeleje kwamba kwa utaratibu wetu wa *quick wins*, Wilaya ya Mpwapwa imepangiwa shilingi 149,380,000. Fedha hizi zikitumiwa vizuri, zikipangiwa vizuri, zinatosha kabisa kutengeneza hii miradi ambayo ipo katika Wilaya ya Mpwapwa. Kilichobaki tu ni Mheshimiwa Lubeleje kusimamia utekelezaji wa matumizi mazuri ya fedha hizi.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, na mimi pia nina swali la nyongeza. Kwa kuwa matatizo ya maji katika vijiji vilivyotajwa, yanafanana sana na matatizo ya maji katika kijiji cha Mpapa, Tarafa ya Nkonko, Wilaya ya Manyoni.

Mradi wa maji umekuwa ukisimamiwa na *World Bank*, lakini mradi huo yapata miaka miwili sasa bado haujazaa matunda na wananchi wale wameishi katika janga la ukame wa maji kwa muda mrefu; Je, Serikali inasema nini katika kuwaondoa wananchi wale katika matatizo hayo kwa sababu hata watoto wamekuwa wakipangiwea wakati mwingine muda wa kunywa maji? Ahsante!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpwapwa, Manyoni, kwa bahati nzuri nina habari njema kwamba katika utaratibu wetu wa *quick wins,* Halmashauri zote za Wilaya na Manispaa zitapewa fedha katika mwaka huu huu 2007/2008 hata kabla ya 2008/2009.

Tukichelewa kidogo, labda itaingia mwaka ule kwenye mwezi wa Julai. Na kwa bahati nzuri Wilaya ya Manyoni nayo imetengewa fedha. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mlata awe na subira kidogo kwa sababu mwezi wa Julai tutapata fedha.

Fedha hizi zitatumika kutengeneza miradi ile ya haraka haraka wakati tunasubiri maamuzi makubwa ya mradi mkubwa unaofadhiliwa na *World Bank*.

Na. 54

**Ukosefu wa Soko la Mifugo na Malambo**

**MHE. GOSBERT BLANDES** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Mkoa wa Kagera na hasa Wilaya ya Karagwe, Misenyi, Ngara, Muleba, Biharamulo, Bukoba Vijijini na Chato kuna mifugo mingi na kwa kuwa wafugaji hao hawana soko la uhakika la kuuzia mifugo yao pamoja na maziwa na pia kuna ukosefu wa malambo na majosho:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani kwa wananchi wa jimo la Karagwe kuwajengea kiwanda cha nyama na maziwa?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea wananchi wa jimbo la Karagwe malambo na majosho ya kutosha?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Gosbert Blandes lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kushughulikia mkakati wa masuala mbalimbali yanayohusu mifugo Serikali kupitia Wizara yangu imeweza kupitisha Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006 iliyoendana na utungaji wa Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006, Sheria ya Maziwa Na. 8 ya 2004 na sasa Sheria ya Ngozi na Ustawi wa Mifugo iko kwenye maandalizi. Aidha ili kuhakikisha suala hili linahusisha sekta binafsi, Bodi ya Nyama na Bodi ya Taifa ya Maziwa zimekwishaundwa. Natoa wito kwa wafugaji wa Karagwe wakishirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe kutumia Sera na Sheria hizo nzuri ili waunde umoja na washirikiane na sekta binafsi kuanzisha viwanda vya nyama na maziwa. Wizara yangu kwa upande wake itakuwa tayari kutoa utalaam na ushauri kila patakapohitajika. Aidha, kupitia *NARCO* wawekezaji wameonyesha nia ya kujenga kiwanda cha nyama katika Mkoa wa Kagera (Kyaka). Hivyo ni matumaini ya Wizara mara kiwanda hiki itakapojengwa wafugaji wa Karagwe na Kagera kwa ujumla watakitumia katika kuuza mifugo yao.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la ujenzi, ukarabati na uendeshaji wa majosho ni la Halmashauri, Wilaya ya Karagwe ina jumla ya majosho 25, kati ya hayo majiosho 12 ni mabovu na 13 ni mazima, lakini hayatumiki kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo ukosefu wa maji, udhaifu wa vikundi vya wafugaji katika kusimamia matumizi ya majosho na gharama kubwa za dawa. Majosho 5 yaliyokuwa mabovu katika vijiji vya Ihambe, Nyaishozi, Nkwenda, Kahundwe na Katera yamekarabitiwa kati ya mwaka 2005/06 na 2006/2007. Aidha, mwaka 2006/2007 chini ya *DADPs* fedha zilitengwa kwa ajili ya kujenga malambo mawili katika vijiji vya Kashanda kwa shilingi milioni 19.5 na Nyakagoyegoye shilingi milioni 11. Aidha, kwa mwaka 2007/08 jumla ya shilingi milioni 12. zilitumika katika ujenzi wa mabirika sita ya kunyweshea maji mifugo katika vijiji vya Bukangara (3) na Chamuchuzi (3). Nazishauri

Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe na zingine katika Mkoa wa Kagera, ziendelee kuweka kwenye mipango yao ya maendeleo miradi ya kuendeleza sekta ya mifugo *(DADPs)* ikiwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya masoko ya mifugo, malambo na majosho.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda nishukuru majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ametueleza kwamba Serikali kupitia *NARCO* inategemea kujenga kiwanda cha nyama Kayaka, Mkoani Kagera; ningependa kufahamu, ni lini kiwanda hicho kitajengwa na kitaanza kutumika. Swali la pili; kwa kuwa katika Jimbo la Karagwe kuna tatizo kubwa la wahamiaji haramu kutoka nchi jirani na pia kuna migogoro kati ya Ranchi ya Kitengule pamoja na wamiliki wake waliomilikishwa na Serikali. Je, Serikali inalijua hili? Kama inalijua, lini Waziri mwenye dhamana au Naibu Waziri watakuja kutatua matatizo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu, napenda kumpongeza Mheshimiwa Blandes kwa namna anavyofuatilia mambo ya mifugo katika Jimbo lake. Kwanza kabisa napenda kumhakikishia kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iko tayari kuwasaidia wananchi wa Karagwe na kuhakikisha kwamba kiwanda kinajengwa. Kufuatia hatua hizo, Wizara yangu imeishatangaza tenda ya kuwatafuta wawekezaji ambao watajenga viwanda vya nyma katika sehemu mbali mbali Tanzania. Kwa upande wa Kayaka Mkoa wa Kagera, tumeishatangaza na wawekezaji wameonyesha nia ya kuwekeza na sasa hivi kilichobakia, tunafanya mchakato kumpata mwekezaji. Lakini, kwa mwaka 2008/2009, *NARCO* nayo itapewa shilingi bilioni 3 kwa ajili ya kuanzisha viwanda vya nyama na kimojawapo kitakuwa Kayaka. Kwa hiyo, naamini kwamba baada ya mchakato wa kumpata mwekezaji, nina hakika kwamba *NARCO* itaingia nao ubia na kujenga kiwanda cha nyama katika Mkoa wa Kagera, upande wa Kayaka ambacho kitatumiwa na wafugaji wa Karagwe kuuza ng’ombe wao katika kiwanda hicho. Kuhusu matatizo yanayowakabili wananchi wa Karagwe kuhusu mambo ya mifugo, kuhusu wavamizi wanaotoka Uganda na sehemu zingine, tunayafahamu. Tumeishamwita Meneja wa *NARCO* kutoka kule, akaja akatueleza habari hizo na tukaagiza kwamba matatizo hayo yashughulikiwe. Lakini, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Blandes, Mbunge wa Karagwe kwamba, Mheshimiwa Waziri wangu ama mimi mwenyewe tunatarajia kutembelea sehemu hizo na kutatua hayo matatizo mara tu Bunge hili litakapoisha. *(Makofi)*

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa swali la msingi la Mheshimiwa Blandes la uwingi wa mifugo katika Mkoa wa Kagera, linafanana sana na wingi wa mifugo katika Mkoa wa Arusha na hasa katika Wilaya za Ngorongoro, Monduli na Longido; na kwa kuwa juzi nilikuwa huko Kenya, wanajenga kiwanda kikubwa sana cha nyama; na kwa kuwa wameanza kukataa mifugo kutoka Tanzania, wanahifadhi wenyewe wakisubiri kutengeneza hicho kiwanda; ni lini kiwanda kikubwa pia kitajengwa

katika Wilaya ya Ngorongoro ili kupunguza idadi ya mifugo inayokwenda Kenya na kuwanufaisha wakenya? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba Jimbo la Mheshimiwa Mbunge lina mifugo mingi. Lakini pia, kwa hali halisi ya Tanzania tuna mifugo mingi, nafikiri ni nchi ya tatu katika Afrika. Tanzania tuna ng'ombe milioni 18.5, mbuzi milionii 11.7, kondoo milioni 3.9, nguruwe miloni 1.7, kuku wa kienyeji milioni 33, kuku wa kisasa wanaofugwa zaidi ya milioni 20 mbali ya sungura, bata mzinga n.k. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hilo, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kupitia *NARCO* tumekwishatangaza tenda za kuweza kujenga viwanda sehemu mbali mbali. Kimojawapo ni kama ambavyo amejibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Lakini pia, kiwanda kingine kitajengwa Arusha, Ruvu na tuko katika hatua nyingine ya kutangaza kiwanda kitakachojengwa Mbeya na sehemu zingine. Ninaamini kabisa viwanda hivi vitakapofunguliwa na kujengwa na ndiyo maana katika jibu la Msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema katika bajeti ya mwaka huu, tumetenga rasmi bilioni 3 ambazo zitapelekwa *NARCO* kwa ajili ya kuhamasisha kujengwa viwanda ili mifugo yetu isiendelee kwenda nchi jirani na pato la mifugo liweze kuchangia katika pato la taifa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumebakiwa na muda mfupi na maswali bado tunayo. Tuwashukuru tu Mawaziri wenye dhamana ya vitoweo kwa majibu hayo mazuri kabisa. Sasa tunaendelea na swali linalofuata. *(Kicheko)*

Na. 55

**Kuwatambua na Kuwasaidia Watoto Yatima**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina utaratibu wa kuwatambua watoto walio kwenye mazingira magumu, kwa lengo la kubaini mahitaji yao ya msingi:-

Je, Serikali ina mipango gani ya kusaidia watoto hao ikiwa ni pamoja na watoto yatima wanaoongoza kaya?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji kwa kupitia bajeti ya Serikali na ufadhili toka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo imekuwa ikiendesha zoezi la kuwatabua watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi pamoja na mahitaji na matatizo yao. Baada ya kuwatambua

watoto hao jamii inawezeshwa kuweka mipango kazi ya kuwahudumia watoto hao ambao ndani yake wamo watoto wanaoongoza kaya. Aidha, katika jamii zimeundwa Kamati ambazo husimamia utoaji wa huduma mbalimbali kwa watoto hao ndani ya jamii husika. Baadhi ya watoto wamejengewa nyumba kupitia utaratibu huu. Mwelekeo wa Serikali ni kwamba watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira hatarishi walelewe na kukuzwa ndani ya jamii badala ya kuwatenga na kuwaweka katika vituo vya kulelea watoto. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo imeandaa mpango kazi wa taifa wenye makadirio ya huduma, malezi na ulinzi kwa watoto walio katika mazingira hatarishi. Tunashirikiana na mashirika na asasi mbalimbali katika kutoa huduma hizo. Mpango huu unalenga kutoa mwongozo na kufuatilia, kuratibu na kusimamia mwelekeo katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali zinazolenga kuwalinda na kuwahudumia watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi. Ni nia ya Serikali kuanzisha mfuko wa pamoja ukijumuisha bajeti ya Seriokali pamoja na mashirika na wadau. Kwa kipindi cha mwaka 2008/09 Wizara imetenga shilingi 260 milioni kwa ajili ya shughuli hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa rai kwa jamii na wananchi wote kwa ujumla kwamba suala la kulea watoto waishio katika mazingira hatarishi ni la jamii, kuwapeleka vituoni kulelewa liwe jambo la mwisho wakati juhudi nyingine zimeshindikana. Aidha, katika jamii upo utaratibu wa mama mkubwa ambao umeanzishwa kwa lengo la kusaidia upatikanaji wa huduma kwa watoto waliotambuliwa kuwa katika mazingira hatarishi ndani ya jamii husika. Katika jamii huteuliwa walezi ambao hutoa uangalizi wa karibu wakati wote kwa watoto walio katika kundi hili.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa majibu mazuri na naishukuru Serikali kwa juhudi kubwa ambazo wanafanya katika kusaidia watoto wa nchi. Swali langu lililenga sana Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, lakini kwa vile Serikali ni moja, nitaendelea na swali hili.

Kwa kuwa Wabunge wengi wanajiwa na watoto yatima wakitaka kusaidiwa watoto hao kulipiwa ada, karo na michango mingine hasa ya sekondari; Serikali inasema nini kuhusu kuwasamehe watoto yatima malipo, ada na karo hizo? Swali la pili, kwa vile ambavyo *UNICEF* kila mwaka huwa inatenga fedha na kuipa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa ajili ya kusaidia pamoja na mambo mengine, watoto yatima; hivi fedha hizi zinafanya kazi gani kwa vile katika Wilaya ya Kongwa sijawahi kuona fedha hizi zikifika huko?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza, ni kweli kwamba baadhi ya watoto wanawafuata Wabunge na watu wengine kuomba kuwasaidia kulipia karo na mambo mengine yanayohusiana na masomo. Utaratibu uliopo katika Halmashauri na kushirikiana na Wizara ya Afya, ni kwamba hawa watoto wote ambao wanaishi katika mazingira hatarishi huwa wanatambuliwa katika maeneo husika.

Natoa ushauri kwamba hawa watoto ambao wametambuliwa katika Halmashauri zao, waende kwenye Halmashauri husika ambako kule Serikali pamoja na wadau huwa tunatoa misaada pamoja na kuwasaidia kupata ada na mahitaji mengineyo, kwa hiyo watakapotambuliwa maeneo wanapoishi basi kule, wataweza kupata mahitaji hayo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *UNICEF* kutoa pesa na kwamba hajaziona huko Kongwa, ni kwamba *UNICEF* ni mojawapo ya wadau ambao wanasaidia Serikali ikishirikiana na wadau wengine na orodha iliyopo ni kubwa sana, hivyo inawezekana kwamba *UNICEF* katika hela anazopata huwa wanapeleka katika maeneo Ambayo wamepangiwa, na kwa sababu kuna wadau mbalimbali kwa ruhusa yako Mheshimiwa Mwenyekiti nitaomba nikuletee orodha ya wadau ambao wanatoa pesa hizi ili Waheshimiwa Wabunge iwasaidie waweze kuona ni wadau gani wanapatikana katika maeneo yao ili waweze kufuatilia na kujua kwamba ni wapi wanahudumia.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru sana, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nataka niulize swali dogo la nyongeza;

Kwa kuwa, tatizo la watoto la watoto wanaoishi katika mazingira magumu na hatarishi vipo kila eneo na kla Jimbo, na kwa kuwa tatizo hili lipo hata hapa nje ya mlango wa Bunge unapoingia unakutana na hawa Watoto hatarishi, Je Wizara inalijua hilo na kama inalijua hilo ina utaratibu gani na hao watoto wanaoishi hapa na wapo nje ya Bunge?

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu lakini watoto hatarishi? Ni watoto walioko katika mazingira magumu siyo watoto hatarishi, labda tuirekebishe hiyo(*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Killimbah kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokuwa nimejibu katika jibu langu la msingi ni kwamba Serikali ina mpango wa utambuzi wa watoto ambao wanaishi katika mazingira hatarishi, naomba nichukue tena nafasi hii kwamba ni lazima tuwafahamishe na tuwape uelewa Jamii kwamba watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi ni jukumu la jamii kwanza.

Lakini pili pale inapobidi kuwepo na msaada wa ziada basi inabidi kwanza watambuliwe na waweze kusaidia katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti hao watoto ambao wanaonekana wakiwa wanafuata nje ya geti la Bunge, mimi nadhani ni kuwapa tu maelezo kwamba wanatakiwa waende sehemu zao ili wakapate huduma katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile naomba niseme ya kwamba lile suala la kusema tunawapa senti moja moja pale mlangoni mimi nadhani huu siyo utaratibu mzuri, tunatakiwa tuwaelimishe ili waweze kwenda katika maeneo yao husika na wakifika kule watapata huduma zao badala ya kuwa wananing'inia pale getini.

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha naomba niruhusu swali la mwisho lililobakia, naomba nimwite Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o Mbunge wa Viti Maalum aweze kuuliza hilo swali la mwisho kwa siku ya leo.

Na. 56

**Ukiukwaji wa Haki za Mtoto**

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O** aliuliza**:-**

Kwa kuwa kumekuwapo na matukio mengi hapa nchini ya ukiukwaji wa haki za watoto kunako sababisha watoto kuteseka na kufanyiwa vitendo mbalimbali vya kikatili:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanzisha Kamati za kushughulikia masuala ya Watoto kwenye ngazi ya Vijiji, Kata na Wilaya?

(b) Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuanzisha kamisheni chini ya Wizara ili kutoa msukumo mkubwa wa masuala mazima ya watoto?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu**:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o Mbunge Viti Maalum lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika siku za hivi karibuni kumekuwepo na matukio mengi ya ukiukwaji wa haki za watoto kunakosababisha watoto kuteseka kwa kufanyiwa vitendo mbalimbali vya ukatili na unyanyasaji. matukio hayo yanawanyima watoto haki zao za msingi. Kwa kuwa Serikali za Mitaa zina Kamati za Huduma za Jamii, katika ngazi za Halmashauri, Kata, Mitaa hadi kwenye Vijiji. Wizara yangu inashauri Halmashauri ziimarishe na kutumia Kamati hizi kuratibu masuala ya haki za watoto. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa tunatoa mafunzo na miongozo kwa Maafisa Maendeleo Jamii wa Wilaya na Kata ili nao waweze kutoa mafunzo kwa Kamati hizo.

Kamati hizo zikipata uelewa wa kutosha zitakuwa na uwezo wa kudhibiti ukiukwaji wa haki za watoto katika maeneo yao. napenda kutoa wito pale ambapo Kamati hizi hazipo Halmashauri husika zihakikishe kuwa zinaundwa na kujengewa uwezo.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kuona umuhimu wa uratibu na usimamizi wa masuala ya watoto iliunda Idara ya Maendeleo ya Mtoto chini ya Wizara yangu Julai mwaka 2003. Idara hii kwa kushirikiana na wadau wa Maendeleo (*Development Partners)* wameanza mchakato wa kuunda Kamati ya Kitaifa ya Haki za Mtoto *(National Child Rights Committee)*.

Lengo kuu la Kamati hii ni kuratibu na kufuatilia shughuli zote zinazohusu Ustawi, Maendeleo na haki za Mtoto zinazofanywa na Serikali, Mashirika ya Kiraia na Wadau wengine.

Aidha, Pamoja na kuendelea na Mchakato wa kuunda Kamati hii, hata hivyo suala la kuanzisha kamisheni ya haki za watoto litaangaliwa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuonesha ari kubwa katika kufuatilia na kutetea haki za watoto.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

(1) Kwa Kuwa, ukiukwaji wa haki za watoto umekuwa unatokea mashuleni ikiwa ni pamoja na watoto kupigwa, adhabu za viboko, je Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba adhabu ya viboko inakomeshwa mashuleni ili kupunguza watoto kuumizwa na kuachiwa ulemavu wa kudumu?

(2)Kwa kuwa, hizi Kamati zilizotajwa zipo na zinaendelea kuwepo, na ukiukwaji wa haki za watoto umeendelea kufanyika kuanzia kwenye vijiji, familia, Je, Serikali ilipoamua kutoa namba za simu ambazo watoto wanapiga, je kwenye maeneo ambako hakuna mawasiliano ya simu watoto watumie mbinu gani, na wakati mwingine wale wanaowapiga au kuwanyanyasa ni walezi ama wazazi wao?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli bado kuna adhabu za viboko na kupigwa katika mashule yetu, lakini kama ninakumbuka kwenye miaka ya 1990 ama 2000 kulikuwepo na maelekezo kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwamba watoto wasipewe adhabu ya viboko shuleni, na kama inabidi apewe adhabu ya viboko ilikuwa ni lazima mzazi awepo na Mwalimu Mkuu wa Shule awepo na viboko visizidi viboko viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwamba kama kweli kuna Walimu ambao wanapiga watoto, ambayo ni kweli, basi ningependa kusema kwamba hilo ni kosa kwa hiyo anapomwumiza mtoto ni kosa la jinai na Walimu hawa kama watachukuliwa hatua za kisheria itakuwa ndiyo njia moja wapo ya kuweza kufanya *enforcement* ya maagizo ya Serikali, kwa sababu kutoa maagizo au Sheria bila *enforcement* itakuwa haijasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu la pili ni kama ifuatavyo; Kamati hizo zipo na bado ukiukwaji wa Sheria na haki za watoto unaendelea kuwepo katika jamii zetu, inatokea kwa sababu Kamati hizi zipo zimeundwa lakini hazijajengewa uwezo wa kutambua wajibu wao na mipaka ya utekelezaji wao wa kazi katika jamii yetu.Ningependa nitoe wito kwa Halmashauri zetu kwamba kama kweli zimechukua hatua za kuunda hizo Kamati basi hizi Kamati zipewe uwezo wa kuweza kuelewa kwamba haki za mtoto ni zipi na pale ambapo zinavunjwa wachukue hatua gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nirudie tena kutoa wito kwa Halmashauti ambazo bado hazina hizi Kamati za Huduma za Jamii pamoja na Kamati za Ulinzi ambazo najua kwamba zikijengewa uwezo zinaweza zikasaidia sana kupunguza unyanyasaji wa watoto katika ngazi ya kaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika familia wazazi wanaumiza watoto, lakini wale wazazi wanaoumiza watoto wao ni wazazi ambao nafikiri wana matatizo na wenyewe wanatakiwa wafanyiwe ushauri nasaha, ndiyo sababu tunasema kwamba hizi Kamati zijengewe uwezo wa kutoa ushauri nasaha ndiyo sababu kwamba hizi Kamati zipewe uwezo wa kutoa ushauri nasaha na kutoa adhabu pale ambapo Sheria ya haki za mtoto zinakiukwa?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba baada ya majibu mazuri sana Mheshimiwa Naibu Waziri niongezee majibu ya ziada kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba bado kwenye shule zetu Walimu wanatumia adhabu ya kuwachapa viboko wanafunzi, lakini naomba nitumie fursa hii kulieleza Bunge lako tukufu na kupitia Bunge lako kuwaeleza wananchi kwa jumla na hasa Walimu katika shule za Msingi na shule za sekondari kwamba, kutoa adhabu ya kuchapa viboko wanafunzi ni lazima izingatie Sheria ya elimu namba (10) ya mwaka 1978 na nyongeza zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wa kawaida hawaruhusiwi kuwachapa viboko wanafunzi, ni Walimu Wakuu peke yake ndiyo wanaoruhusiwa kuwachapa wanafunzi viboko, na viboko vyenyewe visizidi viwili, na kila mwanafunzi anapochapwa kiboko ni lazima rekodi ya kuchapwa mwanafunzi huyo iwekwe kwenye *register* ya shule ambayo inakuwa wazi kwa ajili ya ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana.*(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge kipindi cha maswali na majibu kimekwisha. Labda tu kwa kuzingatia kauli iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri mwenye

dhamana ya elimu ningeomba labda uchukue pia swali la nyongeza na la msingi la Mheshimiwa Job Ndunga. Hoja yake ya msingi pia ilikuwa ni Serikali kufikiria kuondoa ada kwa watoto wanaodhihirika ni yatima na wanaoishi katika mazingira magumu, nafikiri hilo pia labda mngelichukua ili kuona wakati wa Bajeti zenu mnaweza mkatusaidia kutujibu kwa taratibu zipi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, vilevile nimeombwa na Waheshimiwa Wabunge hapa wakati Mheshimiwa Naibu Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji akijibu swali la Mheshimiwa Martha Mlata, amesema kwamba utaratibu za miradi ya *quick wins* karibu utakuwa tayari kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge wameomba wagawiwe orodha ya miradi hiyo na taratibu zake na idadi ya fedha ambazo zitagawiwa katika kila Jimbo.

Baada ya matangazo hayo yanayotokana na maswali ya leo asubuhi, ninayo taarifa kutoka kwenye ofisi ya Mheshimiwa Spika, akiniarifu safari ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba atakuwa safarini kikazi kwa siku ya leo Dar es Salaam, lakini atarejea jioni na wakati atakapokuwa hayupo amemteua Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, kuwa Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni na atakaimu nafasi hiyo mpaka Waziri Mkuu atakaporudi siyo kipindi chote cha Bunge hili la Bajeti. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, vilevile nimepokea tangazo kutoka kwa *Assistance Chief Whip* wa Kambi ya Upinzani, ameomba niwatangazie Kamati ya Uongozi ya Kambi ya Upinzani kwamba kutakuwepo na kikao cha Kamati ya Uongozi ya Kambi hiyo leo baada ya kusitishwa kwa shughuli za Bunge saa Saba mchana katika ukumbi wa shughuli zao wa kawaida.

Waheshimiwa Wabunge kabla sijawatambulisha wageni, ninalo tena tangazo jingine la Kikao cha Kamati ya Katiba Sheria na Utawala, nimeombwa na Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, niwatangazie Wajumbe wa Katiba Sheria na Utawala kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo leo saa tano asubuhi, ukumbi namba 231 jengo la utawala. Kwa hiyo, Wajumbe hao tafadhali wahudhurie kikao hicho.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa pia na Mheshimiwa Dr. Wilbroad Peter Slaa, Mbunge wa Karatu na Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo tarehe 18 Juni, 2008 saa saba kamili mchana kutakuwa na Kikao cha Kamati katika ukumbi namba 219 ukumbi wa *Chief Kasusura* ghorofa ya pili jengo la utawala na Wajumbe wote mnaombwa kuhudhuria kikao hicho cha Wajumbe wa Kamati husika.

Waheshimiwa Wabunge ninayo orodha ya wageni wetu katika siku hii ya leo. Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi,

ameomba niwatambulishe kwenu Viongozi wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (*DARUSO*) kama ifuatavyo:-

Ndugu Ismail Emanuel, Kaimu Rais wa *DARUSO*, nadhani yupo hapa karibu sana, kuna Reginald Godchance Kaimu Waziri Mkuu, Mgeta Frank Spika wa Bunge la Wanachuo, Sijoverwa Tandika Waziri wa Mikopo, Rosemary Mushi Mjumbe wa Kamati ya *DARUSO* hao ndiyo wageni kutoka *DARUSO*. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge pia kuna wageni wa Mheshimiwa Yahya Kassim Issa kama ifuatavyo:-

Ndugu Hassan Mwinyi Bakari Katibu Uchumi na Fedha wa Wilaya ya Kati Unguja, Ndugu Hamis Mtumwa Jaku Mwenyekiti wa CCM tawi la Pongwe na Ndugu Fatma Ally Musa Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Duga Kiembeni.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa na Mheshimiwa Joyce Masunga, niwatangazie kwamba leo ana wageni nao ni watoto wake wawili ambao wapo hapa ndani ningeomba wasimame, karibuni sana na poleni sana kwa msiba mkubwa wa Babu uliowapata na karibuni tena Bungeni.

Nimeombwa na Mheshimiwa Bujiku Sakila, nimtangazie uwepo wa watoto wake, Wande, Mulya, Yemba na Lucy karibuni sana. Pia tunao wageni kutoka *NMB* Kanda ya Kati Dodoma ambao ni Bi. Lilian Mwinula na Bi. Zoe Kastiko, Meneja wa Tawi na Meneja wa Tawi la *NMB* Dodoma karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge Mwisho tunao wanafunzi 35 na Mwalimu wao kutoka shule ya sekondari ya Ilboru Mkoani Arusha. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge hayo ndiyo matangazo kwa siku hii ya leo na ninawashukuru kwa shughuli za asubuhi za maswali na majibu. Sasa naomba nimwite Katibu atuongoze katika shughuli inayofuata. Katibu endelea na *Order Paper*.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2007 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka 2008/2009

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge ninao orodha nyingine ndefu tunaendelea na mjadala wa hotuba kama tulivyoanza na msemaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani atafuatiwa na Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mwenyekiti wa Bunge.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza kwa siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niungane na wenzangu kumpongeza Waziri na timu yake kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kutuletea Bajeti pamoja na mapungufu mengi ambayo tumeyasahihisha ni matumaini yetu kwamba watayazingatia ya vianzio vipya ambavyo tumevipendekeza na kwamba watavifanyia kazi ili wananchi wa Tanzania waondokane na umaskini uliokithiri na zaidi rasilimali zao ambazo bado hawajafaidika nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mambo ambayo ningependa kuyasema ni kwamba katika bajeti tumeshauri kwamba eneo moja ambalo ni rasilimali za nchi ambazo bado wananchi hawajafaidika ni sehemu ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapendekezo ambayo tumeyatoa, tumeeleza kwamba uvuvi ungeweza kutuingizia bilioni nyingi za fedha ambazo hivi sasa hazikusanywi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha ni kwamba wavuvi wetu wadogo wadogo ndiyo wanaotozwa fedha nyingi kila siku na tunawaacha wavuvi wakubwa hawatozwi kitu chochote, bahati mbaya Serikali bado haijawapa nafasi wavuvi wadogo wadogo kuwasaidia na hata kuwasikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wetu wadogo wadogo ambao kwa bahati nzuri jana nilipata nafasi ya kuonana nao kutoka Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, Mara, Mwanza na Kagera.

Hapa wamenionesha stakabadhi za malipo wanayolipa kwa kila mzigo wa samaki wanaovua na kufika nao bandarini, wanalipa *royalty* au mrahaba waasilimia 5 kwa kila bidhaa ya samaki wanayoleta bandarini na hiyo inakokolewa bila ya kuangalia gharama zao ambazo wameingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazo risiti zao hapa, ninalo bando kubwa sana la risiti kuliko hili, lakini mbaya zaidi hawa wavuvi wadogo wanatozwa ushuru huu wakati meli zinazovua katika Bahari kuu hakuna hata moja inayotozwa hata senti moja ya ushuru.(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaizuliza Serikali inaposema inataka kupambana na umasikini unauchukua ukanda wote wa Bahari na maziwa yetu wavuvi wetu wote wanatozwa kodi kwa kipato kidogo wanachokipata, unaziacha meli kubwa ambazo zinachafua mazingira na kuchukua rasilimali, hawatumii hata kitu kimoja cha Tanzania, hawaajiri watanzania, wala si mafuta, wala si maji lakini unakwenda kuwakamua wavuvi wadogo wadogo na unasema unapambana na umaskini, hii *cluster* ya *MKUKUTA* iko wapi kwa wavuvi hawa (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya si mapungufu ya msingi kwamba Serikali yetu haijatizama kwa kina namna gani itamuondoa Mtanzania kwenye umaskini. Mbaya zaidi ni kwamba kila Mvuvi na kila mwenye chombo anatozwa ushuru na leseni. Kuna leseni ya mwenye chombo shilingi 5600/- na kila Mvuvi aliyeko katika chombo naye analipa shilingi 5000/-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni biashara gani tunaifanya ya kumkomboa Mtanzania, *are we serious*? Hakuna baharia hata mmoja wa kigeni anayetozwa ushuru hata senti tano, Watanzania wanatozwa fedha *whether* wamepata samaki ama hawakupata samaki wao wakifika pale wanatozwa fedha. Hujali gharama zao, kweli tuna imani na Watanzania hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya makosa hayo hayo kwa wakulima, tunafanya makosa hayo hayo kwa wachimbaji wadogo wadogo, mchimbaji mdogo wakati wote anahamishwa anapelekewa *FFU* na Makampuni makubwa tunakaa nayo juu ya meza na tunafanya *negociataion* nao, hapa hatufanyi haki kwa raia wetu (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo kimoja cha uvuvi kwa kawaida huwa kina watu kama 45, unakusanya shilingi 5000/- kwa kila mmoja, hajaenda kuvua hajui kama samaki atawapata ama hatapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baya zaidi ni kwamba Serikali inaandika kwa Wakurugenzi wa Halmashauri za Miji inawaambia kwamba ili kuzuia Uvuvi haramu wavuvi hawa wazuiwe iwapo watatumia vifaa vifuatavyo, wavu wa mtando, wavu wa ring net, kuzamia kwa kutumia miwani ya kupiga mbizi au mitungi ya hewa aina ya *oxygen*.

Mheshimiwa Mwenyekiti hiki ni kichekesho mimi sijapata kuona katika dunia yeyote kwamba *oxygen* inaharibu mazingira, eti mtu apigwe marufuku kutumia mitungi ya *oxygen* kwa sababu unaharibu mazingira, eti mtungi wa *oxygen* unaharibu mazingira watu wapigwe marufuku kutumia au viatu vile akivaa ndani ya Bahari akizamia vinaharibu mazingira navyo apigwe marufuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baya zaidi miwani wanayovaa ndani ya maji ili kuwaona samaki walipo nayo wanaambiwa inaharibu mazingira, barua yenyewe

haikuwashirikisha wavuvi wenyewe, imekwenda kwa Halmashauri moja kwa moja. Je wanawatakia mema watu hawa kweli, unataka watu hawa waishi kweli katika dunia hii ya Mwenyezi Mungu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi hawa wamejitahidi kwenda Wizarani kulalamika na bahati mbaya Sheria inawaambia wakichelewa ku-*appeal* kwa Waziri watazuiliwa kufanya kazi ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu zaidi ya 6000 watakuwa hawana ajira na sisi tumesema Serikali itapata ajira ya watu Milioni moja baada ya miaka mitano. Hivi hawa wanyonge wa Mungu wakale wapi, na waishi wapi? Barua iko hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera zinaweza kuwa nzuri kwa maana ya maneno, matamshi na majibu tunayojibiwa Bungeni. *(Makofi)*

Lakini hali halisi katika *field* ni tofauti, wananchi bado hatujakaa kitako kuwatatulia matatizo yao ya hali halisi waliyonayo hasa watu wa chini, wakubwa hawana matatizo, mikataba tutaunda tume saba na *consultant* atalipwa bilioni 85 ili wakubwa wasije wakaudhika eti kwa sababu wamewekeza Tanzania, lakini raia wa Tanzania yeye barua moja tu ya Mkurugenzi baada ya siku 30 amesimamishwa kazi zake na riziki yake imepotea, *are we doing justice to these people?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatembea kwenye viapo vyetu, tunawasaidia kweli Watanzania kuondokana na umaskini? Ninaomba sana Serikali rasilimali yetu ni Watanzania wetu, rasilimali yetu ni ardhi yetu na Madini yetu pamoja na mengine ndani ya nchi yetu, tusipige siasa tufanye kazi ya kuwasaidia Watanzania(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili mipango mingi ya Serikali imekwama kwa sababu ya utaratibu mbovu wa maamuzi. Katika dunia ya leo ambayo inakimbia, utaratibu wetu wa kufanya maamuzi katika Serikali unakwamisha mambo ya msingi kabisa.

Kuna kiwanda kimoja pale Zanzibar kimejengwa ni kama *plant* ya ku-*process* chakula cha kuuzwa ndani ya ndege huu ni mwaka wa nne wanabishana mwekezaji na *TRA*, wangeweza ku-*supply* chakula kwenye ndege zote na *contract* zipo, Waziri wa Fedha analifahamu, Serikali wanalifahamu, Makamishna wanalifahamu ni mwaka wa nne hujapata maamuzi mwekezaji, na Sheria hapa zinasema *within sixty days* mwekezaji awe amejua amekubaliwa ama amekataliwa, wanafika mwaka mzima hata majibu hawapati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunatumia fedha za Serikali kusafiri kuwaleta wawekezaji hapa, halafu wenyewe hatupo tayari kuwakaribisha wawekezaji hao tuna-*frustrate* tu. Sasa nauliza tunachotaka ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, naiomba sana Serikali, iharakishe utaratibu wa maamuzi, kama kuna sheria inasema siku 60 basi iwe ni siku 60. Anayepinga hiyo sheria achukuliwe hatua, maana sheria imepitishwa na Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne, sisi Tanzania nafikiri bado hatujajua ni vipi tunaweza tukabadilisha huu mfumo wa uchumi wetu. Moja ambalo litatusaidia ni kuwaiga wenzetu, lazima tu-*own* wenyewe hizi *projects* zetu. Njia za ku-*own* ni vile vyombo tulivyovianzisha, vifanye utafiti vimiliki, kwa mfano, unaitaka *NDC* iingie ubia na shirika lolote la nchi; kama *NDC* hawajafanya utafiti wakajua rasilimali zilizoko katika mradi watakaoufanya, wakimwachia mwekezaji aje aingie afanye utafiti na wao, *negotiation power* yao itakuwa ndogo. Utaziona nchi kama vile Dubai na wengine, wanafanya utafiti wa jambo wanalotaka, wanajua thamani yake halafu ndiyo wanamwambia mwekezaji njoo uwekeze. Leo sisi watu wanakuja wana-*determine* wanavyotaka wao, ndiyo maana Williamson tumeweza kuuza hisa 25 kwa dola 180,000 na dola 25 zilizobakia, zimeshatolewa sadaka leo. Hapo ndipo tulipofika Tanzania. Mwekezaji anasema kwa miaka 15 yeye anakula hasara, lakini hahami yupo na ana-*invest;* je, ana-*invest* vipi na akula hasara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kuanzia sasa tunaiomba Serikali, isiruhusu *investor* yeyote ku-*invest* bila ya kuwa na Mtanzania na asilimia isiyopungua angalau 15. Huwezi kuwaacha wageni wanachukua rasilimali za nchi wanaondoka, wanawaacha Watanzania wakiwa maskini. Lazima sasa Wabunge tujitahidi, Watanzania warasimishwe rasilimali zetu. Anataka mwekezaji aje tunamkaribisha na hatuna tatizo, lakini lazima uwe na *partnership* na Mtanzania. Mtanzania asaidiwe, asichukuliwe tu kama bendera; asaidiwe kuambiwa mali hii thamani yake ni kiasi fulani. Hili ndiyo tatizo ambalo lipo hivi sasa. Utakuta tumetoa maeneo ya madini, tuwapa Watanzania wengi leseni, lakini kwa sababu hawajui rasilimali iliyoko kwenye madini yenyewe, mtu anauza eneo la *uranium* kwa dola 15,000, 20,000. Anayewekeza anakuja kuchukua mamilioni, kwa kwenda kuingia kwenye *stock exchange,* Mtanzania anabaki na umaskini. Hatujamsaidia Mtanzania kwa kumpa leseni; msaidie Mtanzania kwa kujua rasilimali uliyompa ina thamani gani na yeye anaweza kuingia ubia na mtu kwa thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, nami niweze kuchangia katika Bajeti hii ya Serikali. Kwa kuanza, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Mawaziri wake. Vilevile naipongeza Serikali kwa bajeti nzuri, ambayo wametuletea safari hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ni nzuri na hasa baadhi ya maeneo ambayo tumekuwa tukiyapigia kelele, Serikali imeamua kuyatazama na kuyatilia maanani. Suala ambalo nitalizungumzia kwanza ni pale Serikali ilipoamua kuliangalia na kuliona eneo la utengemezi la bajeti yetu. Tumekuwa tukipiga kelele sana. Mimi nipo kwenye Kamati ya Hesabu za Serikali, yale mafungu yanapokuja michango ya wahisani kwa kweli tumekuwa tukiipigia kelele sana, wanatoa ahadi ambazo hawazitekelezi; suala hili linatuumiza na linaturejesha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Hesabu za Serikali, watakuwa mashahidi kwamba, mafungu mengi ambayo yanapata ahadi kutoka nje na hasa katika mafungu ya maendeleo, ahadi zile zimekuwa hazitekelezwi kwa baadhi ya maeneo kwa asilimia 100. Utaona kwamba, maeneo ambayo mara nyingi yanapata chochote ni yale ambayo hayana manufaa ya moja kwa moja kwa Mtanzania. Nina maeneo ambayo wahisani nadhani huwa wanaona kwao ni bora zaidi. Sehemu mojawapo ambayo imepata bahati kubwa sana katika michango hii ya Wahisani ni suala la UKIMWI. Suala hili limekuwa linapata mchango mzuri tu katika sekta karibu zote. UKIMWI unachangiwa vizuri sana.

Sehemu waliyoahidi miundombinu ya barabara, madaraja na maeneo mengine; tunapohoji na kuuliza kwa nini hili halijatekelezwa, jibu tunalopata ni kwamba bajeti zetu na zao haziendi wakati mmoja. Sisi wakati tunapoanza kusoma bajeti yetu katikati ya mwaka, baadhi ya wenzetu wengine ambao wanaahidi kutuchangia, bajeti zao wanasoma mwanzoni mwa mwaka na wengine katika robo ya mwanzo ya mwaka. Kwa hiyo, kutokuwa na uwiano mzuri, inapelekea wakati mwingine tunafika mahali zile fedha hatuzipati. Kwa kweli kwenye ahadi, hili si la msingi sana, huwa hatuoni msingi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri, kwenye ukurasa wa 21 kuna sehemu wanasema; hata hivyo upo, wasiwasi kwamba misaada na mikopo kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo haitapatikana kama ilivyoahidiwa kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 22, kitabu kinasema, utegemezi mkubwa wa bajeti kwa misaada ya wahisani ambayo haitabiliki, unaathiri mipango ya Serikali ya muda wa wakati na utekelezaji wa mpango wa kila mwaka. Kwa hiyo, ingawa bado tunahitaji misaada ya nje ni lazima tuanze mbio za kujitegemea. Hili nitaendelea kulisifu sana, ingawa kuna baadhi ya wenzangu wameonyesha wasiwasi katika eneo hili. Nasema ni bora tuanze kujitegemea kwa kidogo tulichonacho na tukawa na uhakika kitu gani tunakifanya, kuliko kupewa ahadi na sisi tusitoe chochote kwa tamaa kwamba, mwenzetu atatufanyia lile lakini mwisho wa mwaka, lile linakuwa halijafanyika na sisi hatukuweza kutenga chochote cha kusaidia suala lile. Kwa hiyo, huu mpango wa kuanza kujitegemea uwe endelevu. Zipo nchi za majirani ambazo zinajitegemea karibu kwa asilimia 100 na wala hakuna tatizo lolote wanaendelea na miundombinu yao ni mizuri. Kwa hiyo na sisi tuelekee huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika hili, hawa watendaji wetu wanaokwenda ku-*negotiate* na wahisani kwa niaba ya nchi hii; basi wawe waangalifu sana na misaada inayokuja. Hivi karibuni tulikaa na Mabalozi kwenye Kamati ya Hesabu za Serikali, wakati mwingine tunanyimwa misaada kwa ahadi ambazo watendaji wamekwenda kuahidi kule za ajabu kidogo.

Mtendaji amekaa na wahisani anawaahidi kwamba, ndani ya kipindi cha mwaka mmoja, tutakuwa tumeshawafunga mafisadi wanaofika kumi au watano. Sasa ahadi kama hii ambayo imefungamana na kesi za mahakamani; kwenda kupatana na wahisani kwa kweli wangeanza kuachana nazo, kwa sababu zimepitwa na wakati. Mambo haya yalikuwa yakifanyika wakati wa ukoloni, sasa hivi siyo wakati wake tena.

Sisi tuliwabana wahisani wale kwamba, ninyi mtatupaje ahadi? Wakasema hapana hizi hatutoi sisi ni wenzenu wanaokuja kuzungumza na sisi ndiyo wanaosema vitu hivi! Kwa hiyo, maadam utekelezaji haujafanyika, ndiyo maana tunaweza kuzuia misaada. Hili siyo zuri, halina afya na jaribu sana kuzungumza na watendaji; ahadi za aina hii waziepuke, kwa sababu ni za wakati wa ukoloni na sasa hivi tuko mbali sana na ukoloni. Wengi wetu tumezaliwa nje ya ukoloni, hazifai kabisa na waachane nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo nitaichangia ni misamaha ya kodi. Pamoja na kwamba, tumeanza mbio za kutaka kujitegemea, lakini vilevile nitaisifu hii bajeti kwa sababu imeliona tatizo zima la misamaha ambayo inatolewa katika maeneo mbalimbali. Misamaha mingi ambayo imekuwa ikitoka, haijawa na manufaa ya moja kwa moja kwa wananchi kwa sababu hawafaidiki nayo. Tumepewa asilimia ya misamaha inayotolewa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano. Nitawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, kama hili wameliona.

Naomba washirikiane na *TRA* ili kuweza kupitia upya ile misamaha na kuangalia umuhimu wa misamaha yenyewe. Hii si kwa Jamhuri ya Muungano tu, lakini hata ile misahama inayotoka upande wa pili wa Jamhuri, yaani upande wa Zanzibar ni vizuri ikaangaliwa na ionekane kama ina faida ambayo wananchi wanaweza wakaipata. Isiwe ni misamaha ambayo inalenga kuwatajirisha baadhi ya watu wanaotumia visingizio kupata misamaha, lakini ukweli na undani wake ilie misaada hawaitumii kama inavyopaswa.

Kwa mfano, wafanyabiashara wa vyakula kwa upande wa pili wa Jamhuri, yaani Zanzibar, misamaha ile ambayo wanapewa haiwanufaishi wananchi, kwa sababu vyakula bado bei iko juu sana na hawastahili kuvinunua kwa bei hizo ambazo waliopata misamaha wanauza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujitegemea, suala muhimu ambalo wengi sana walishalichangia ni miundombinu. Bahati nzuri, Wabunge wengi sana, wanaotoka upande wa Magharibi ya nchi wamelizungumza kwa sauti kubwa hili. Nadhani si vyema Serikali kutowasikiliza, kwa sababu upande ule tukiufungua, kuna nchi karibu nne ambazo Bandari ya Dar es Salaam, pamoja na Bandari ya Mtwara ni masafa mafupi sana kuliko kutumia bandari nyingine yoyote kama Kusini mwa Afrika au Afrika Kusini na kwingineko. Tuhakikishe kwamba, hicho kidogo tunachokipata, tunakiwekeza katika

miundombinu ya barabara na reli ili kuufungua upande wa Magharibi wa nchi na hatimaye kuweza kufungua biashara na nchi jirani za Congo, Rwanda na Burundi, kama ambavyo wengi wameshazungumza. Hili litakuja kutusaidia taratibu, lakini basi hilo liende sambamba na uimarishaji wa utendaji wa bandari zetu.

Bandari ya Dar es Salaam ni adha; unaleta kitu chako, *clearance* inachukua muda mrefu sana; unaleta *container* lako linachukua muda mrefu sana kuli-*clear*. Ukienda utapewa maelezo mazuri tu ya namna gani wanaweza wakafanya hiyo shughuli kwa haraka. Ushahidi ni nchi jirani zetu, ambao wangeweza kuitumia bandari ile bado wanaikimbia. Pamoja na mgogoro uliotokea Kenya, unategemea *alternative* ingekuwa bandari yetu sisi ya Dar es Salaam, lakini hata hivyo, bado Bandari ya Mombasa inakuwa muhimu, pamoja na umbali wake mpaka kuweza kuzifikia nchi husika.

Sasa pale panataka kazi ya makusudi kabisa, kwanza, uimarishaji wa miundombinu yake ili kuweza kufanya shughuli hizo kwa haraka, kwa sababu hayo yanawezekana kwenye nchi nyingine yanafanyika. Tusaidiane basi, Bandari ya Mtwara inahitaji nayo iimarishwe ili kuweza kufungua milango kwa nchi za Malawi na Zambia. Hii itasaidia ukuaji wa biashara na kukuza ajira. Watanzania wengi, watafanya kazi za kusafirisha mizigo kuweza kuifikisha huko inakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Zanzibar pia iangaliwe na pale ambapo Bandari ya Dar es Salaam itakuwa imeshashiba, tunaweza tuka-*off load* mizigo Zanzibar ikawa inasaidia kusubiri kuletwa huku na hatimaye kuweza kufikishwa huko inakotarajiwa kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wetu kwa asilimia karibu 80 unategemea zaidi kilimo. Wengi sana wameshalizungumza hili. Bahati nzuri jana nilikuwa namsikiliza Mheshimiwa Charles Keenja, alikuwa na mchango mzuri sana kwenye sekta hii ya kilimo na inaweza ikawa sehemu ya mapinduzi ya kilimo katika nchi. Tujitahidi kuangalia vitu hivi, kwa kuvipangia bajeti na kuweza kuvipa fedha inayostahili ili kuhakikisha kwamba, wakulima wetu nao wananufaika na bajeti ya nchi hii na wananufaika na pato linalotokana na kazi yao, ambayo inatokana na kutokwa jasho jingi sana juani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 20 imegusiwa tu kwamba, Tume ya Pamoja ya Fedha iwemo, lakini tunahitaji kujua zaidi; kitu gani kinakwamisha? Hiyo iliyofikiwa basi iwekwe wazi tujue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi nyuma kidogo, kwenye suala la misamaha ya kodi. Tufanye basi utaratibu wa kuweka wazi hiyo misamaha. Huyo anayesamehewa ni nani; tujue ije humu Bungeni. Wabunge wajue nani anasamehewa, ili aweze kukabiliwa huko, ikiwa msamaha ule hautumii vizuri kwa ajili ya kuwanufaisha wananchi na badala yake anautumia kwa ajili ya kujitajirisha yeye. Vilevile tuweze kuwajua pande zote mbili za Muungano; nani na nani wanasamehewa na kwa mantiki ipi na anatumia vipi msamaha ule kuwanufaisha walalahoi. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kengele ya mwanzo ilikwishalia, napenda kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura, niiunge mkono hii bajeti. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na Manaibu wake, lakini isiwe nzuri katika hiki kitabu tu, iwe nzuri vilevile kwenye utekelezaji. Waisimamie hii bajeti nzuri ambayo wametuletea ili iweze kufanya kazi na hatimaye mwakani wakija hapa, tuweze kuwapa pongezi zaidi kwa bajeti nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza, nimkumbushe tu Mheshimiwa Waziri azungumze na watu wa *TRA;* kuna tatizo kidogo katika masuala yanayohusu Muungano. Naomba pia mzungumzie tatizo la magari, bado ni adha ili kuona namna gani adha hii inaweza kuondoka.

Yupo Mbunge amekwishalichangia hilo, lakini mimi nalitilia mkazo tu kwamba, suala lile bado ni usumbufu mkubwa sana kwa wananchi liangaliwe na lipatiwe ufumbuzi ili wananchi waweze kujihisi kweli ni wananchi wa Jamhuri hii ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura nakushukuru sana na naiunga mkono hii bajeti. (*Makofi*)

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie katika hoja hii muhimu sana ya bajeti ya mwaka 2008/09. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na wasaidizi wake wote, pamoja na Taasisi ambazo zipo chini ya Wizara hii, kwa kutuletea bajeti nzuri, ambayo kama maoni yetu yatazingatiwa vizuri, ninaamini kabisa itaweza kuinua uchumi wa nchi hii na kuwasaidia Watanzania. Kwa kuzingatia hali ngumu ya kiuchumi dunia nzima na katika nchi hii na changamoto ambazo zinaukabili uchumi wetu, ninasema bajeti hii ni safi na ninawapongeza sana wenzetu wa Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema bajeti hii ni nzuri, kwa sababu imezingatia ugawaji wa uchumi wetu katika sekta kubwa nne, ambazo kwa kweli ni rahisi sana kuziratibu badala ya zile Sekta tisa walizokuwa wakizitumia siku za nyuma. Vilevile ni kwa mara ya kwanza, bajeti hii inapanga kutekeleza matumizi ya kawaida kwa fedha za ndani kwa asilimia 100 na tumepunguza utegemezi kama ilivyoelezwa katika hotuba hii, kutoka asilimia 42 hadi asilimia 34 kwenye bajeti ya mwaka huu. Hii ndiyo njia ya kuelekea katika kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpangaji mzuri ni yule ambaye anapata kidogo, anatumia kidogo zaidi na anabakisha sehemu ya kuwekeza kwa ajili ya kesho. Kwa hiyo, ninaamini kabisa zile bilioni 938 ambazo zitaingizwa katika bajeti yetu ya maendeleo, zitasaidia sana kuinua bajeti zijazo ili ziweze kutekelezwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikubaliane na rai ya Serikali kuwa, kuelekeza rasilimali zaidi katika maeneo yatakayokuza uchumi kwa haraka, ndiyo moja ya msingi mkuu wa kukuzia uchumi. Kwa bahati mbaya, rai hii ni ya maneno tu, haizingatiwi kwa

vitendo. Ninaamini kwamba, katika hizo Sekta Kuu zilizopangwa, Sekta ambazo ni muhimu na zitatufikisha haraka ni Kilimo na Miundombinu, hasa barabara za vijijini, kwani kilimo kinabeba maslahi zaidi ya asilimia 80 ya wananchi wetu. Kilimo na Miundombinu, vina nafasi ya kupanua ajira ndani na nje ya sekta hizo. Pia sekta hizi zitaongeza upatikanaji wa fedha za kigeni, kwa uuzaji wa mazao nje na kuweza kusafirisha bidhaa za wananchi kutoka huko vijijini hadi katika bandari na kusafirishwa kwenda nje. Kilimo kitatutatulia tatizo la ajira na miji kusongamana sana, kwa kuwa kitatoa ajira kule vijijini. Kwa hiyo, kupunguza msongamano Mijini. Kilimo kitatutatulia tatizo la njaa, ambalo sasa hivi ndiyo janga kubwa dunia nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba, inaelekea maneno yaliyosemwa ni mazuri, lakini uzito katika kupanga kwenye Sekta hizi haupo. Kwa mfano, kwenye bajeti ya mwaka 2007/2008, kilimo kilipangiwa asilimia 6.2 wakati Sekta nyingine zilipangiwa zaidi ya asilimia kumi na mahali pengine karibu asilimia 19.5. Mwaka huu kilimo kimepangiwa asilimia sita tu, si ajabu hata mchango wake katika Bajeti ya Taifa umepungua kutoka asilimia 5.7 mpaka asilimia nne. Kwa hiyo ni wazi kabisa, kwa sababu kilimo hatukukipa uzito, vilevile mchango wake katika Pato la Taifa unapungua kuanzia mwaka 2005 hadi mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kukigawia kilimo asilimia sita ni kwenda kinyume vilevile na tamko la Wakuu wa Nchi, lilitolewa mwezi Julai, 2003 kule Maputo *(The Maputo Declaration),* ambayo ilisema kwamba, kwa kuzingatia janga la njaa katika Bara hili, basi kila nchi katika bajeti yake ya Serikali, iweze kutenga si chini ya asilimia kumi. Sisi hapa leo tunatenga asilimia sita; kwa hiyo, inaonekana ni wazi kabisa, bajeti yetu hii haikuzingatia hata muono ule wa Viongozi wa Nchi za Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Fedha alisema, anategemea mchango wa Sekta Binafsi; hivi Tanzania tuna wakulima wangapi binafsi? Wakulima wengi ni wakulima wadogo wadogo ambao mpaka hivi sasa wanategemea zaidi msaada wa Serikali katika kuwapatia pembejeo, mitaji na kadhalika. Vilevile kama tunategemea wawekezaji binafsi kutoka nje; wengi huwa hawavutiwi na Sekta kama hizi za Kilimo na Miundombinu. Wanataka waende mahali ambapo watapata *quick wins* na huko ni kwenye viwanda, lakini siyo kwenye maeneo kama hayo ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo ni kwamba, tusitegemee sekta binafsi kuingia zaidi katika kilimo, badala ya kuitaka Serikali kuonyesha njia kwa kupanga kiwango kinachostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, mgao wa rasilimali katika Bajeti ya Maendeleo, hauonyeshi kuweka uzito kwenye maeneo ya utekelezaji. Kwa mfano, kati ya Bajeti ya Maendeleo ya shilingi 2,489,480 mwaka huu ni shilingi milioni 389 tu, sawa na asilimia 16, zimetengwa kwa miradi itakayosimamiwa na Mikoa na Serikali za Mitaa; kule ndiko utekelezaji ulipo. Kinyume chake, utaona kwamba kwenye Serikali na Idara zinazojitegemea huku Makao Makuu, zimetengwa 2,099,786 sawa na asilimia 84. Ningetaka kuuliza; hivi hii *remote control* itatusaidia?

Tupeleke fedha kule ambako ndiko kwenye utekelezaji. Hivi hiyo *D by D* iko hapa? Kwa kweli hii inaonyesha wazi kwamba, tunaangalia zaidi kwenye Mawizara, badala ya kuzipeleka fedha kule vijijini na kwenye Halmashauri ambako ndiko kwenye usimamizi. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa riba na mikopo ya benki za biashara nao hautoi uzito kwenye Sekta hizo mbili nilizozisema. Kwa mfano, mwaka 2007 kati ya mikopo ya 2,883,000 iliyotolewa, kilimo kilipewa asilimia 9.9 tu na usafirishaji ukapangiwa asilimia 7.0, wakati maeneo kama bidhaa viwandani vilipangiwa asilimia 19 na biashara asilimia 17. Hivi kweli tunatambua kuwa Kilimo na Miundombinu ndiyo zenye fursa kubwa za kukuza uchumi kwa haraka? Mimi nafikiri jibu ni kwamba, hatutambui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 42 ya Taarifa ya Hali ya Uchumi, inataka kuboresha usambazaji wa maji Mijini na Vijijini. Lakini azma hii haiungwi mkono kibajeti. Mwaka 2007/08, maji yalitengewa bilioni 309, mwaka huu kwenye bajeti hii zimepangwa bilioni 230.6 tu; hivi hapa tunasema nini; kweli tunathibitisha yale tuliyopanga kuyatekeleza kwa vitendo? Sikubaliani na sababu ya kukamilisha Mradi wa Shinyanga - Kahama kana kwamba, ndiyo basi na tatizo la maji limekwisha nchini. Maeneo mengi sana sasa hivi yana matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapiga kura wangu katika Mji Mdogo wa Kisarawe, umbali wa kilomita sita tu kutoka mpakani na Dar es Salaam, wapo katika matatizo makubwa sana ya maji na haya mambo yanatoka kila wakati hata katika Vyombo vya Habari. Huko Vijijini, hali imekuwa mbaya zaidi. Kwa hiyo, labda niseme tu nimetumwa na wapiga kura wangu kule Kisarawe, kama katika bajeti hii pale Kisarawe Mjini ambapo wanataka milioni 300 tu za kuweza kununua mashine na kutengeneza vyanzo vya maji hawatazipata, nimeambiwa nisiiunge mkono hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa heshima ya Chama cha Mapinduzi na mimi nikiwa mkereketwa wa Chama hicho, hotuba hii nitaiunga mkono. Bali naomba nitoe tahadhari kwa Waziri Mkuu na Waziri wa Maji, katika bajeti zao nisipopata jibu la kuridhisha, nasikitika kwamba, nitatekeleza hii amri ya wapiga kura wangu na sitounga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya vikwazo vikubwa katika uchumi wetu ni riba ya juu ya mikopo toka Benki za Biashara. Wenye uwezo wa kudhibiti riba ni Serikali na Benki Kuu. Kama tulivyoelezwa katika hotuba hii kuwa mwaka uliopita ni Serikali kwa kupunguza mikopo ya ndani na Benki Kuu kusimamia vizuri ile Sera ya Fedha, kuliweza kupunguza riba kutoka asilimia 16 mpaka 15. Mimi ninaishauri Serikali na Benki Kuu, waendelee kuzingatia maeneo hayo ili ile riba ishuke na hasa kwa ajili ya kukopesha wakulima wadogo wadogo vijijini, waweze kukopa na waweze kuzalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu marekebisho ya mfumo wa kodi, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kulenga maeneo ambayo yatawaletea watu wa chini unafuu. Punguzo hilo, halitawafikia wale walengwa pasipokuwa na usimamizi mzuri.

Kwa hiyo basi, zile mamlaka za kuratibu na kusimamia kama vile *EWURA* na *SUMATRA,* hapana budi zipewe maelekezo ya kutosha, ziweze kusimamia vizuri kuona kwamba hili punguzo lililoonyeshwa kwenye bajeti hii ni kweli linatekelezwa na wafanyabiashara wanaotoa huduma. Yakifanyika haya, ninaamini kabisa mwananchi wa chini kule ataona kwamba, punguzo la kodi kwa kiwango cha chini na mapunguzo mengine yaliyoonyeshwa mle ndani ya Hotuba ya Waziri, yanaweza yakawanufaisha na wao wakaweza kutekeleza majukumu yao kutokana na bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa nipigiwe kelele ya pili, la msingi nasema kwamba, bajeti ni nzuri lakini kuna maneno zaidi kuliko vitendo. Tafadhali, ningeomba bajeti ionyeshe kwamba, maeneo ambayo ndiyo yenye nafasi ya kuzalisha, ndiyo yanayopewa umuhimu; maeneo kama Kilimo, Miundombinu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru. Ahsante sana na naiunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii, niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi ya mwaka 2008/09. Kwanza na mimi nianze kwa kuwapongeza Waziri, kaka yangu, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Manaibu wake; Mheshimiwa Jeremiah Sumari na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na Katibu wa Wizara hiyo, kwa kuandaa bajeti hii vizuri sana na kuiwasilisha vyema hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba, katika *Monetary Policy Statement* imetueleza kuwa, *GDP* imekuwa kufikia asilimia 7.1 toka asilimia 6.7 iliyokuwa mwaka 2006 na *projections* zinaonyesha kwamba itaendelea kukua. Kwa hiyo, uchumi wetu utaendelea kuwa nzuri. Naomba nitoe pongezi sana kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Monetary Policy Statement* pia imekiri kuwa, kushuka kwa uchumi wa dunia na kupanda kwa bei za mafuta na upungufu wa chakula duniani, kutaathiri mwenendo mzima wa pato la ndani la Taifa na mfumko wa bei. Sasa kwa mujibu wa mwenendo wa kufikia lengo la Mkakati wa Kupunguza Umaskini ifikapo mwaka 2025, kwa miaka hii kumi na saba na nusu iliyobakia, tuna changamoto kubwa ya kuhakikisha ukuaji wa ongezeko la watu la asilimia tatu kwa mwaka, linaendana sambamba na ukuaji wa kipato cha wastani kati ya asilimia saba na nane ya *GDP* kwa kipindi hiki cha miaka kumi na saba na nusu. *Any drop* ya *rate* hii ya asilimia saba na nane ya *GDP* kwa mwaka wowote ule, wachumi wanasema hatutafikia lengo. *(Makofi)*

Wataalam wanatuambia nini, hasa tukiangalia hali hii ya mabadiliko ya uchumi wa dunia; je, haita-*affect* mwenendo mzima wa mipango yetu? Je, wanatuhakikishia zile *priority programmes* zitakuwa *adequately funded?* Je, pato la mwananchi wa kawaida mkulima kule Namtumbo litakua?

Ushauri wangu ni kwamba, lazima kuwepo na usimamizi wa zile *guidelines* zinazo-*facilitate strategic resources allocation* katika changamoto zinazohusiana ili

kuweza kupata njia ya kuweza kukuza uchumi wa nchi yetu na kwenda kuelekea kuwa uchumi wa tatu mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wote waliozungumza hapa, wamezungumzia kilimo; kila mtu amelia na kilimo kwa staili mbalimbali. Kwa hiyo, tulichokuwa tunaiomba Serikali; itambue kwamba sasa wakati umefika wa kuongeza Bajeti ya Kilimo, ifikie asilimia angalau kumi ya Bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeelezwa kilimo kimeshuka katika uchangiaji wa Pato la Taifa na kwamba, sekta zinazoongoza katika Pato la Taifa ni Utalii, Mawasiliano na Madini. Ukitazama kwa ujumla, sekta hizi zinasaidia uchumi mkubwa. Kilimo ni Sekta ambayo inaisaidia nchi na wananchi wake katika ajira na pato lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amani ya nchi yetu na *political stability,* inachangiwa sana na usalama wa chakula wa nchi yetu na ajira iliyopo katika kilimo, ndiyo maana tunakuwa na *political stability* na amani ya nchi yetu. Iwapo hakuna chakula na hakuna ajira ya kutosha kwa wakulima wetu, nchi yetu itayumba. Kwa hiyo, naomba Serikali iendelee kusimamia kwa vitendo, uzalishaji wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa cha mwaka 2007, ukurasa wa pili *paragraph* ya nne inasema: "Kupungua kwa mchango wa shughuli za kiuchumi katika kilimo, hakumaanishi kupungua kwa uzalishaji katika kilimo, bali inaashiria kuongezeka zaidi kwa shughuli za kiuchumi katika maeneo mengine."

Ni kweli maeneo mengine, shughuli zake za kiuchumi zimekua, lakini nasema kwa mfano mdogo nilionao wa mkoa wetu wa kilimo ambao unategemewa sana kwa zao la mahindi, uzalishaji wake umeshuka. *(Makofi)*

Mwaka 1996/97 hekta 124,000 zililimwa na mapato yake yalikuwa ni tani 299,328; mwaka 2006/07 hekta 126,987, ongezeko la hekta karibu 2,900, lakini mapato ya zao la kilimo yalikuwa ni tani 230,422. Ukitazama kuna tofauti ya tani zaidi ya 60,000 zilizopungua za uzalishaji wa mahindi. Kwa hiyo, tunaomba hapa wataalam watazame, najua wametazama kwa ujumla. Katika maeneo hasa ambayo yanategemewa kwa chakula kama Mkoa wa Ruvuma, mwaka 2006 zimepungua zaidi ya tani 60,000 za mahindi ya chakula. Kwa hiyo, lazima utafiti ufanyike, iangaliwe kwa nini mazao haya yamepungua. Ukitazama kwa haraka, unakuta mbolea imekuwa ghali sana. *(Makofi)*

Mbolea zimekuwa ghali, wakulima nao wanashindwa kutia mbolea ya kutosha katika mashamba yao. Sasa tuangalie sana, tunaishukuru Serikali mwaka huu imeongeza ile bajeti ya ruzuku ya mbolea, kutoka dola milioni 20 mpaka bilioni 31.8. Tuangalie kwa undani pia mbolea duniani zimepanda; kupanda kwa mbolea duniani hakutaleta *impact* sana kwa hizi bilioni 10.8 zilizoongezeka. Sasa tunachoomba, Serikali i-*concentrate* kupeleka mbolea hizi kwenye maeneo ambayo yata-*produce* chakula cha kutosha, kwa sababu hakuna chakula duniani. Mwaka 2007, Serikali ilitoa kibali cha tani

300,000 za mahindi kwa wafanyabiashara, lakini wameleta tani 800,000 tu za chakula hapa, kwa sababu hakuna chakula duniani.

Sasa tunaiomba Serikali, mbolea hii i-*concentrate* kwenye ile Mikoa inayozalisha ili kuleta *impact.* Tusipopeleka mbolea ya kutosha kwenye mikoa inayozalisha chakula kama Ruvuma, tutaathiri na hatutaleta *impact.* Tuwekeze ili tuweze kupata majibu mazuri. Serikali yetu imewekeza kwenye mpira, ndiyo maana leo tunaona matokeo mazuri ya mpira. Kwa hiyo, tuwekeze na kwenye kilimo. Serikali imeleta Maximo pale, ameleta mpira mzuri na leo tunaburudika. Tunaamini kabisa yale ni matokeo ya kuwekeza kwenye mpira. Tunaomba, ili kuleta *impact* basi tuwekeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru sana Serikali kwa kuweka mazingira mazuri kwa mkulima na miundombinu ya barabara, umwagiliaji na kadhalika. Mazingira haya bado hayatoshi, nilikuwa naomba katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 30 *paragraph* ya 44(a) anasema, sehemu kubwa ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya kilimo, zitaelekezwa katika ruzuku ya mbolea, hifadhi ya chakula *(SGR)*, utafiti wa mbegu na mafunzo. Tulikuwa tunaomba sana, katika haya mafunzo, Serikali iwekeze kusomesha vijana ambao watakuja kufundisha elimu ya ugani watakaokaa vijijini, kwa ngazi ya cheti, ambao watawafundisha kwa vitendo wakulima wetu ili kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *training in good farming practice* ni muhimu sana, katika kupata zile *inputs* ambazo Serikali na mkulima wamewekeza. Mkulima kama hana elimu ya kilimo cha kisasa, hawezi kuzalisha vizuri. Nashauri Serikali iwekeze kwa vijana wapya, kwa kuwapatia elimu hii ya ugani na watakaa pale vijijini na kutoa elimu kama walimu wa *Grade A* wanavyopewa elimu ya cheti na kukaa kule. Kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali iwekeze kwenye hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nitakuwa mnyimi wa fadhila kwa wakulima wa tumbaku nisipowazungumzia. Katika utaratibu wa bajeti yetu, tumeona kwamba, sigara ni moja ya *product* ambayo inachangia sana uchumi wa Taifa letu. Sigara hii chanzo chake ni tumbaku. Mwaka jana sigara imechangia bilioni 90 *in land revenue.* Mwaka jana *export* ya tumbaku imechangia pato la *foreign exchange 89,986,000 dollars,* lakini bado mkulima wa tumbaku hajaangaliwa vizuri. Taasisi inayoangalia uzalishaji wa tumbaku kisheria, bado haijaangaliwa vizuri ili kuweza kusimamia uzalishaji. Tusiongeze tu kodi, lakini uzalishaji ubaki pale pale. Tuangalie kuongeza uzalishaji ili kodi ziongezeke zaidi, tusitoze kodi nyingi lakini tumbaku zao lake lizalishwe kwa wingi kwa kuangalia uzalishaji na pato letu tunaamini litakuwa kubwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nitaishukuru sana Serikali, ikiangalia taasisi ambazo zinasimamia uzalishaji wa zao hili la tumbaku ili tuweze kusimamia vizuri uzalishaji huo na kuweza kuongeza Pato la Taifa. Viwanda vinavyo-*process* tumbaku, *capacity* yake ni *78,000 tones,* lakini tumbaku inayozalishwa ni *54,000 tones.* Kwa hiyo, bado kuna *deficit* kubwa hapa ya uzalishaji wa tumbaku. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali iangalie, tuwekeze ili tupate zaidi. *Simple mathematics;* moja jumlisha moja unapata mbili. Tunaomba sana

Serikali iwekeze, tuweze kupata zaidi na tuweze kuchangia uchumi wa Taifa letu kwa uzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii. Naomba kwa mujibu wa kumbukumbu, niseme naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Vita Rashidi Kawawa na kama Mwenyekiti wa Bodi ya Tumbaku, ulipaswa uliseme hilo ili kuweka mambo yako sawasawa. Baada ya kukusikiliza, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe na Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro ajiandae.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja zilizopo mbele yetu. Naanza kwa kuipongeza Serikali, kwa jitihada zake za kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi, ndani ya nchi yetu. Jitihada hizi zimekuwa zikionekana kwa ile mipango na mikakati ya mara kwa mara, ambayo Serikali inaiandaa kila siku. *(Makofi)*

Mipango yote hiyo, ina lengo la kuondoa matatizo ya Mtanzania. Kumekuwa na mipango; MKUKUTA, MKURABITA, MKUMBITA, *Mini-Tiger Plan, TASAF* na mipango mingine mbalimbali ya kuwawezesha wananchi kiuchumi, yote hayo yanalenga kuleta maisha bora kwa Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina matatizo makubwa, sote tunaelewa na si rahisi kabisa matatizo hayo kuondoka kwa muda mfupi. Hii ni kwa sababu hata nchi zinazoendelea, tunasema nchi za huko duniani na wao bado wana matatizo yao ya kiaina. Kuna matatizo ya ukosefu wa ajira huko pia, lakini vilevile kuna umaskini wa aina ya kule ambao hatuwezi kuulinganisha na wa kwetu. Hata omba omba wapo kule, lakini wanaomba kwa staili ya Kizungu; anachukua gitaa, anakaa pembeni anaimba na kucheza, wewe unasema huyu baba amekaa hapa anatumbuiza, kumbe anaomba. *(Makofi)*

La msingi ni kuangalia namna gani Serikali imejipanga kutatua matatizo haya ndani ya nchi yetu. Ndiyo maana Serikali imekuja na bajeti hii, ambayo kila mtu anasema ni nzuri. Wale wanaonuna na kukereka kwa kuwa tunaisifu Bajeti ya Serikali, waendelee kufanya hivyo, lakini sisi tunajumuika na Watanzania walio wengi kuisifia bajeti yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutatua matatizo ya Tanzania, inahitaji kiwango kikubwa cha fedha na kuona ni namna gani fedha hizi zitatumika. Kwa hiyo, naomba Serikali itumie fedha hizi kama ilivyopangiwa, vinginevyo, hatutaelewana humu Bungeni. *CAG* ameshapewa meno, afanye kazi yake vizuri; alete ripoti yake kama kutatokea upungufu wa fedha au ubadhirifu, Wabunge hatutakuwa na mswalie Mtume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema bajeti ni nzuri hasa ukiangalia maeneo yote mawili yanayohusiana na bajeti. Tukija eneo la kodi; kwanza, ninaipongeza *TRA* kwa kazi nzuri ambayo inaifanya ya kukusanya kodi. Hii inaonekana dhahiri, tukiangalia kile

kigezo cha *tax effort* tumeona *trend* yake inavyokuwa. Mwaka 2006/07 ilikuwa ni asilimia 14.3; 2007/08 asilimia 16.7; na 2008/09 tumekadiria kukusanya mapato kwa *GDP* asilimia 18.5; hii ni *trend* nzuri. Inaonenyesha *TRA* inavyofanya jitihada na kwa maana hiyo, ndiyo Serikali itaweza ku-*finance recurrent expenditure* yake, kwa kutumia mapato ya ndani. Hii ni lazima Serikali ya Chama Tawala tujisifie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kwenda kuomba mkopo kwa ajili ya ku-*finance* matumizi ya kawaida. Hii ni sawa na baba aliyeshindwa kuilisha nyumba yake, anakwenda kwa jirani kuomba chakula; hiki ni kitendo cha aibu. Tutafute fedha za nje kwa ajili ya ku-*finance* miradi ya maendeleo na ile miradi ambayo tutakuwa na hakika baadae itakuja ku-*generate* mapato ili tusiwape mzigo wa kulipa kodi wajukuu zetu na watoto wetu, kwa kuwa tumekopa pesa na kuzitumia kwa mapato ya ndani; Miradi ambayo italenga uwezo wa kutoa mapato na baadaye tukalipa deni ambalo tumelikopa ni kwa kuweka kwenye sekta hizo ambazo ni za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna marekebisho ya mfumo wa kodi; naipongeza Serikali kwa kuliona hili. Sasa hivi tuna wakati mgumu, kila mmoja amezungumza hapa; mfumko wa bei umesababisha bei ya mafuta kupanda. Kwa hiyo, ndiyo maana Serikali ikaona basi tuweke kodi kwenye kima cha chini cha mshahara na kwenye *tax bracket* nyingine zile zinazofuatia kodi ili kusaidia angalau kuchuchua kwa lugha ya kwetu Kisiwani; ile *disposal income* ya hawa wahusika. Ninaiomba Serikali hapa ipige *calculations,* tuone *real term* ni kiasi gani hasa wamesaidia waliopunguziwa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tunazaana sana. Mwenyekiti wangu wa CCM wa Mkoa wa Lindi amesema, Watanzania tunazaa kama kompyuta, kwa maana kompyuta ukiipa *comand print* inafyatua tu zile *documents.* Kwa hiyo, tuna wategemezi katika familia kwa asilimia kubwa sana.

Kwa hiyo, kupunguza kodi katika kipato wakati huu wa dhiki ya chakula na mfumko wa bei, itaweza kusaidia Watanzania walio wengi, ambao katika familia pengine mmoja au wawili ndiyo wafanyabiashara au ndiyo wanaopata mshahara, wengi wanawategea wale. Kwa hiyo, itakuwa imewasaidia walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imepunguzwa kodi katika pembejeo na zana za kilimo na hii itawasaidia wakulima wengi kupanua kilimo, hasa kwa wakati huu. Nije kwenye kodi ya mafuta. Kodi ya mafuta haikuongezwa katika kipindi hiki, imekuwa *freezed.* Naipongeza Serikali kwa hilo na kodi haikuondolewa, imebakia katika kiwango kile cha mwaka jana.

Nia na madhumuni ya kutoza hii kodi tuliyoizungumzia mwaka jana kwenye bajeti, bado ingalipo. Tumeambiwa tutatozwa kodi kwenye mafuta, ili kupata mapato ya kutengenezea barabara zetu na tatizo la barabara bado lipo. Suala la msingi hapa, tunaiomba Serikali itupe takwimu itueleze ni mapato ya kiasi gani yamekusanywa kutoka kianzio hiki cha mafuta na kiasi gani cha pesa kimetumika kutengenezea barabara na ni

barabara zipi. Kwa sababu sasa hivi hatutaki *statements* za kisiasa, tunataka *statements* za kiutendaji. Mmelitenda vipi hili mtueleze? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine lililochukuliwa ni kupanua wigo wa kodi, ambalo ni suala zuri tu. Watanzania wachache kabisa ndiyo wanaolipa kodi, lakini tupo wengi tu. Kwa hiyo, kupanua wigo kutasaidia kutowa *relief* kwa wale wachache ambao wanalipa kodi. Vilevile kuna sekta isiyo rasmi, bado haijaguswa kabisa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ikiwezeshwa kwa sababu kuna *principle* ya kodi ambayo inasema *ability to pay;* hatuwezi kuwakata kodi kama hawajawa na uwezo wa kulipa kodi. Kwa hiyo, Serikali iiwezeshe sekta isiyo rasmi, iendelee kuwawezesha wajasiriamali wafikie kiwango cha kuweza kulipa kodi ili nao wachangie kulipa kodi katika nchi hii. Siyo *fair* kutumia huduma ambazo zinalipiwa kodi na walipa kodi wengine, lakini wengine tukawa tunatumia tu bila kuchangia chochote. Sote tushiriki katika kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema bajeti ni nzuri kwa maeneo yote mawili; nimegusia yale ya kodi, sasa nakuja maeneo ya kipaumbele. Maeneo ya kipaumbele yamechaguliwa, kwa kuangalia matakwa ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ambayo tumeiuza kwa wananchi na wakatupa kura nyingi zaidi na Chama cha Mapinduzi kikawa madarakani. Kwa hiyo, ni sahihi kabisa hivi vipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo mengi ya elimu, ambayo wenzangu wengi wamekwisha yazungumzia. Shule tumezijenga katika Kata zote na tunaendelea kuzijenga, lakini kuna matatizo makubwa ya walimu; yaani ni jambo zito kabisa, unaenda kwenye shule unamkuta mwalimu mmoja au wawili. Walimu wanapata kizunguzungu, wanajiuliza nipangie ratiba gani mimi ya kufundisha watoto hawa na nipo peke yangu! Hili ni suala la msingi linalohitaji kuzingatiwa. Wengine wamesema, hata madawati na maabara hakuna ni kweli, mambo mengi tu yamekosekana. Kwa hiyo, naomba twende kama tulivyojipangia; hela ziende ku-*finance* mambo hayo.

Nakubaliana kabisa na Serikali kuwa, kipaumbele chetu cha pili kiwe ni miundombinu. Nakubaliana nao pia kwa kusema kuwa, kipindi cha bajeti hiki hatutaanzisha miradi mipya; kwa sababu tumekuwa tukiweka hii miradi kisiasa, tunawapa matumaini wananchi lakini tija haipatikani. Umetengeneza barabara hapa nusu umeacha, kesho pale umetengeneza robo barabara, kesho kutwa pale umechimba chimba kidogo tu. Unawapa matumaini kwa kuweka miradi mingi na si danganya toto, kusema kwamba, tunajenga barabara umeacha lakini hatimaye haimaliziki na wala manufaa hayapatikani. Kwa hiyo, ni sahihi kabisa safari hii kushughulikia ile miradi ambayo tayari imeshaanza inaendelea. Tuimalize ili iishe, watu wanufaike na zile barabara na mwakani tuingie katika miradi mingine. Nayo twende nayo iishe, hatimaye matunda yataonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani kabisa na kupunguzwa kwa bajeti ya maji. Mimi ni Makamu Mwenyekiti wa ile Kamati ya Kilimo na Maji. Matatizo ya maji yapo. Lile suala la kuambiwa kuwa maji yamepunguzwa kwa sababu mradi umemalizika,

sikubaliani nalo. Bajeti ingebakia kama mwaka jana, *priority* ya watu ni maji; tafiti zinasema hivyo. Bajeti ya Maji mwakani lazima iongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala yanayohusu Zanzibar; mwaka jana nilizungumza hapa na mwaka huu nitazungumza na mwakani nitazungumza vilevile mpaka nimalize kipindi changu cha Ubunge, labda kuna siku moja Serikali itasikia na kuyazingatia. Tumesema kuna mambo mengine lazima tufikiriane, kwa mfano, kuna kodi ya mapato ya wafanyabiashara na Watumishi wa Serikali ya Muungano ambao wapo kule Zanzibar. Tumeomba basi kodi ya mapato ibakie kule, kwa sababu huduma wanatumia za kule; kwa nini wale walipa kodi wa Serikali ya Mapinduzi ndiyo walipe hizi huduma na wao wasichangie; kuna ugumu gani?

*Corporataion tax* kwa yale makampuni ambayo matawi yake yako Zanzibar; kwa nini ile kodi isibakie kule? Wanatakiwa wafunge *final account* zao kule, ijulikane faida waliyopata kwenye zile *branches* asilimia 30 ibakie kule Zanzibar, waendelee kupata *service* na mchango wao wa kodi wakiwa wameutoa.

Suala lingine ni kuhusu *VAT* katika haya makampuni ya simu. Kuna minara mingi ipo tu kule; sijui *Vodacom, TIGO* na kadhalika, kodi ibakie kule hata kama zimekuwa *registered* Tanzania Bara. Kwa *Zantel* ambayo imesajiliwa kule Zanzibar nayo ilipe huku; ngoma *draw,* kuna tatizo gani? Mimi silioni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ada ile inayoitwa *Safety Fee,* ambayo inatozwa *airport;* shilingi 1,000 kwa raia na dola tano kwa *foreigner;* nayo kwa nini isibakie kule Zanzibar ihudumia vile Viwanja vya Ndege vya Zanzibar ambako kuna matatizo ya mapato?

Tunashukuru *TRA Office* ya Zanzibar ni nzuri; watumishi sasa wameanza kuajiriwa wapo pale wanafanya kazi nzuri. Tunawapongeza vijana wetu, lakini tunahitaji *IT Officer* na Mwanasheria, tutafutiwe hao wapelekwe. Sasa hivi tuna-*deal* na makampuni makubwa makubwa ya nje, hoteli kubwa kubwa na *Multinational Companies* yanakuja pale. Wanakuja na Wanasheria wao, wanafika Ofisini pale wanataka ushauri wa kisheria, sisi tunajigonga gonga tu hatuna Mwanasheria. Vilevile Zanzibar tayari imekwishapitishwa *Tax Appeal Act,* ambayo itaunda Bodi na *Tribunal* ambapo kesi zote za kodi zitapelekwa kule. Tunataka Mwanasheria wa kusimamia hizi kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni *exemptions.* Kwa kweli inasikitisha sana, asilimia 20 ya *exemptions* za huku Bara ni kubwa, lakini asilimia 90 kwa Zanzibar ni mbaya zaidi. Tunajua hizi *exemptions* zimewekwa kisheria, lakini sasa tuangalie pengine hawa waliopewa *exemption* wana-*abuse* hii nafasi waliyopewa. Wanachukua ile l*oophole* ya kisheria, wana-*evade* hizi kodi. Tusitoe *block exemption;* tukitoa tutaliwa watakuwa wanaitumia vibaya. Tutoe *exemption on case by case basis,* halafu wanapokuja na miradi yao watueleze, kama wanataka kujenga hoteli watatumia vitu gani na kiasi gani; mfano, nitatumia mifuko ya saruji 1,000. Kwa hiyo, tujaribu ku-*monitor*

kiwango kile cha 1,000 waliyoisema. Tusipokuwa makini wakisema 1,000 wataleta 5,000 au 10,000 kwa sababu watasoma hali ya soko na ziada wataiingiza kwenye *market* na kufanya biashara. Hivyo hivyo kwa vifaa vingine.

Tupitie vilevile kwenye hizi *NGOs*, zinahitaji kusaidiwa kwa sababu zipo *non profit*. Zinahitaji kusaidiwa, lakini je, kile kinachosaidiwa ndio hasa kinachotakiwa kwa mfano, wana maafisa 20, watapata msaada wa pikipiki 50 au 100 ni kweli zitatumika kwenye *NGO* au nyingine zitaingizwa kwenye soko ziuzwe? Nadhani tupitie katika maeneo yetu hayo ya Sheria, tuone dosari iko wapi tuweze kuweka sawa.

Kusamehe ni sawa, kwa sababu tunawavutia wategea uchumi; kuna taasisi za dini ambazo zinatoa mchango mkubwa, hatuwezi kusema lazima walipe kodi kwa vifaa vinavyoingia au mambo mengine, lakini tuangalie kama wanakwenda vizuri. Je, yanakwenda kwenye mstari au wanajinufaisha wao kupitia *loopholes* za kwenye sheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekwenda kama cherehani, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja hii muhimu ya Mipango na Bajeti kwa mwaka 2008/09. Nami ningependa kujiunga na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wengine wa Wizara, kwa hotuba nzuri ambayo wametoa. Vilevile ningependa kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge, ambao wametangulia kabla yangu, kwani wameeleza masuala mengi muhimu, ambayo na mimi nilikuwa nikiyafikiria na wamenisaidia kuyachangia. Kwa hiyo, sidhani kama itakuwa ni jambo la msingi kwa mimi kuyachangia tena, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la faraja kubwa sana, kuona kwamba, mipango yetu na bajeti yetu imekuwa ikifuata mipango na mikakati ya muda mrefu ya nchi yetu. Mipango hii na bajeti hii, imekuwa ikifuata mpango wetu mkuu wa Dira ya Taifa ya 2025, MKUKUTA na mipango mingine kama vile *Millenium Goals,* pamoja na kubwa linalotazamwa la Ilani ya Uchaguzi ya 2005 mpaka 2010. Nashukuru kwamba, kwa sehemu kubwa, haya yametekelezwa kwa kuzingatia yaliyomo humu ndani na tumepata mafanikio mazuri sana.

Mimi nashukuru kwamba, Waheshimiwa Wabunge, wameyataja yote vizuri sana na pengine nisingependa kuyarudia. Ningependa tu kusemea baadhi ya maeneo, ambayo yanaonekana kwa namna fulani, pengine yamewekwa benchi au hayapo katika utekelezaji ambao unakwenda katika ari, nguvu na kasi inayotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujikita katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005, ambayo hivi sasa ndio tuna *count down* kufikia 2010. Kama nilivyosema, mengi yamekwenda vizuri, lakini baadhi yake bado yanastahili yaangaliwe vizuri zaidi. Ilani hii ina malengo makuu mawili; moja ni kujenga uchumi wa kisasa wa nchi

inayojitegemea na pili ni kuwawezesha wananchi kumiliki na kuendesha uchumi wa nchi yao kwa faida yao, hayo ndio malengo makuu mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujikita katika kuyachambua haya, kabla sijaingia katika matatizo yanayowakabili wananchi wangu wa Wilaya ya Mkinga hapo baadaye. Sasa basi, yameulizwa maswali mengi. Katika ibara ya 25 mpaka 29, Ilani hii imejikita katika misingi mikuu ya kujenga uchumi wa kisasa. Imeelezwa kwamba, Sekta ya Viwanda ndio Sekta Kiongozi, kwa maana kwamba, ndio kichocheo kikuu cha maendeleo cha sekta nyingine.

Uzalishaji katika kilimo, maliasili na katika sekta nyingine, unategemea sana mitambo, teknolojia na taaluma nyingine ambazo zinatoka katika Sekta ya Viwanda. Ajira na maendeleo ya kasi kubwa ya kisasa, *(modernization),* itatokana na Sekta ya Viwanda. Kwa msingi huo basi, imeonekana kwamba ili tuweze kupata maendeleo mazuri ya Ari Mpya, Nguvu Mpya, Kasi Mpya, hapana budi haya Mapinduzi ya Kilimo tunayoyazungumzia, yaende sambamba na Mapinduzi ya Viwanda. Hilo limezungumzwa kinaga ubaga kwamba sayansi, ubunifu, teknolojia na uhandisi ambao unatokana na viwanda, ndio unaoweza kuongeza tija na uafanisi katika sekta nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunapozungumza Mapinduzi ya Kilimo, mkulima wetu huyu tunalalamika hawezi kupata maendeleo kwa sababu bado anategemea lile jembe la zamani. Plao, trekta na pembejeo nyingine, vyote vinatokana na viwanda. Mvuvi anategemea vifaa vinavyotokana na viwanda kuweza kuendelea na shughuli zake. Sekta ya Madini na kwingineko kokote, wanategemea shughuli hizi ili kujiendeleza. Kwa msingi huo basi, ndio Ilani hii ikaeleza tufanye Mapinduzi ya Viwanda ili yatuwezeshe kujisukuma mbele kwa kasi kubwa zaidi katika maeneo mengine hayo. Sasa hilo limewekewa mkazo na ikaelezwa humu ndani kwamba, Mapinduzi ya Kilimo na Mapinduzi ya Viwanda, ndio kazi muhimu zenye kipaumbele cha kwanza katika kufanya mapinduzi yetu ya kujenga uchumi wa kisasa na huo ndio msingi mkuu wa kujenga uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ajabu sana kwamba, katika utekelezaji wa Sera hii, mipango ya muda mrefu na bajeti, bahati mbaya haikuzingatia hilo lililoelezwa katika Ilani. Wizara ya Viwanda na Biashara na taasisi zake 17 na shughuli zao zote, hazimo kabisa katika vile vipaumbele sita. Vipo chini kabisa na havichukuliwi kwamba ni vitu ambavyo vinasaidia kuleta msukumo huo unaotakiwa! Tumekuwa tukijikita katika maeneo ambayo yanaleta matokeo ya haraka, lakini taasisi kwa mfano zile za utafiti wa kisayansi, zilizo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara na zilizo chini ya Wizara ya Kilimo ni muhimu kuweza kutuletea mapinduzi haya ambayo tunayataka. Tumekuwa tukizipuuzia, kwa kuamini kwamba, hizi tukiwekeza huku, hatutapata matokeo hivi sasa. Matokeo yake, yanapokuja yale ndio yanaleta tija na ufanisi ambao tunataka utuendeleze. Kwa bahati mbaya, hilo halikuzingatiwa na katika kupanga mipango ya muda mrefu na kugawa rasilimali zetu, taasisi hizi zinakuwa zinapuuziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi maalum kama vile *NDC* na *SIDO,* zimewekewa mkazo maalum humu ndani. *NDC* inatakiwa ilete maendeleo makubwa ya Sekta ya

Viwanda Mama. Mchuchuma na Liganga ni shughuli kubwa ambazo zimezungumziwa kwa muda mrefu sana. Viwanda vile vya kemikali vimewekewa mkazo mkubwa sana. Ukitizama maombi waliyoomba *NDC* kwa mfano na fedha waliyopewa, wameomba mabilioni wamepewa milioni chache sana, ambazo labda ni *imprest* tu. Hii maana yake, *Dorector General* kufanya kazi hiyo kuliko kufanya kazi za maendeleo. Sasa haya Mapinduzi ya Viwanda tunayoyataka; tutayapata namna gani katika msingi huo?

*SIDO* ndio imepewa kazi ya kuendesha na kuendeleza wajasiriamali wadogo wadogo katika viwanda vidogo vidogo. *SIDO* maombi yake yamechukuliwa wakapewa sehemu ndogo sana, licha ya hivyo, *SIDO* inawasaidia wajasiriamali sio tu kwa kuwafundisha taaluma mbalimbali na kuwapa teknolojia hizi, lakini vilevile inatoa mikopo kwa hawa wajasiriamali.

*SIDO* nayo kwa bahati mbaya, imepewa mgao mdogo. Bahati mbaya vilevile hata katika zile taasisi za kutoa fedha za mikopo, hazikufikiriwa kupewa mikopo. Sasa kwa namna hiyo, sijui tutakwendaje? Hizi taasisi za sayansi, ambazo zinatakiwa zituongozee utafiti na maendeleo; kuna *CARMATEC, TEMDO* na *TIRDO* zimesahauliwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa nasema ni jambo ambalo bahati mbaya limetiliwa mkazo katika Ilani, lakini kiutekelezaji halikupewa mkazo. Suala lingine la kulifikiria ni kwamba, katika miaka ya 70, nchi yetu ilikuwa ina msingi mzuri wa viwanda. Tulikuwa na viwanda vya bidhaa za kilimo, mitambo ya kilimo *UFI,* tulikuwa na *MUTAVA* inatengeneza matrekta, kulikuwa na viwanda vya magari, viwanda vya baiskeli, viwanda vya nguo, viwanda vya ngozi, *Morogoro Complex* na viwanda vingine vingi tu. Vile viwanda kwa sababu ya maendeleo ya utandawazi na kwa sababu nyingine nyingine vikafa.

Sasa katika Ilani hii ikasemwa kuwa, tufanye jitihada tutafute wawekezaji waweze kuwekeza katika viwanda hivyo, tuvifufue, tuviendeleza na kutengeneza viwanda vingine ili ile kasi yetu ya maendeleo iweze kupatikana. Hilo nalo halitaweza kupatikana, iwapo Wizara na taasisi zenye jukumu la kusaidia viwanda hivyo kutengeneza ubunifu na kuendeleza maendeleo, havijapewa uzito na bajeti ya kuwasaidia. Kwa hiyo, hilo ni suala ambalo tunasema kwamba, kwa bahati mbaya labda tumetetereka kidogo na ni vizuri tujirekebishe; hizi taasisi za utafiti na maendeleo, zina kazi kubwa ya kutusaidia kuendeleza haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema tulifanya makosa, Ilani hii inatuambia kaulimbiu yake ni Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya. Jitihada ile tuliyoifanya zamani, tuifanye sasa hivi kwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya ili tuweze kufikia huko. Tumesema ili tuweze kundelea katika masuala haya, tumeunda vyombo kama *EPZA* ili vitusaidie kutengeneza viwanda vya kuzalisha bidhaa za kuuza nje. Tukasema tutatengeneza maeneo maalum ya kuzalisha bidhaa kwa ajili ya masoko; *SEZ* na *EPZA,* lakini pamoja na kuunda vyombo hivi, bado kimipango na kibajeti, hatujaipa umuhimu ule unaotakiwa ili viweze kutekeleza shughuli zake hizi. Sasa hiyo ni kinyume na matarajio ya Ilani hii; tunakaribia kufika mwisho, *SEZ* moja iliyopo pale Dar es Salaam

inakaribia kumalizika lakini matarajio ni kwamba, ilikuwa kila mkoa ifikapo mwisho wa bajeti hii, ungekuwa na *SEZ* za kutosha. Sasa hapo tumeacha hatujatengeneza hilo, najua tu sungura mdogo huyu anatupa tabu, lakini nafikiri katika mgao huu si vizuri tukaziacha kabisa zikadidimia kinyume cha matarajio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, tuna taasisi kama zile ambazo zinatusaidia kuboresha masoko. Tumetengeneza Bodi ya Stakabadhi ya Masoko, kwa msaada wa wahisani. Hivi karibuni msaada wa wahisani utamalizika na sisi tunafurahi humu ndani tunasema, tunaendelea kutoka kwenye utegemezi na wao wataondoka, lakini sisi tunategemea hiyo na taasisi nyingine tuzilipie wenyewe. Bahati mbaya hili hatulioni, mchango wetu katika hilo ni mdogo sana. Sasa haya nafikiri ni masuala ambayo tunahitaji kuyatazama, endapo tunataka kuliendeleza suala hili. Tumezungumza juu ya kutengeneza Masoko ya Kimataifa Makambako na Segera, lakini toka tuzungumze masuala haya; miaka inakwenda inarudi, bado haiyajafanyiwa maendeleo. Tukatengeneza moja hapa Kibaigwa, tukasema linahitaji kufanyiwa marekebisho yaendelezwe, lakini nalo bado. Sasa nafikiri haya masuala tusiwe na kasi tu ya kuunda taasisi hizi na vyombo halafu tusiangalie sawasawa, hatuwezi kuleta mapinduzi ya kiuchumi yanayotakiwa na kujenga uchumi wa kisasa kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hilo ni kwa upande huo mmoja wa kujenga uchumi wa kisasa. Nafikiri ili tuujenge uchumi wa kisasa, hatuna budi kutoa umuhimu unaostahili kwa Sekta ya Viwanda na Biashara na kuwekeza inavyostahili ili kuweza kuyapata Mapinduzi hayo. Pili, tuje kwenye suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi. Naipongeza sana Serikali kwamba, imejitahidi kutengeneza mifuko mingi sana juu ya masuala haya; MKUKUTA, MKURABITA na kadhalika. Suala la kujiuliza; pamoja na Mfuko wa Rais, tumefanya tathmini ya mifuko hii je, imewafikia walengwa? Wananchi wanyonge kule vijijini, wakulima wadogowadogo na wafanyabiashara wadogowadogo, *SACCOs* tumeunda nyingi, *SACCAs* tumeunda nyingi; je, zimenufaika au wamenufaika wajanja wa mjini, ambao ndio wanakwenda kuchukua fedha hizi au *middle class* ndio wanaonufaika? Tufanye nini ili kuweza kuwanufaisha wananchi, kadiri inavyotakiwa ipo haja ya kulitazama suala hilo.

Tunafurahi kwamba, Serikali imefanya utaratibu wa kufanya Benki ya Rasilimali iongezewe mtaji ili ufikie shilingi 50,000,000, kama baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walivyosema, hizo si nyingi hazitoshi. Imepigwa hatua, lakini napo tuangalie kama hizi nazo zinafaidisha ukuaji uliotakiwa na wananchi wanawezeshwa kadiri inavyowezekana katika hali nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la kutazama *credit management* na *credit guarantee.* Wananchi wengi, wanapata shida kupata mikopo kutokana na masharti magumu ambayo bado yapo. MKURABITA bado haujaweza kusaidia sana. Hata Mfuko wa Rais, wananchi bado wanapata vikwazo vingi na matatizo mengi. Ipo haja ya kuufanyia tathmini utaratibu mzima huu, kawa sababu wananchi wamepata matumaini makubwa sana kwamba, hii mikopo ndio mkombozi wao, lakini kiuhalisi ukienda katika utendaji unakwama sana, walioomba ni wengi sana na waliopata ni wachache sana. Hii inatokana na urasimu mwingi uliopo.

Vilevile Serikali Kuu na Benki Kuu, wafikirie namna gani wanaweza kupanua wigo wa ku-*create guarantees* ili kuweza kusisimua uchumi wetu katika maeneo mbalimbali na kuwawezesha wananchi kuingia katika masuala haya ya uzalishaji mali, huduma na biashara ili kuendeleza uchumi na kupambana na umaskini kama inavyotarajiwa leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo ya jumla, nashukuru sana kwamba na sisi Wilaya ya Mkinga, tumefaidika chini ya Ilani na mipango hii mbalimbali. Sasa hivi nashukuru kusema kwamba, barabara ya Tanga – Horohoro imo chini ya Mpango wa *MCC* na inatarajiwa kutiwa lami.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwandoro, hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sana sikuisikia. Naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi nami nishiriki katika mjadala wa hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, ambao unaenda vizuri. Nianze kwa kuungana na Waheshimiwa Wabunge, walionitangulia kuzungumza; kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu wote wawili, Gavana wa Benki Kuu, Kamishna Mkuu wa *TRA* na Wasaidizi wote Wizara ya Fedha na Uchumi na Wizara ya Mipango, kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya, wakishirikiana na Serikali nzima; kusimamia misingi ya kiuchumi iliyotufikisha hapa, chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tukaweza kuwa na bajeti ya kuzungumza, tukisema kuwa matumizi ya ndani tunajitegemea. Hongera sana Serikali ya Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa sababu ni mara ya kwanza nasimama kuzungumza, kwa niaba ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na kwa niaba yangu binafsi, natoa salamu za rambirambi kwa Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, *CDF, General* Mwamunyange na kupitia kwa *General* Mwamunyange kwa jamaa, ndugu na marafiki wa marehemu waliofariki kufuatia ajali kubwa ya helikopta ya jeshi huko Arusha. Tunaomba Mwenyezi Mungu, azilaze roho za marehemu pema peponi, amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba, Serikali ichukulie kwa uzito wa pekee, ushauri ulitolewa kwa niaba ya Bunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dr. Abdalah Kigoda. Nimeipitia taarifa ya Kamati yetu ya Bunge, imechambua na kutoa ushauri unaofaa. Naipongeza sana Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa kuisimamia sekta hii kwa niaba yetu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na suala la ulinzi usalama wa raia na mali zao. Hii bajeti haitatekelezeka nchi yetu ikiingia katika hali ya hatari kiusalama, kwa hiyo ni lazima tutambue mchango wa majeshi yetu ya ulinzi na usalama, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika mazingira magumu. Naishukuru Serikali, inachukua hatua ya kuboresha mazingira yao magumu ya kazi, lakini haijafanya vya kutosha.

Naishia hapo, mbele ya safari tutazungumza zaidi kwa sababu Serikali inatoa ushirikiano mzuri kwa Kamati yetu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama katika kuboresha mazingira mazuri ya kuwezesha ulinzi na usalama wa raia na mali zao.

Hali ya usalama katika Mkoa wa Kagera, imeelezwa na Mheshimiwa Blandes, kwa mfano tu wa Karagwe; magari yanasafiri kwa kusindikizwa na askari polisi, tunahatarisha maisha ya askari hao. Maana yake wao ndio *target,* wanakuwa kwenye mabasi au kwenye magari kwa sababu hatuna magari ya *escort* na hatujaweka ulinzi madhubuti katika mkoa huo; maeneo ya Ngara, Karagwe na Muleba, kuhakikisha watu wanaishi kwa amani. Hili ni jambo la kuliwekea mpango maalum. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, amani ya watumishi wa umma; ni ukweli usiopingika kwamba, hakuna amani katika utumishi wa umma. Mfano wa kwanza ni jinsi siri zinavyovuja katika Serikali yetu ni ishara ya kuonyesha watumishi wetu wa umma wana namna fulani ya kutoridhika na wanayofanyiwa, kwa hiyo, wanakosa hata uzalendo wanakiuka viapo vyao. Mishahara yao kwa kweli haitoshi, kima cha chini cha shilingi 100,000 hakitoshi. Kima cha chini ndio wanaotumia mkaa, ingawa na mimi natumia mkaa, pamoja na kwamba ni Mbunge lakini napikia mkaa. Unaweza kupikia majiko yoyote ni uhuru wa mtu, uwezo wa mtu na vipaumbele vyake, lakini gunia la mkaa karibu shilingi 30,000. Sasa mfumko wa bei ni tatizo ambalo linawakumba sana wakulima wa Muleba na hata watumishi wa umma ambao wapo mijini katika mazingira magumu sana, lazima vichwa vichemke. *Brain* zipo, bahati nzuri wote wapo na ni wasikivu, wataifanyia kazi. Hatuwezi tukasema mfumko wa bei upo kwa sababu ya utandawazi, lazima na sisi tutafute namna. Nitatoa mapendekezo machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna amani kwenye vyombo vya habari; tunasoma haya magazeti, huo ndio ukweli. Vyombo vya habari tunavihitaji sana vijenge mazingira mazuri katika nchi yetu na vijenge jina zuri la nchi yetu, ili wawekezaji waweze kuja nchini kuwekeza, lakini hawana amani. Sasa nimesikia mambo ya kusikitisha, ambayo naomba Serikali iyachukulie kwa uzito wa pekee. Wabunge wawili, tena Viongozi; Mwenyekiti na Makamu wake wa Kamati ya Hesabu za Serikali wanasema, kuna watumishi wa umma wamekwenda kuongea na wabia wetu katika maeneo ambayo tunawaita wahisani, wakawaambia tutafunga watu sijui kumi sijui watano kwa mwaka ili mtusaidie. Watutake radhi hawa watumishi na waende kuzifuta kauli hizo. Hii ni kutisha watumishi wetu, hivi mtu anatumikia umma, tuhuma tu zikitoka anaweza akadhani kuna shinikizo la wahisani la kumfunga si muda mrefu ili pesa zije, hatuzitaki hizo pesa za wahisani za kufunga watoto wetu ili watupe hela. Wasilete, kwanza tunaweza kujigharamia matumizi ya ndani, maendeleo tutakopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii imefanya kazi nzuri na Mheshimiwa Rais ametueleza, tunakopesheka. Uwiano wa deni na *GDP* yetu ni mzuri (asilimia 20) tu. Kwa hiyo, tunakopesheka, naishauri Serikali itumie vyombo vya mabenki tukope. Hawa wahisani wenye masharti ya kufedhehesha kama haya, tusiwabembeleze tena kwa sababu tumejijengea uwezo kwa kushirikiana na wananchi wetu ili tuweze kuwekeza katika uzalishaji na kuweza kupanua wigo wa kodi na hivyo tutakuwa tumemsaidia Mheshimiwa Kitilya, Kamishna Mkuu wa *TRA,* anakamua ng'ombe, mwisho atakamua damu, lazima tumlishe ng'ombe huyu. Anayetakiwa kumlisha ng'ombe ni Serikali na maziwa ndio umma wenyewe tunaokamuliwa kulipa kodi. Kwa hiyo, tupanue wigo kwa kuwekeza zaidi na si kwa kuongeza kodi nyingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa hapa sharti uhuru wa vyombo vya habari uwekwe sawa, ndio tupate *support* ya wabia wetu wa maendeleo, imenishtua sana. Hivi ni nini kinachogomba kwenye uhuru wa vyombo vya habari? Maana yake wadau wa msingi wa vyombo vya habari ni sisi tunaosoma habari, wao wanatupasha habari na ni haki ya Kikatiba. Sasa hivi hii sheria ina matatizo gani? Kama ndio tatizo tuleteeni hiyo sheria, kama mna ugomvi kule hamuelewani, tutautatua ndani ya Ukumbi huu ili sheria hiyo iwepo. Waandishi wa habari wafurahi, tukiona inatuvuruga tunafuta, mambo yote yanafanyika humu humu. Hakuna sheria, uhuru wa vyombo vya habari upo, wanaandika kila kitu mpaka hata vikao vya siri na hawakamatwi. Tupewe taarifa ni waandishi wa habari wanagapi wamekamatwa na kuwekwa polisi au rumande, kwa kuandika habari. Tusiwe tunaleta hisia, Tanzania hakuna uhuru wa vyombo vya habari, wakati uhuru uliopo Tanzania haupo Afrika nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kuanzisha magazeti hata kesho na ukaandika chochote. Viongozi tunaandikwa, watu hawakamatwi. Sasa uhuru zaidi ya huo, kama ni sheria, hiyo ni Sheria ya Bunge ni mali yetu. Tuleteeni, Serikali msigombane na vyombo vya habari au hawa wahisani ili kuwe na amani na watusaidie kutangaza jina zuri la Serikali yetu, inayofanya vizuri. Haya mazuri, nawaomba waandishi wa habari wayaandike kwamba, Serikali imeweza kujenga misingi ya uchumi, tunajitegemea kwa mapato ya ndani. Waandishi wa habari andikeni hilo ni zito, sio kuandika suala la bajeti mbadala.

Lazima niwachokoze rafiki zangu hawa ni wachokozi sana. Mimi nawapenda sana hawa marafiki zangu, nataka muendelee kuwa kwenye Bunge, lakini msiongezeke, mbaki hivyo hivyo, kwa sababu tunashirikiana vizuri. Hawa tumeshaelewana, tunashirikiana vizuri na wanaunga mkono mambo yanayofanywa na Serikali. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuimarishe kilimo cha wakulima wadogo wadogo; wale wakubwa watu kutoka nje wasiletwe, lazima wakulima wawe ni Watanzania, kwa sababu watalima kwenye ardhi yetu. Tumewapa migodi, tuwape na ardhi? Mimi siungi mkono hoja ya kuwaita wawekezaji eti kutoka nje, kuja kuwekeza kwenye kilimo kikubwa. *Sokoine University* walituahidi kwamba, wataweka mitaala ya kuzalisha wataalam wa kilimo. Mwanzoni walikuwa wanazalisha watawala wa kilimo, miaka imepita mitano bila shaka wame-*graduate.* Tuwe na Watanzania, tuchague

wanaopenda na wenye uwezo, tuwape fedha, mitambo, mbolea na mbegu za mifugo, wafuge mifugo. Tumeshamsaidia Mtanzania mmoja hapo kufuga na kuwa na kiwanda cha nyama. Naipongeza Serikali kwa wazo hili, wawe kama 50 wa namna hiyo na kuwadhamini kwenye mabenki ili wazalishe, wakishindwa tunawanyang'anya hizo mali tunawapa wengine, mpaka tutakapozowea ili nchi yetu iweze kwenda kwa kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali imetenga hela ya kutosha, kumalizia miradi inayoendelea ya miundombinu ya barabara. Barabara ya Kagoma – Muleba – Biharamulo - Lusaunga, mnaitengeneza vizuri sana na Mheshimiwa Rais, anaitaja mara nyingi, nawapongeza sana. Kopeni hela tumalizie zilizobaki; Tabora kwenda Kigoma, Nyakanazi kwenda Kigoma, mpaka Rukwa kwenda Kusini na ya Babati kwenda Iringa kupitia Dodoma. Tukope halafu uchumi utachemka na hapo ndio tutalima. Tukisema Waziri wa Kilimo hamasisha, sijui nini; mwaka huu umekwisha hatujapewa taarifa. Mimi namsubiri Waziri wa Kilimo, lazima anipe maelezo; tumeanza miaka miwili *ASDP;* tumelima nini na tumevuna nini? Hatuwezi kuwa tunazungumza Mpango Maalum wa Kufufua Kilimo, wakati hatuzalishi hata gunia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *D by D,* kupeleka madaraka kwa wananchi. Sasa Kamati ya Fedha na Uchumi, imetueleza vizuri kwamba, tatizo fedha ambazo tunapeleka kwenye Halmashauri za Wilaya kwa matrilioni, hazifiki ambapo tumekusudia ziende. Kuna ubadhirifu na wizi, kwa hiyo, wanapendekeza udhibiti uwepo na Waziri nakushukuru unasema utabadilisha hata Sheria ya Halmashauri za Wilaya, Sura Namba 290 na Sheria ya Fedha, Sura Namba 348 ili kuweka udhibiti. Mlipaji Mkuu wa Serikali adhibiti, hili ni jambo zuri, lakini napenda kwenye maelekezo hayo au marekebisho hayo, Wabunge wasiwe Wajumbe tena wa Halmashauri za Wilaya. Tuna Kamati ya Fedha na Uchumi, inasimamia usimamizi wa hesabu za Serikali za Halmashauri, sisi wakiwa wanakutana kule, tunakuwa Bungeni na hata ukienda kura yako ni moja; una Jimbo zima kama la kwangu lina watu 300,000 na Kata 19. Nikiingia kwenye Halmashauri au Kamati ya Fedha na Uchumi, mathalani ukiwashauri wakakataa, maana sijaingia wakanikatalia kwa sababu sijahudhuria, sina muda wa kuwepo kwenda kule, vikao vinaitishwa nikiwa huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mnaweza mkacheka haya, Waziri Mkuu ameweka ratiba vikao viitishwe tukiwa huku huku nje, vinaitishwa halafu maamuzi yakishatolewa wanasema na ninyi ni Madiwani mlihusika! Sasa katika Utawala Bora; hivi kweli unaweza ukaja hapa Bungeni kuanza kuwasimamia wale wanzako ambao umevuruga nao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mdhibiti na Mkuguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; Serikali ichukulie kwa uzito wake mgongano wa madaraka na uwajibikaji, haya ni mambo ya mwanzoni mwa miaka ya 1980 na sasa tuko 2008. Mabadiliko haya yazingatie kwamba, Bunge sasa linasimamia Halmashauri za Wilaya, yaani Serikali za Mitaa na Serikali Kuu yenyewe, sasa hatuwezi tukawa tunajisimamia halafu tunasimamia; ni mkanganyiko. Siyo kwamba mimi ninawadharau Madiwani, siwadharau kabisa, lakini mtu anasema na ninyi ni Madiwani na ni kweli, kwa sababu usipokuwa kwenye kikao na ni Mjumbe; unawajibika na maamuzi hayo. Sasa hatuwezi kwenda

kisanii, hasa sisi wanasheria tunajua, yaani unakuwa mjumbe kwa vikao usivyohudhuria kisanii, kwa sababu sheria inasema unawajibika na maamuzi. Wabunge ni hivyo hivyo, ukiwa Dar es Salaam tukaamua hapa, huwezi kutukanusha ukasema mimi sitambui. Kuna Kanuni zetu za Bunge tunakudhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya Kiwanja cha Ndege cha Bukoba, wenzangu walionitangulia wamesema ni dharura ya kwanza au ya pili hiyo.

**MWENYEKITI:** Ni ya pili, Mheshimiwa Masilingi.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Ninaunga mkono hoja, mambo ni mazuri, mengine tutakutana mbele ya safari nikichangia yatakayofuata. Ninashukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Wilson Masilingi, naona kweli gari lilishika kasi haswa.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nachukua nafasi hii ya kipekee, ambayo ni adimu, kuipongeza sana Hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, aliyotuletea Mheshimiwa Mustafa Mkulo. Hotuba hii inaleta matumaini sana; ni nzuri, inaeleweka na nadhani haijawahi kutokea mpaka inafikia hata Wapinzani pamoja na kukosoa kwa sababu ni sehemu yao ya kukosoa, wanaikubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hii hotuba ambayo ni nzuri, niwapongeze sana Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na ndugu yangu, Mheshimiwa Jeremiah Sumari, kwa kweli wamemsaidia sana Waziri na bajeti inaeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue nafasi ya kipekee, kuishukuru sana *TRA* kwa sababu mpaka tunapozungumza, kama mapato yasingekusanywa vizuri, huenda tusingepanga hata bajeti, kwa sababu huwezi ukapanga bajeti kama huna uhakika wa kukusanya mapato. Kwa hiyo, ninawapongeza sana wenzetu hawa wa *TRA,* wakiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi na Kamishna Mkuu, Bwana Kitilya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii bajeti ninavyoiona mimi siyo mbaya ni nzuri, pamoja na kwamba, kuna malalamiko sana kwa wenzetu Wapinzani, lakini niseme kwamba ni nzuri tu. Hii bajeti ni nzuri kwa …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yono Kevela, hebu jielekeze kwenye hotuba ili tuweze kwenda sawa sawa.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimwa Mwenyekiti, sawa sawa, kwa hiyo ni bajeti nzuri, kwa mfano, suala la mfumko wa bei, si la Tanzania tu, nchi zote zinakumbana na tatizo hili. Hata ukienda Kenya au Ulaya kule, mfumko upo. Tatizo la mafuta limeathiri nchi mbalimbali, sasa kwa sababu watu wanaangalia sehemu ndogo tu ya Tanzania, wanaona mfumko wa bei labda ni hapa Tanzania tu, lakini ukweli ni tatizo la Dunia nzima. Kwa hiyo, ninaipongeza sana Serikali, kwa jinsi ambavyo imetengeneza

bajeti na jinsi ambavyo imeanza kujitoa kwamba, hatategemea sana wahisani, kwa kweli ninaipongeza sana Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nizungumze hapa kwenye ushauri tu kwamba, kwa vile tuna kiwanda kinachoitwa *Tipper*, kingesaidia sana Serikali, pamoja na kwamba kweli tuna soko huria la mafuta, lakini soko huria la mafuta si kwamba kuwa huria itatesa wananchi wa kawaida. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria kwamba, tuiwezeshe *Tipper* tuweze kuagiza mafuta kusudi tuweze ku-*balance* na ku-*regulate* bei. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iangalie hilo, *Tipper* iwezeshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu lingine la jumla, nilitaka nizungumzie kuhusu suala la viwanda; kwenye Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, inaeleza kabisa kuhusu suala la viwanda, elimu na kilimo kwamba ni lazima tuelekeze nguvu kule. Sawa, tunajitahidi kwenye barabara, lakini suala la viwanda kama hatutaviboresha vya kawaida, vya kati na vikubwa, kwa sababu tutakuwa na mazao mengi ya kilimo, tutapeleka wapi? Si lazima tu-*process,* tukisha-*process* tuna-*add value* kwa hiyo tuki-*add value* moja kwa moja, mkulima wetu wa kawaida atapata unafuu mahali pa kupeleka. Kwa hiyo, suala la kilimo ni kitu muhimu, lakini viwanda ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri sana bajeti iongezwe kwenye viwanda, kama inavyoongezwa kwenye kilimo. Wenzetu wa Serikali kweli mmefanya kazi vizuri, mmeongeza bajeti nzuri kwenye kilimo na hata inafikia wakati mnatoa ruzuku; sasa ninajiuliza mbona ruzuku kwenye viwanda hakuna? Viwanda mnawaachia watu binafsi nao hawana nguvu, wawezeshwe. Kama kilimo chenyewe mnasema na watu binafsi wachangie, lakini mtu binafsi hataweza lazima awezeshwe, hata nchi za wenzetu ambazo zimeendelea za Ujerumani na Japan, wazalendo wanawezeshwa. Ninachoangalia hapa, suala la uzalendo lazima liwekewe umuhimu sana, siyo kuwawezesha; mnawawezesha watu wa nje, sasa uchumi si utaenda huko nje? Tuwawezeshe watu wetu ambao ni wa kawaida, hawa wanyonge. Bahati nzuri kuna mipango kama hii ya MKURABITA, sawa lakini je, inatekelezwa na je, huyu mnyonge anawezeshwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano hai tu, nilikuwa natembea kwenye kijiji changu pale Ilembura; mambo ya MKURABITA ukimweleza mjasiriamali au pale Makambako vijana wengi zile hela zinapokuja, wanafikiri ni za wenye mali. Ujasiriamali, maana yake za wenye mali (wafanyabiashara wakubwa). Kwa hiyo, mwananchi wa kawaida huyu, anakuwa bado hajafaidika na ujasiriamali (hizi hela ambazo zinakuja). Kwa hiyo, nilikuwa ninafikiria kwamba, kwa sababu tayari tunalenga watu ambao ni wanyonge, hatulengi watu ambao wana uwezo. Hivyo, ni vizuri tuangalie nguvu zetu, tuelekeze kwa watu ambao ni watu wa kawaida kabisa, wanyonge hawa tuwawezeshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeishauri sana Serikali iangalie hata hizi *SIDO; SIDO* inafika hadi mpaka vijijini, ndio wanaita *entrepreneurship* ipo kule ndio *SIDO.* Sasa mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda, bajeti ile ilikuwa ndogo sana, ninaishauri

Serikali iwawezeshe wenzetu wa *SIDO* na siyo *SIDO* tu hata *TILDO* na *NDC.* Wawezeshwe hawa watu kwa kweli itasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nizungumzie suala la viwanda kuhusu mbolea. Tunahangaika suala la mbolea, ninaishukuru Serikali mmeisaidia sana Mijingu mpaka inafikia hatua mmeipa ruzuku. Wapo watu wengine wanahangaika sana kutaka kuwekeza kutoka Marekani, wanataka kuwekeza mambo ya *organic fertilizer.* Labda nizungumze haraka haraka, kuna mwekezaji mmoja anaitwa *TIGI International Limited,* ambaye anashirikiana kabisa na mwekezaji kutoka Marekani, mbolea yake inaitwa *Food Natural Organic Fertilizer Composite.*

Huyu mwekezaji amehangaika kwenda mpaka pale Wizara ya Kilimo, amepewa kibali lakini yule mtu inatakiwa awezeshwe. Mbolea ile ni nzuri, ina hifadhi udongo, inatunza rasilimali ya udongo na haina madhara. *Organic Fertilizer* na *raw materials* ni vitu vidogo sana; ni maganda ya karanga tu na maji machafu na haya maganda ya karanga ile karanga yenyewe bado inaweza ikatengenezwa sabuni. Kwa hiyo, nchi yetu ingeweza kulima karanga kiasi cha kutosha, kwa mfano, wenzetu wa Singida, Dodoma na Iringa, wangeafaidika sana na hii *Project*. Huu Mradi wa Kiwanda cha Mbolea ambayo inaitwa *Organic Fertilizer,* naelewa wahusika wanaufahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama hao watu wangewezeshwa ingekuwa vizuri na bahati nzuri *location* tunategemea iwekwe pale Ikingula, Wanging'ombe. Tumewawezesha tu wametoa hekari 150, sasa pale kinachotakiwa ni suala la kupeleka huu umeme wa gridi, ambao upo jirani pale Makambako na suala la reli lipo pale jirani. Tukiwezeshe kiwanja cha ndege, ambacho kipo pale Ilembura, nacho kitasaidia sana kwa sababu kinakuwa cha aina yake; kinakuwa ni tofauti katika Afrika, yaani ni kiwanda kikubwa katika Afrika. Kwa hiyo, hili tatizo la mbolea kwa wakulima lingepungua sana. Mbolea sasa hivi mfuko kama wa *DAP* ni gharama kubwa kule, inafika mpaka Sh.100,000; huwezi ukaamini, watu wanalalamika sana. Sasa kama Mungu angetujalia 2009/10, tukajenga hicho kiwanda, inge-*compute* na mbolea nyingine, sawa mbolea za chumvi chumvi zipo nzuri lakini zina madhara fulani Fulani, hatuwezi tukasema ni nzuri moja kwa moja. Hii *organic fertilizer* ingesaidia sana kutunza mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niondoke huko nizungumzie kuhusu suala hili la UKIMWI. Janga la UKIMWI bado ni tishio, nilikuwa ninaangalia bajeti inaangalia vipi hili tatizo. Mbaya zaidi, kitu kinachoonekana hapa ni kwamba, sisi wa Mkoa wa Iringa ni waathirika wakubwa, tumechukua namba moja asilimia 14.5, *approaching* kama asilimia 15, yaani katika watu 100 watu 14.5 au 15 wameathirika.

Tulikuwa tunafuatilia takwimu ambazo anatoa Waziri Mkuu, kwa kweli zimenisikitisha sana kwamba, mkoa wetu pamoja na kwamba ni *among the big four* wa ku-*produce* chakula, sasa tunaathirika tumekuwa *among the best* kwenye suala la *HIV*. Hili limenishtua kweli, lakini siwezi nikasema sisi labda tuna matatizo ni maingiliano, kwa sababu kule kuna mambo ya mbao, watu wanatoka nchi mbalimbali wanakuja pale, halafu kuna barabara kubwa pale watu wa Zambia na sehemu nyingine wanakuja, kuna viazi na vitu vingine; kwa hiyo, wageni wameingia wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tulikuwa tunafikiria Serikali iangalie uwezekano wa kutusaidia iweze kuleta kinga, sasa kinga zipo za aina mbalimbali, kwa sababu wanaleta dawa, lakini kinga ni bora kuliko tiba. Suala la elimu, wamwagwe wataalam pale watoe elimu ikiwezekana hata makanisani na misikitini, kwa sababu ni suala la tabia. Watoe ruzuku, pesa ziende kwenye misikiti, watu watabadilika tu pamoja na kwamba, kuna sababu nyingi tu kwa mfano, hali ya hewa; kuna baridi sana kule, lakini hiyo siyo *factor.* Kuna mambo mengi, jana nilikuwa ninaongea na Dr. Mpangule akasema, bwana inawezekana *research* imefanyika, mambo ya *circumcision* ni kitu muhimu sana. Watu wangeweza kutoa elimu, wakafanya watoto wa kiume wakawa wanatahiriwa, siyo ukeketaji hapana; athari ya UKIMWI ingeweza kupungua. Maeneo mengine *research* imeshafanyika mfano, Kenya na sehemu nyingine kwamba, *circumcision* inapunguza sana maambukizi ya UKIMWI kwa asilimia 40. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona watu hawanielewi hapa, kwa kweli suala la kinga ni kitu muhimu sana. Kwa hiyo, nilikuwa ninafikiria sasa hivi badala ya kujielekeza kwenye tiba, tujielekeze kwenye kinga; fedha zitolewe kwa ajili ya kinga, *condom* zimwagwe kule nyingi tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sehemu nyingine vijijini kule *condom* hazipatikani na sehemu nyingine zinauzwa kwa bei kubwa; Sh.200 uchumi haupo. Kwa hiyo, hilo ni tatizo lakini hatushauri kwamba, watu watumie *condom* hapana, tunashauri vilevile kama kuna uwezekano, wananchi waokoke nayo ni nzuri tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la suala la UKIMWI linanisumbua sana akili; mkoa wetu una matatizo, kwa hiyo, Serikali ninaishauri ielekeze nguvu kule, iangalie ile *rate* ipungue tufike asilimia kumi, ikiwezekana uishe kabisa, hii ingetusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nataka nizungumzie kuhusu suala la wanyamapori. Wanyamapori ni kitega uchumi kizuri sana, nadhani kwenye bajeti nimeangalia naona kinaweza kikaleta maendeleo makubwa tu, lakini ninachotaka kusema ni kwamba, hawa wanyamapori kwenye eneo langu pale *Kipengele Mpanga Game Reserve*, ule mradi ni mzuri lakini ninajaribu kuangalia utekelezaji wake, wananchi wanaulalamikia. Kwa mfano, kabla mimi sijawa Mbunge, mipaka ilionyesha kwamba, wananchi hasa wa Kata ya Luduga, mipaka yao ni hapa maeneo ya Malangali, Mambegu na maeneo ya jirani jirani kwamba mipaka ipo mahali fulani, watu wakahama Mpangampya toka Igalatilo wakahamia Mpangampya. Kilichotokea, sijui ni mambo ya kisiasa mimi sielewi; watu wanasumbuliwa wanaambiwa wahame tena na mbaya zaidi, wakati wanahama wale wananchi waliahidiwa vitu vingi tu; barabara nzuri, maji na zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mpaka sasa hivi watu wanateseka, hawana vitu kama hivyo. Watu wamejitolea kujenga shule ya msingi pale, kwa mfano, Mpangampya lakini wanaambiwa wahame tena wanasumbuliwa. Kwa hiyo, nilikuwa ninaiomba Serikali, waangalie uwezekano ile mipaka ya zamani waifuate na bahati nzuri nilipoongea na Meneja wa *Mpanga Game Reserve,* akaandika barua kwamba

hawatasumbuliwa. Sasa sielewi mipango ya Serikali kama watasumbuliwa au vipi, lakini ninaomba Serikali isiwanyanyase.

Mbaya zaidi, kwa sababu pale wanyama wenyewe ni kidogo sana, yaani kuna digi digi na paa wadogo wadogo wa kuhesabu; sasa ninajaribu kuangalia digi digi wawili wana thamani kuliko maisha ya binadamu ambao wanateseka; kwa nini uwasumbue wananchi? Kwa hiyo, ninaiomba Serikali kwa kweli iangalie kama ingewezekana, kama hamtahamisha wanyama kutoka mahali fulani labda Mikumi au Ruaha kuwahamishia pale Kipengele, basi achaneni na huo mradi, kwa sababu unawaletea athari.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kevela, hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninasema ninaunga mkono hoja bajeti ni nzuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Yono Kevela na ninashauri kuokoka huko ungeanza wewe na baba askafu yupo hapo pembeni yapo, halafu wengine watafuata.

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, niweze kuchangia machache katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi ya Mwaka 2008/09. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Naibu Mawaziri wake, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji Wakuu, kwa maandalizi mazuri ya bajeti hii ya 2008/09. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niipongeze Serikali kwa kusimamia utekelezaji mzuri wa Bajeti ya 2007/08 na ambayo tunafikiria kwamba, tutafikia malengo ambayo tumejipangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya mwaka 2008/09 imekuja wakati kuna hali ngumu sana ya uchumi katika jamii yetu ya Watanzania kutokana na mfumko wa bei za *petrol*, vyakula, malighafi na pembejeo. Wananchi wanategemea Bajeti hii itajibu hali ngumu ya uchumi iliyopo katika nchi yetu hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na bei ya *petrol;* ni kweli imepanda sana katika Soko la Dunia na hili hatuna udhibiti au hatuna uwezo wa kulidhibiti. Ninaomba niiambie Serikali kwamba, licha ya bei hiyo ya mafuta kupanda kwenye Soko la Dunia, Serikali bado inaweza kudhibiti bei ya *petrol* katika biashara ya ndani, kwa kuangalia bei zinazotozwa na wafanyabiashara wa humu ndani. Wafanyabiashara za bidhaa hii ya *petrol*, si ajabu wanaweka *margin* kubwa sana katika biashara zao. Pili, Serikali bado inaweza kudhibiti bei hii ya *petrol* kwa kuangalia upya, uwezekano wa kupunguza kodi katika bidhaa hii ya *petrol* au kuondoa kodi katika bidhaa hii ya *petrol*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu tuliyoyaamua jana, siyo lazima tuendelee nayo mpaka miaka 100 ijayo. Ninasema hivyo nikiwa na maana kwamba, katika hali tuliyofikia sasa, bei ya *petrol* ikipanda tena mara mbili, tatu, maisha yatakuwa magumu sana kwa Mtanzania wa kawaida. Ni vyema basi nishauri kwamba, Serikali itazame upya na iwe na mikakati mipya ya kutazama bei ya bidhaa hii ya *petrol* ambayo ndio inayochangia au ndio kichocheo cha maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niingie kwenye sehemu ya kilimo. Tumekuwa na majina mengi sana na misamiati mingi sana kwenye Sekta hii ya Kilimo; tulianza na kilimo cha kufa na kupona, kilimo ni sekta mama, kilimo sekta kiongozi, kilimo ni uti wa mgongo, lakini bajeti zetu zote ambazo zinaletwa hapa kwa miaka hii mitano, sita iliyopita, hakuna inayoonyesha dalili ya kwamba, misamiati hii tunayoitumia inadhihirika kutokana na bajeti zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi bajeti ya Sekta ya Kilimo imetengewa asilimia sita ya bajeti ya mwaka huu, ambayo ni kiasi kidogo sana. Ni muhimu sana Serikali itambue kwamba, Sekta ya Kilimo ndio inaajiri Watanzania karibu asilimia 80 na pia inachangia kwenye Pato la Taifa.

Serikali ikiongeza uwekezaji katika kilimo, kwanza tutadumisha ajira hii ya asilimia 80 ambayo ipo sasa na tutaibua ajira nyingine, tutaongeza uzalishaji wa mazao ya chakula, tutaongeza ubora wa mazao haya ya chakula na mwisho tutaongeza hata na Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni njia nyingine ambayo ni dhahiri kabisa ya kuongeza ajira katika nchi yetu isipokuwa kilimo. Sekta nyingine zinaweza zikatupa ajira, lakini siyo kiasi cha ajira ambacho tunakipata katika Sekta ya Kilimo.

Ni vyema Serikali iikawekeza kwenye Sekta hii ya Kilimo iongeze hata mchango ufike angalau asilimia kumi ili tuweze kuendelea na iweze kuchangia kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili ni wazi kwamba, kinachohitajika ni mitaji na Waheshimiwa Wabunge wengi hapa wametoa wazo nami ninaungana nao, la kuwa na Benki ya Wakulima. Hili likifanywa na Serikali, tutakuwa tumeondokana na shida ya mitaji katika Sekta hii ya Kilimo na ndipo hapo Serikali inaweza kusema watu binafsi, ikiwa ni pamoja na sisi na wale wa nje, ambao tunataka kuwaita tuingie sasa katika Sekta hii na kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie wigo wa kodi; ni dhahiri kwamba, tukipanua wigo wa kodi, tutapanua au tutaongeza mapato yetu katika miaka ijayo. Sijui kama wigo huu wa kodi, tunaweza kuupanua kwa sasa na ukatusaidia kuongeza mapato katika mwaka huu wa 2008/09.

Mimi naona mpango huu wa kupanua wigo wa kodi, unaweza kutusaidia baada ya mwaka huu wa fedha, maana yake mipango yote tutafanya katika mwaka huu wa 2008/09

lakini kama kuna mipango ambayo imeshaandaliwa ya upanuaji wa wigo huu wa kodi, basi ni vizuri labda Mheshimiwa Waziri wakati aki-*wind up,* atueleze hiyo mikakati na sehemu hizo ambazo wigo wa kodi unaweza kupanukia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili niseme tu kwamba, hatua ya mwanzo katika kupanua wigo wa kodi iwe ni kufuta au kupunguza misamaha ya kodi. Misamaha ya kodi, kwa sasa hivi imekuwa mikubwa sana, ukitazama Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, misamaha ya kodi kwa ushuru wa forodha ina-*range* kutoka asilimia 32 mpaka asilimia 44 kwa mwaka 2005/06 na mwaka 2006/07; na kwa kodi za ndani misamaha ya kodi ipo katika asilimia 75 ya mapato ambayo yamekusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukirekebisha sheria zetu ambazo kwa sasa tunaona ni sheria mbovu ingawa sisi ndio tumezipitisha, tutaweza kupata kiasi hiki cha kodi ambayo tunaisamehe na inakwenda kwa wale wale ambao ndio wanachimba madini katika nchi hii. Sekta ya Madini sasa hivi hatuoni kama inaiingizia Serikali chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa haraka, nizungumzie juu ya uwezeshaji; kuna mifuko mingi ambayo imeanzishwa ya kuwawezesha wananchi wajasiriamali katika nchi yetu, lakini haitoshi. Mimi ningependekeza katika kugawa mabilioni ya JK sasa twende Wilaya kwa Wilaya; Wilaya ipewe mgao wake tuone jinsi ya kukopesha katika *level* ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nije kwenye uwezeshwaji wa wachimbaji wadogo wadogo wa madini, ambao sisi ndio tunawafahamu, maana yake hawa wakubwa tunaona hawachangii chochote kwenye *well being* ya uchumi wetu. Hawa wachimbaji wadogo wadogo, ukitazama machimbo yao hayana hali nzuri ya usalama.

Tumeiona hali hiyo katika machimbo ya Mereran; kunapokuwepo na mvua wanaweza kupatwa na majanga yote kama yale yaliyotokea juzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sasa Serikali iwasaidie hawa wachimbaji wadogo wadogo kwa kuwapa mitaji, zana za kufanyia kazi zao na ikiwezekana pia iwahakikishie soko. Pale Mererani, Serikali ilishasema kwamba inaweza kufungua kiwanda cha kuchonga madini ya *Tanzanite* ili yawe na soko la kuaminika na kuyaongezea thamani ili yasiuzwe yakiwa *raw,* sijui Serikali inasemaje kuhusu suala hili. Maana pia ikifungua kiwanda hicho cha kuchonga *Tanzanite* itakuwa ni kwa faida ya Tanzania maana tutapata kodi kutoka kwa wachimbaji wadogo wadogo na wakubwa pale Mererani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye Jimbo la Arumeru Magharibi, sisi kule tuna shida ya umeme na tuna ahadi nyingi za Serikali ambazo imetupa katika nyakati mbalimbali. Tunaomba Serikali itimize ahadi hizo ambazo imetupa katika nyakati mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naomba niseme kwamba katika Jimbo langu kuna malalamiko ya Walimu Tarajali ambao hawajalipwa stahili zao za fedha za kujikimu katika mwaka wa 2003/2004 na 2004/2005. Naomba Serikali ishughulikie malalamiko haya ya Walimu Tarajali kwa kuwalipa stahili zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niseme kwamba naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Mollel. Sasa namwita Mheshimiwa Rita L. Mlaki na msemaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja hii ya bajeti ya mwaka 2008/2009.

Kwanza nichukue nafasi hii, kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo, Naibu wake, Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, kwa bajeti nzuri sana na kwa kazi kubwa waliyoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa haraka kidogo. Serikali imeweka vipaumbele katika maeneo ya Kilimo, Miundombinu, Maji, Afya na Nishati na Elimu ambayo imetengewa fedha nyingi sana kuliko sekta nyingine, tunashukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti nzima ya Serikali inafikia trilioni saba lakini kama mahitaji yote yangekubalika, hii bajeti ingekwenda mpaka trilioni 12, ninaona imepunguzwa kwa ajili ya fedha tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchangia moja kwa moja jinsi ya kuongeza mapato ili tuweze kuwa na fedha na mahitaji yetu yote yaweze kutimizwa na hatimaye kuongeza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ambalo ninaliona ni la muhimu kulizungumzia ni kwamba Serikali itafute vitega uchumi mbalimbali kutokana na vianzio vyetu ambavyo ni vingi sana, kusema kweli nchi yetu ni tajiri sana. Tupanue wigo wa *investment* ili mapato yaweze kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazingatia maeneo matatu, tupanue wigo namna gani ambayo ni kilimo, viwanda kwa sababu kilimo kinakwenda na viwanda pamoja na utalii japo yapo mambo mengi kama mifugo, uvuvi, madini na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mingi tumekuwa tukiongelea suala hilo na kusema kwamba kilimo ndiyo kitatusaidia au tuongeze thamani kwa kusindika bidhaa zetu, tulete watalii na kadhalika lakini hebu kidogo tubadilishe staili na Serikali. Jukumu letu au jukumu la Serikali imekuwa kuitagaza nchi yetu, kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji, kukaribisha wawekezaji na pia kuwahamasisha wananchi waweze kuwekeza kwenye kilimo na viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mpaka sasa hivi bado tunakwenda taratibu ndio maana naona kuna umuhimu wa kubadilisha. Tutafute msaada, nikiwa na maana msaada wa mawazo, *consultants* ambao tutawachukua watusaidie mawazo. Jinsi gani na tuzingatie kitu gani sana ili tupate maendeleo. Nikisema hivyo, huyu mtaalamu tunaweza tukamchukua kutoka nje na ninasema nje kwa sababu unakuta wana *exposure* kubwa ya wawekezaji na vilevile wanajua maeneo ya kupata fedha.

Nitaomba Mheshimiwa Waziri asijibu kwamba tulikwishafanya hivyo kwa sababu najua Wizara ilikwishafanya hivyo lakini walimleta mtu ambaye siye anayehusika na sekta hizi. Ni watu ambao kweli walijitambulisha na wakawa wanatusaidia kuitangaza Tanzania kwenye *Congress,* tukafahamika vizuri na tukapata misaada kiasi kadhaa lakini tunaweza tukawachukua wale wataalamu wa Rais wa Amerika kwa mfano *Trade Representative* kwa Africa ambao wako pale Washington DC, ambao wale wamekuwa wakimshauri Rais wa Amerika jinsi ya kusaidia Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sasa hivi Kenya, Uganda, Lesotho na Swaziland wanawatumia watu hawa. Unampa *benchmark* kwamba sisi tusaidie katika eneo la kilimo, utalii na viwanda na tunataka utuingizie kwa mfano dola bilioni tano kwa kipindi cha miaka mitatu, huo ni mfano tu, mimi siyo *Accountant*. Mtaalamu huyo unamlipa vizuri, anakuja nchini mwako kwa miaka mitatu, anaweza akatazama eneo la kilimo, anasema sawa. Katika maeneo kadhaa wanafanya *test* hata ya udongo, wanatazama mazao gani yanaota maeneo gani na soko pia, wanafanya yote kwa pamoja. Je, tukilima kwa mfano nyanya, mihogo, mboga za majani, tutapata soko katika maeneo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu mtaalamu haishii hapo, akikuletea mwekezaji, anamsaidia mwekezaji huyo kupata fedha kutoka *IFC,* benki za kimataifa. Pesa za kuwekeza zipo nyingi sana, kinachotafutwa ni masoko na maeneo ya kuwekeza. Anakwenda pia mbali kuwafundisha wakulima kwa fedha ileile mtakayomlipa hapa Tanzania. Kwa mfano, unampata *farmer* mmoja mkubwa, unampa kuanzia Chalinze mpaka Morogoro, pamoja na *out growers* wa pale, Watanzania ambao watakuwa wanalima, wanawekeza vilevile katika kiwanda ambacho atakianzisha yule mtu na anatupa *down stream project,* kuanzia kilimo, viwanda mpaka masoko. Amefanya hivyo katika nchi ya Uganda, mfano uko hai ambao tunaweza pia tukaiga sisi Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ana uwezo wa kukuleta *multinational companies* kwa mfano *Delmont. Delmont* iko hapo Kenya, hapa Tanzania amefungua ofisi ya kuuza tu. Kuna wakati alikuja Tanzania akawa anataka shamba kubwa lakini kuwepo na *out growers* wengi. Tulijitahidi kumuonyesha kuanzia Segera mpaka Tanga, yale maeneo pale pamoja na *out growers* wa Muheza na wengine, matunda yetu yote yangekuwa yanasindikwa na wale wananchi majirani wangepata pa kuuza, tungekuwa tunauza *juice* ya Delmont tunayotengenezea Tanzania badala ya kuletewa kutoka Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ifike wakati tulete vitega uchumi katika nchi yetu kwa kutumia hawa wataalamu au anaweza akamleta *Henz Baked,* tukalima maharage yale

meupe tu, tuka *supply* Tanzania na nje. Kuna soko la *EU*, la *EBA* yaani *Everything But Arms*. Ili kufanikisha haya, ni lazima tuwe na huyu mtaalamu ambaye atatuongoza kufika huko. Soko tumeliongelea sana tangu tumepewa *certificate* nadhani ni mwaka wa kumi na moja lakini hatujaweza kutumia hili soko. Tuombe msaada kutoka kwa hawa wataalamu.

Kwa mfano Ghana, wao wamepewa kilimo cha mihogo na huu umekuwa mradi ambao unasimamiwa na Rais mwenyewe, *Presidential Initiative.* Pale Ghana wanalima mihogo wanapeleka *starch* nje na haifiki hata moja ya mia ya soko la mihogo linalohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba uamuzi huu uwe ni uamuzi wa Baraza la Mawaziri, ili Mawaziri wote kwa mfano ukitaka kilimo au viwanda, Waziri wa Viwanda anahusika, Waziri wa Kilimo, TAMISEMI, Maji na kadhalika wote wakusanyike na iwe Serikali imeamua. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, azingatie suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utalii, kwa mfano matatizo yetu kama ni hoteli, miundombinu au kama ni *market,* hii *Hilton Four Seasonal Hotel Intercontinental,* wakaja hapa na hapohapo atatusaidia katika kufungua ofisi huko Europe, America na Asia kama zilivyokuwepo zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa *Middle East,* inasikitisha tumeweka *trade* ya *Attachee* pale Dubai, amefanya mpango, kuna watu wenye pesa nzuri wanataka kuja hapa kwa utalii lakini tunavyoongea sasa hivi, ametuma habari huku nyumbani mpaka sasa hivi hakuna mtu ambaye ameweza kupeleka *response* kwamba anataka watalii kutoka Arabuni. Hilo halihitaji mtaalamu, ni la kwetu wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiongezea kwa upande wa viwanda, kuna viwanda mbalimbali hapa nchini ambavyo havipo, hebu tujiulize kitu kama *Blue Band,* tunakula *Blue Band* ya Kenya ambayo imetengenezwa na kampuni ambayo si yetu, kwa nini tunashindwa sisi kufanya hiyo? Lakini mtaalamu huyo atatuelimisha, akiwaambia Watanzania kuna *get away* kutoka hapa kwenda soko la *SADC* la watu 400, nina hakika mwekezaji yeyote atakubali kuja hapa akijua kuna soko na pesa pia atatafutiwa kutokana na mikopo ambayo iko mingi duniani. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri azingatie hayo ili tuhakikishe kwamba angalau tumebadilisha hiyo staili ya kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja katika eneo la jiji la Dar es Salaam. Alikuja mwekezaji na mtaalamu mmoja anaitwa De Soto. Alieleza vizuri maana ya *dead capital* na ikaonyesha kwamba tunaweza kuwa na majumba mengi lakini yakawa hayana thamani. Katika jiji la Dar es Salaam, jimbo langu la Kawe, maeneo ya Masaki, Mikocheni, Kunduchi, Tegeta, Mbezi na Kawe yenyewe kuna mali za thamani sana, zinazidi hata bilioni 500. Hii ni idadi ya nyumba 13,000 lakini thamani yake ni ndogo kutokana na miundombinu hafifu ambayo iko katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili wananchi waweze kujiendeleza na nyumba ziwe na thamani, ninaomba Serikali ifanye suala hili kama la dharura. Tunashukuru sana kwa kutusaidia kupata barabara kutoka Oasisi kwenda kule Africana lakini ili kuongeza thamani ya barabara hii na mali zilizopo katika Jimbo hilo ziongezeke thamani, wananchi wako tayari kulipa *property tax* ili waweze kufanikiwa kutengeneza hiyo miundombinu ambayo ni hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo linakera sana, ni msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam. Inasikitisha! Wananchi waliniomba nipande gari mimi mwenyewe niendeshe kuanzia Mwenge mpaka Kunduchi kuanzia saa 12.30, ilinichukua masaa matatu katika foleni hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali ilione hilo, tujaribu kusaidia katika kutatua tatizo hilo. Barabara zinazotoka nje ya jiji la Dar es Salaam, ni muhimu sana zikaboreshwa na zikawa *due carriage way* kwa mfano, utafiti umekwishafanyika kujaribu kuifanya barabara kuanzia pale Mwenge mpaka Kunduchi na mbele ya Kunduchi kidogo angalau ziwe barabara mbili na hili inawezekana. Suala hili ni la muhimu vinginevyo itachelewesha sana kupanuka na kuongeza uchumi kwa sababu zile *lost hours* ambazo zinatokea pale, ni upotevu mkubwa sana wa juhudi za watu. Tusingojee mpaka ifike mahali ambako Dar es Salaam inashindikana kabisa, inakuwa kama nchi nyingine ambazo unasubiri inashindikana, kama tunaweza kuongeza mapato kama nilivyoongelea nyuma katika hili suala la wataalamu, hawa watakaotuongezea, tutaweza kufanikisha na kupata hizi pesa bila kuwa na wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo ninataka kuliongelea ni kuhusu Bandari. Watu wamehamia Mombasa, makontena yanakuja lakini wengine wanaona ni rahisi zaidi kupitishia nchi jirani. Sisi Tanzania hatuko *land locked,* tuna bahari lakini kuna nchi ambazo ni *land locked* zinazotuzunguka nyingi, tutumie fursa hii ili tuweze kupata mapato. Kwa mfano, hivi karibuni nilikuwa Bandarini, tumekuta kwamba maeneo ya kuweka makontena ni finyu. Tuna eneo pale la NASACO na hata UDA inasemekana wako katika mazungumzo, haya mazungumzo yanachukua muda gani, kwa nini yasifanyike haraka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilisahau kulisema ni kuhusu tafiti zilizofanyika, za Serikali. Tafiti zimefanyika na zimefadhiliwa na mashirika ya kimataifa katika Wizara mbalimbali. Ninaomba Serikali itoe hizi tafiti, iunde *Task Force* ambayo itatizama *implementation* hata sera ambazo zimepitishwa ili zisibaki kwenye *shelves* kwa sababu wafadhili wetu hawa wanatupa pia na pesa ya kufuatilia utekelezaji. Wangezitoa hizo tafiti mbalimbali ili ziweze kutekelezwa na wananchi wenyewe wale ambao tunawaita *stakeholders* kuliko kukaa na kusubiri kwamba Serikali itazitazama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tafiti moja ilifanyika kuhusiana na ulimaji wa *palm* ambao ungeweza kutusaidia kupata *crue oil* ya kutengeneza mafuta ya kula.

Mheshimiwa Mwenyekti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Rita Mlaki, Mbunge wa Kawe kwa Mchango wako na Msemaji wetu wa mwisho kwa mchana huu atakuwa ni Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa.

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Wabunge wenzangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Watendaji wake lakini bila kuisahau Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha, Uchumi na Mipango, kwa kazi yao nzuri ya kuandaa bajeti hii. Labda nianze kwa kusema na mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo na mimi nina maoni yangu ambayo kama itaonekana inafaa, basi Mheshimiwa Waziri atayafanyia kazi. Nianze na sekta ya kilimo kwa maana ya chakula. Katika taarifa ya hali ya uchumi duniani, tumeambiwa kwamba kuna viashirio mbalimbali ambavyo vinaonyesha kwamba uchumi wa dunia siyo imara na siyo imara kwa sababu kuna upungufu mkubwa wa chakula, hali ya hewa kwa maana ya uzalishaji haikuwa nzuri lakini pia nchi tajiri kutumia nafaka kwa wingi kuzalisha nishati kwa maana hiyo matokeo yake ni kupanda kwa bei ya chakula duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiunganisha na changamoto inayoikabili nchi yetu katika hali ya uchumi, inasema kwamba hivi sasa uchumi wetu uko katika hali ngumu kutokana na kupanda kwa kasi kwa bei ya mafuta ya petroli, mbolea, malighafi za viwandani kwa. Kwa hiyo, tunalazimika kuchukua hatua za dhati kuzalisha chakula cha kutosha ili kujihami na madhara ya changamoto hiyo. Lakini pia ukuaji yaani ongezeko la 2.9%...

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hizo, kwa kweli ni dhahiri kabisa nilitegemea hata bajeti ya kilimo ingekuwa kubwa. Tanzania tunayo fursa kubwa kwa kweli ya kuleta mapinduzi ya kilimo lakini mapinduzi haya hayawezi kuja na mabadiliko ya namna tunavyowekeza na kuendeleza sekta hii nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye jedwali namba tatu, la bajeti hii, mchanganuo wake unaonyesha kwamba mwaka jana Wizara ya Kilimo ilitengewa 6.2% lakini mwaka huu 6.4% lakini ndiyo tumeshaambiwa changamoto za hali ya chakula duniani ndiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, nchi yenye njaa au watu wenye njaa, sidhani kama watayafikia malengo ambayo yanakusudiwa, hilo pato la Taifa, sidhani kama litafikiwa. Lakini pia sidhani kama sekta ya elimu, Walimu watafundisha na kama watoto watasoma na kama watakuwa na akili kwa kuwa hawajashiba! Lakini pia sekta ya afya, nafikiri hata bajeti haitatosha kwa sababu magonjwa yataongezeka. Kwa hiyo, kwa kweli kuna haja ya kuangalia upya. Mikakati yetu tunayoweka ni mikakati mizuri na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, tumeambiwa atakuja nayo lakini isiishie kwenye vitabu, ni lazima tuitekeleze. Sasa na itoshe na safari ya kuleta mapinduzi ianze katika sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa na Wataalamu hapa, kuna mazao ambayo kwa kweli yana dalili nzuri kabisa ya kuongezeka kwa bei lakini pia ni ya chakula. Kwa mfano mahindi, mpunga, muhogo, ngano, mazao yote jamii ya maharage na mboga. Mazao hayo kama yatalimwa kitaalamu, tutaweza wenyewe kujitosheleza lakini pia tunaweza tukauza nje na tukapata mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naingia sekta nyingine, nayo ni vita dhidi ya UKIMWI. Mwaka juzi 2006/2007, wastani wa kiwango cha maambukizi ilikuwa kwenye asilimia saba nukta kidogo lakini mwaka jana asilimia bado iko palepale, imeongezeka na kuwa asilimia 7.4. Tunaambiwa wastani wa asilimia sita ya maambukizi haya, yapo vijijini na asilimia 11.9 mijini. Kwa maana nyingine kati ya watu nane wa Tanzania katika asilimia mia wana virusi vya UKIMWI. Sasa idadi ya Wabunge hapa tuko mia tatu na zaidi watu kama 22 au 23 wameathirika, ni hatari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia kwenye bajeti, mwaka jana jedwali hilo la tatu, HIV/AIDS, ilitengewa asilimia 1.8 yaani bilioni 107.7, mwaka huu imetengewa asilimia 1.5 sawa na bilioni 107. Ongezeko la waathirika linaendelea lakini bajeti inashuka, sasa sijui mambo haya vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini karibu kila Wizara inapewa pesa yaani inatengewa pesa za UKIMWI lakini je hizi pesa za UKIMWI zinawafikia walengwa? Ni pesa nyingi sana zinazotengwa lakini bado tunaaona asilimia ya waathirika inaendelea kupanda juu. Sasa basi imefika wakati Serikali ibadilishe mbinu zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi katika semina moja, tuliambiwa Serikali za Mitaa zinatengewa 5% tu ya bajeti kwa ajili ya UKIMWI. Serikali za Mitaa zina watu wengi na tena zinacheleweshewa fedha hizo na wakati huo hela zinatumika sivyo. Lakini pia tumeambiwa kwamba katika matumizi ya pesa hizo kwa mwaka 2007/2008, ni 3% tu ndizo ambazo zimetumika vizuri lakini kuna asilimia zaidi ya tisini hazijulikani zimetumika vipi, *are we serious*? Naomba Serikali iliangalie suala hili kwa makini la sivyo nchi nzima itakuwa na maradhi ya UKIMWI na hatutafikia malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie kuhusu suala la jinsia, ijapokuwa Wabunge wengi hasa akina mama waliolizungumzia, wanadai *fifty fifty* lakini bajeti imeshaletwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 31 wa taarifa ya uchumi, niipongeze sana Serikali kwa kupanga hii programu ya kuwawezesha akina mama na wao kuwa washiriki wakubwa au wadau wakubwa katika maaamuzi katika ngazi zote za utendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada hizi zisiishie kwenye kitabu na ikiwezekana ifikapo mwaka 2015 angalau 45% katika ngazi zote akima mama wawe wanashirikishwa. Akina mama wanaweza na wengi sifa wanazo. Kwa hiyo, tusiwabeze, tuwaendeleze na Serikali iwape uwezo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekti, nizungumzie kuhusu Mfuko wa Maendeleo wa Jamii yaani *TASAF*. Niendelee kuipongeza Serikali, kwa kweli imetusaidia sana wananchi kutatua shida zetu katika miradi mbalimbali lakini fedha hizi kidogo zinakuwa zinachelewa. Miradi inapoibuliwa, inachukua muda mrefu kuletwa, inafika hata miezi minne bila kuletwa. Sasa urasimu huu ungepunguzwa kidogo kwa sababu kila tukikaa *inflation* ya pesa inaongezeka sasa hizo pesa hazitaweza kufikia malengo ambayo yanakusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mheshimiwa mwenzangu amesema kwamba mchango wa 20% kwa wananchi wetu na hali ya sasa, nafikiri ungefikiriwa upya, uwezo unakuwa mdogo. Mwananchi ukimwambia akajitolee anaangalia kwanza yeye hajapata kilo moja ya sukari wala mkate wake, kwa hiyo, *attendance* haipo matokeo yake sasa wawakilishi yaani Mbunge kwa upande wetu Zanzibar mwakilishi ndio mzigo unatuangukia inabidi sasa tutoe pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwamba ule Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo, hapa ndiyo unapostahili kwa kweli japokuwa sijaona chochote mwaka huu lakini ninapenda Mheshimiwa Waziri au Waziri mhusika atueleze maendeleo ya mfuko wetu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kama Kenya, ina wafadhili na hata Uganda nayo lakini zina mifuko hii. Sasa inakuwaje sisi Tanzania tuambiwe wafadhili hawataki na kadhalika, tuna nini? Pesa hizi haziendi sisi mifukoni mwetu zinakwenda kwenye maendeleo na mikakati imeshafanywa ni kwa namna gani pesa hizo zitapelekwa kule. Wewe Mbunge ndiyo Mwenyekiti lakini huzioni pesa utakaa na Kamati yako tu. Naomba sana suala hili liangaliwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichangie suala zima la bajeti hii kuhusu Tume ya Pamoja ya Fedha. Waheshimiwa wenzangu waliotangulia, wamezungumza na mimi nitaongezea si vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana katika bajeti, tuliambiwa kwamba Tume hii wakati bajeti inasomwa ilikuwa imeshawasilisha mapendekezo yake Serikalini ili kuyapitia na kupata muafaka na kila Serikali ilipewa majukumu yake. Lakini cha kushangaza katika *paragraph* ya 31 ya bajeti naomba ninukuu:-

*"Serikali ya Muungano na ya Mapinduzi ya Zanzibar zinaendelea na zoezi la kupitia na kuchambua ripoti ya Tume ya Pamoja ya Fedha kuhusu vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano kama sehemu ya mchango huo, Tume ya Pamoja ya Fedha inachambua maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi za ziada ili kuziwezesha Serikali hizo mbili kufikia maamuzi kuhusu mapendekezo ya Tume."*

Sasa hii *paragraph* inajichanganya kwa kweli, hujui sasa ripoti iko Tume au iko Serikalini. Mheshimiwa Waziri wakati ana-*windup*, nataka ufafanuzi hapa, Tume imepeleka au Tume bado inachambua kwa sababu huu ni mwaka wa tatu sasa na matatizo yanaendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, …

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, unga mkono hoja, hiyo ni kengele ya pili sasa.

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nashukuru sana tumemaliza kipindi cha asubuhi na ninaomba tu nimtaje Msemaji wetu wa kwanza tutakaporudi tena leo jioni. Msemaji wetu wa kwanza kwenye agenda yetu atakuwa ni Mheshimiwa Benson Mpesya, ataanza na wengine watafuatia kadri ya orodha itakavyotayarishwa na Katibu wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(*Saa 07.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni*)
(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba niwataje wachangiaji watakaoanza wanne wa mwanzo, nao ni Mheshimiwa Benson Mpesya, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa Hilda Ngoye na Mheshimiwa Castro Ligalama nao wajiandae. Kwa hiyo, moja kwa moja namwita Mheshimiwa Benson Mpesya, Askofu.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu ya Waziri wa Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kusimama hapa nikiwa bukheri wa afya njema. Lakini pia nitumie nafasi hii, kuwashukuru wapiga kura wangu wote wa Mbeya Mjini ambao naamini kabisa watakuwa kandokando ya *TV* zao wakijua Mbunge wao anazungumza nini na anawazungumzia nini katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia michango mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge, wamezungumza mengi, makubwa, mazito na wakati mwingine ukisikiliza

sana, unaweza kufikiri kwamba hakuna kitu kinachoendelea katika utendaji wa Serikali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia nafasi hii, kwanza kabisa kumwelezea Waziri Mkulo kwa muda mfupi niliomwona pamoja na Manaibu wake wote wawili. Kwangu, namwona ni mtu mtulivu na Manaibu Waziri wake wote wawili ni watulivu. Nimemwona kama mtu msikivu na Manaibu wake wote wawili ni wasikivu. Nimewaona ni watu wanaochanganyika na watu, kwa hiyo hawa ni watu wa watu na si ajabu sasa wamekuja na bajeti ambayo kwa kweli imezingatia usikivu wao, utulivu wao na mengi ambayo tumeyazungumza. Nawapongeza sana kwa kuileta bajeti hii pamoja na ndugu zangu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwapongezi hivi hivi tu, nawapongeza kwa kile ambacho tunakiona kimefanyika. Bajeti hii inaonekana imezingatia mwaka jana tuliangukia wapi na sasa tunakwenda wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti bila kuwepo makusanyo ni kazi bure. Kwa nafasi hii, napenda niwapongeze sana ndugu zangu wa *TRA,* akiwepo ndugu yangu Kitilya, kwa kazi nzuri ya kuimarisha mapato ya nchi yetu. Lakini nataka niseme kwamba hapo walipofikia hapatoshi, naamini kabisa wanaweza kukusanya zaidi, ingefaa sana tungefikia kwenye Sh. 500bn/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ambao tuna ng’ombe mmoja wa maziwa, tunafahamu fika ukitaka ng’ombe akupatie maziwa mengi, unapomkamua lazima uwe na pumba au mashudu karibu, ndipo anapotoa maziwa mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mwaka jana, wakati wa sikukuu ya mlipa kodi, mgeni rasmi alikuwa ni Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wafanyakazi wa *TRA* nchi nzima walitoa ombi lao la kutaka angalau kwa kazi nzito wanayoifanya, wapatiwe *bonus*. Nami nasema kwa kazi nzuri hii na ili wafikie malengo mazuri, naomba Serikali iangalie namna ya kuwaenzi hao wafanyakazi wa *TRA* kwa sababu ni ombi ambalo walikuwa wameomba la kupatiwa *bonus*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimesimama nikiifurahia bajeti hii, naomba niwaeleze wapiga kura wangu, kwa nini naifurahia bajeti hii na naiunga mkono. Naiunga mkono kwa sababu, kwanza kabisa, kwa mara ya kwanza katika historia ya bajeti nilizoziona, Uwanja wa Ndege wa Songwe, umepewa Sh. 13bn/=. Kwa bajeti ya mwaka huu tumepangiwa Sh. 13bn/= kwa ajili ya kumalizia Uwanja wa Kimataifa wa Songwe. Naishukuru sana Serikali yangu kwa mtazamo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hilo tu, Serikali imefanya kazi ya ziada, imeshamaliza mchakato wa kumpata mkandarasi na *BADEA* imeshatoa *no objection*. Naiomba Serikali sasa ili kuepukana na kupanda kwa gharama za ujenzi wa kila siku, mkandarasi huyo afike *site* pale Songwe ili aanze kazi mara moja. Uwanja ule ni kwa ajili ya kuibua fursa mbalimbali za kiuchumi ambao ukikamilika naamini majirani zetu wa

Malawi, Zambia na DRC, watapata fursa ya kutuingizia fedha za kigeni. Naipongeza sana Serikali kwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga bajeti hii mkono kwa sababu nataka wanafunzi wangu wa Shule ya Sekondari ya Loleza, Iyunga, Mbeya *Day* na zingine zote, waendelee na masomo yao kwa sababu ni bajeti itakayowawezesha wao kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile bajeti hii ndiyo imebeba dhamana ya mikopo ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu. Ili wanafunzi hawa waende kusoma na kuja kututumikia baadaye wanahitaji bajeti hii ipite. Sababu zote hizi, zinanilazimisha niiunge mkono kwa dhati kabisa bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, napenda nirejee hasa katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 42. Pamoja na mazuri yote ya bajeti, naomba nitoe ushauri wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 42 tunazungumzia juu ya kodi za magari, nianzie na pale (c), magari yenye CC 1500 mpaka 2500. Magari haya ndiyo yale ambayo mengi ni *pickup* wanazotumia wanavijiji kule vijijini, ni *taxi* ambazo zinawasaidia wagonjwa wetu. Nilikuwa naangalia juu ya punguzo la malipo, niliona wamepunguziwa kama asilimia ishirini tu lakini (d) ambapo ndipo yalipojaa magari ya Waheshimiwa Wabunge ya kuanzia CC 4000 mpaka 5000, punguzo lake ni karibu asilimia sitini na saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuwatendee haki Watanzania na hasa watu wa hali ya chini. Haitaeleweka na hawatatuelewa, kwa nini kwenye ngazi hii, labda mpaka nipate maelezo, punguzo limekuwa ni karibu asilimia sitini na saba lakini hapa ambapo kuna wanyonge ambao wanatumia *pickup* hizi kwa ajili ya kusafiria, tumewapunguzia kwa asilimia ishirini tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kana kwamba haitoshi, kipengele (d) ambako ndiko kwenye malori na mabasi, punguzo lake ni kama asilimia kumi na nne tu. Watakaoumia, ni wananchi wetu ndio wanaotumia malori hayo kubeba mazao yao. Watakaoumia ni wananchi wetu ambao ndio watakaopanda mabasi hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi, niliwasikia kabisa *DABOA,* wakitaka wapandishe nauli kwa asilimia thelathini na wanataka wapandishe kabla ya punguzo halijawafikia, kabla hatujapitisha rasmi hii bajeti. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ayaangalie maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kuna kutofautiana kwa asilimia, huyu asilimia ishirini, huyu mmepunguzia asilimia sitini na saba, huyu kumi na nne, hakuna mtu atakayeelewa ulikuwa unatumia vigezo gani katika punguzo hilo? Kwa haraka haraka watu watafikiri kwamba hapa kwa sababu ndiyo magari ya Wabunge yapo mengi

wamejipendelea wao. Nafikiri upendeleo wetu sisi uwe ni kwa watu wa chini, wanyonge ambao uwezo wao ni mdogo. Kwa hiyo, naomba eneo hili liangaliwe ili tufanye marekebisho na bajeti hii kwa hakika imfae mtu wa hali ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakikutangulia watu wakasema mengi, yanayobaki yanakuwa ni ya kudondoza. Kwa hiyo naomba nizungumze yale mengine ambayo yanaonekana ni madogo lakini yanakera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hii sarafu, umezuka mtindo kwamba baadhi ya taasisi zetu za Serikali zinazikataa baadhi ya sarafu tulizonazo ambazo ni malipo halali na hili limekuwa kero kwa wananchi wa ngazi ya chini. Wakizipeleka benki zinakataliwa kwamba hizi sarafu hatuzitambui, basi ni vema Serikali ikatamka ni sarafu zipi ambazo imeamua kuzifuta rasmi kwamba si malipo halali katika matumizi na kadhalika. Hata benki zetu na hata Benki Kuu zimekuwa zikikataa sarafu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inapofika mahali mtu amekusanya zile sarafu hasa hizi *SACCOS* ambazo marejesho yake yanaweza kuwa Sh.110/= au 100.20/= au Sh. 100.50/= wamejikuta wengine wana laki tatu au nne ambazo ni sarafu na hawakubaliwi kubadilisha ili ziwe noti.

Naomba mwongozo wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha atuambie ni sarafu zipi ambazo zimefutika. Vijijini huko bado hizo sarafu zinatumika! Sasa unaposema zisitumike maana yake unawaongezea ukali wa maisha, unafanya kile alichotakiwa anunue kwa Sh. 50/= sasa alazimishwe kununua kwa Sh. 100/= au Sh. 200/=. Sasa hii inaongeza ukali wa maisha, naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nimeangalia katika miji kama mitatu mikubwa Mbeya, Shinyanga na Mwanza, naomba niulize kwa nini hawa *Bayport Financial Services* wanalalamikiwa kila mahali na kundi kubwa la watu?

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, wananchi wanapoilalamikia taasisi ya kifedha kama hii, ni vema taasisi hiyo ikajitokeza, ikaeleza ni kitu gani kinafanya wao na wateja wao wagombane. Pale kwangu Mbeya Mjini, ni kero kubwa sana, watu wanaandamana kwa ajili ya kulalamikia mikataba ya *Bayport Financial Services*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha afuatilie, ajue wanalalamika nini ili tuwaase watu wetu wasijiingize hovyo katika baadhi ya hizi taasisi lazima wajue ni kiasi gani cha riba kinatozwa na mikataba iwe wazi, wapewe nakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoonekana katika taasisi hii, wale wanaokopa hawapewi nakala ya kwamba umekopa kiasi gani na utawajibika kulipa kiasi gani na hasa Walimu wamekuwa ni *victims* katika tukio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema, Serikali isije kufanya makosa ya kukipuuza kilimo. Kipaumbele cha elimu na afya, mimi sikatai lakini nataka niwaambie katika mambo ya uchumi hizi zote ni sekta za huduma, zinazalisha lakini

matokeo yake tutakuja kuyaona mwishoni sana. Naomba ikiwezekana sekta hii ya kilimo iongezewe mara mbili ya hapa ilipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya kilimo imechukuliwa kama sekta, haijaangaliwa nafasi ya kilimo katika kudhibiti mfumuko wa bei, haijaangaliwa nafasi ya kilimo katika kutoa ajira, wala tusingekuwa na shida zile ajira ambazo zimeahidiwa na Rais wetu na Ilani yetu, zingepatikana bila matatizo kwa kuimarisha sekta hii ya kilimo. Tunakiangalia kilimo wala hatuangalii kwamba kilimo ndicho kinachoweza kutupatia malighafi za viwanda vyetu na fedha za kigeni ili kupunguza matumizi holela ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kilimo hicho hicho, tunapozungumza juu ya mapinduzi ya kijani, lazima sasa hivi Serikali ituambie ina mipango gani ya kuhakikisha kwamba mbolea inapatikana kwa bei rahisi zaidi kuliko miaka ya nyuma ili watu wazalishe zaidi. Naiomba Serikali na hasa nimwombe Waziri Mkuu, katika tishio hili la njaa kama mazoea yetu, ni vema sasa tukajipanga, viongozi tukatembelea yale mazoea ambayo tunaona yapo tuhimize watu kuzalisha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishaunga mkono, kwa hiyo nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba awali kabisa, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo au ya pili katika kuchangia bajeti hii ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Waziri wa Fedha na Uchumi pamoja na Manaibu wake na Watendaji wao wakuu katika maandalizi mazuri ya bajeti hii ya mwaka huu 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupungua kwa utegemezi katika bajeti yetu hii ya mwaka huu kutoka asilimia arobaini na mbili ya mwaka uliopita na kufikia asilimia thelathini na nne kwa mwaka ujao, ni hatua nzuri. Kwa hiyo, naomba niipongeze Serikali kwa juhudi hii ambayo imefanyika hadi tukafikia hatua hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya utegemezi, kwa kweli hatuwezi kwenda mbele, hata Mheshimiwa Waziri mwenyewe amekiri kwamba katika utegemezi huwezi kuendelea kufanya maendeleo unayotaka na ameonyesha wasiwasi kwamba inawezekana kabisa katika baadhi ya miradi ya maendeleo ikaathirika kwa sababu hatuna uhakika wa kupata fedha hiyo. Sasa hiyo ni hatari, lazima tuwe na uhakika wa kufanya mambo yetu wenyewe. Sasa kama kuna utegemezi wa aina hiyo, ni lazima Serikali ijitahidi kuchukua hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia machache, ambayo nafikiri Serikali inaweza kufanya ili kukuza uchumi wetu. Naomba nizungumzie machache kuhusu uwekezaji katika sekta za uzalishaji, nitaanza na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchumi wa nchi zote zilizoendelea, hakuna nchi ambayo imeweza kuendelea kwa kutumia kilimo cha kujikimu yaani *subsistence agriculture*, hakuna nchi ya aina hiyo. Kwa hiyo, kama tutaendelea kufanya hivyo maana yake tunarudi palepale na kuwa maskini moja kwa moja. Hapa kwetu wakulima wengi wapo vijijini na huko ndiko kuna *subsistence agriculture* na ndiyo maana tunaona vijana wengi wanatoka vijijini wanakimbilia mijini kwa sababu hiyo ajira yao kuu yaani kilimo haina tija kwa hiyo kwa vyovyote vile wanakimbilia mijini ili angalau waweze kuona mabadiliko fulani ambayo yanaweza kufanyika katika maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa napenda kurudia kupendekeza kwamba sasa tuamue kuanza kilimo cha mashamba makubwa yaani *large scale agriculture*. *TIC* pale kuna *land bank* ambayo ipo *idle* tu. *Land bank* ile inaonyesha kwamba kuna maeneo mengi sana, makubwa sana hapa nchini ambayo yangeweza kutumika kwa ajili ya kilimo, lakini kwa bahati mbaya sana maeneo hayo hayajaendelezwa, hayajawekewa miundombinu ya kutosha ili wananchi waweze kuwekeza katika kilimo cha *large scale*. *Large scale farming* ingetusaidia sana, moja, kwanza kukuza uchumi lakini vilevile ingetusaidia katika kuwaajiri vijana wetu ambao wanakimbilia mijini, wangebaki huko huko wakaajiriwa na sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kuendelea na *subsistence agriculture* labda kwa ku-*introduce contract farming* ambayo kama tutakuwa na wakulima wakubwa basi katika maeneo ambayo ni ya jirani wale wakulima wadogo wafanyiwe *contracts* za kilimo na hao wakulima wakubwa. Kwa maana hiyo basi, hata kilimo chao hao wakulima wadogo wadogo walioko jirani kitakuwa *mechanised*, wataweza kupata pembejeo za kutosha na kilimo chao kitaboreka kuliko hiki kilimo cha jembe la mkono, hatutafika hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha jembe la mkono tumekikataa miaka nenda rudi, sasa tuamue basi kuchukua hatua. Hivi tutakataa kila siku tutalalamika hatutaki jembe la mkono, jembe la mkono halitusaidii, mpaka lini? Naomba hivi sasa Serikali ifanye uamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie sekta ya mifugo. Sekta hii tunaisemea lakini tumeisahau. Leo hii Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Magufuli alikuwa anatamka takwimu za mifugo tuliyonayo hapa nchini. Idadi ya ng'ombe tulionao hapa nchini, ni kubwa sana, nafikiri karibu milioni kumi lakini haijatoa mchango wowote katika uchumi wetu, hata kidogo na hapa naona mifugo hatuisemei sana tupo katika kilimo tu, tuisemee na mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tungeamua kuiongezea thamani, tukaiboresha, tukaiuza nje kama wanyama lakini vilevile tungesisitiza kwa sekta binafsi kuanzisha viwanda vya kusindika nyama, leo hii tungekuwa tunazungumzia kuuza nyama iliyosindikwa au iliyoboreshwa nje ya nchi. Kwa nini kila siku tunasema Botswana wametupita, wanapeleka nyama yao South Africa na hata katika soko la *EU?* Leo sisi

hapa kwa nini tusichukue hatua za haraka?  Hiyo ni moja ya sehemu ambayo ingetusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo katika sekta za viwanda, tumesema viwanda vitashughulikiwa na sekta binafsi, *fine*, sekta binafsi itafanya lakini tumewa-*motivate* kiasi gani hawa wawekezaji katika viwanda, tumewasaidia namna gani maana unaposema sekta binafsi Mtanzania huyu wa kawaida unaweza kupata idadi ndogo sana ya watu kama hawa wa kuweza kujitegemea wenyewe kuweza kuwekeza katika viwanda. Kuwekeza katika viwanda hasa vile vikubwa acha vile vya kati hasa vile vikubwa, si kazi ndogo lakini ni lazima waanze kwa kuwa *motivated* na Serikali, iwasaidie na kuwapa vivutio vya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo vilevile maana yake unaongeza wigo wa maeneo ya kupata kodi na kuchangia katika uchumi wa nchi na pia unaongeza idadi ya ajira kwa vijana wetu, ndiyo ajira zenyewe hizi, viwanda ndio vinachukua watu wa namna hiyo. Lakini viwanda navyo tunasema kwamba sekta binafsi itashughulikia, *no*! Wewe kama Serikali *you are responsible*, hiyo sekta binafsi je, umeisaidia kwa kiasi gani?  *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutaweza hata kidogo kuzisaidia hizi sekta tulizoziwekea kipaumbele hasa hizi za huduma, maji, elimu, afya.  Huwezi kuzisaidia hizi mpaka uboreshe *productive sectors* hizi nilizozizungumzia.  Kwa hiyo, ni lazima tusisitize sana kuhakikisha kwamba hizi *productive sectors* tunaziimarisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto kubwa sana ya uhaba wa chakula na gharama zake katika dunia.  Hili tumelisikia na linaendelea kutangazwa sijui tunashtuka kwa kiasi gani.  Jibu la uhakika ambalo linaweza kutusaidia siyo la kutumia mvua bali ni la umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *National Irrigation Master Plan* yetu Tanzania ambayo tulishiriki wenyewe katika kuiandaa, tulijiwekea lengo la kulima hekta 405,000 ili kujitosheleza katika kilimo cha umwagiliaji lakini hivi sasa tunalima hekta 279,000 au zaidi kidogo tu.  *Okay* unaweza kusema angalau tumefikia kwenye nusu yake lakini naomba Serikali ijizatiti vizuri zaidi.  Katika mpango wa mwaka huu umwagiliaji inapewa kama Sh. 13bn/= kutoka Hazina, lakini naelewa vilevile Mikoa kupitia *D by D* nayo itapata fedha katika miradi ya *DADPS* na *DFID*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uzoefu wangu nilionao, fedha hii kule Mikoani si kidogo huwa ni nyingi kwa ajili ya umwagiliaji ule mdogo. Naomba hapa nitoe wito hasa kwa wenzetu wa TAMISEMI huko Mikoani na Wilayani, hii fedha inataka sana ufuatiliaji. Nina ushahidi, kuna mahali Fulani, fedha hii ilijenga nyumba badala ya kumwagilia.  Kwa hiyo, naomba sana, fedha hii ikifika kule ni nyingi lakini vimiradi vipo vidogo vidogo navyo vingesaidia katika suala zima la chakula lakini kuna tatizo la ufuatiliaji kama nilivyosema.  Naomba sana Mikoa itusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza hili kwa sababu gani?  Kwa sababu hivi sasa duniani kama ilivyotangazwa kwamba kutakuwa na njaa kuna baadhi ya nchi zimeshaanza kufungia chakula chao, hawatauza nje, sasa kama hawatauza nje hasa huko Asia tutakimbilia wapi? Maana yake ni kwamba, sisi wenyewe ni lazima tujitosheleze. Hili tusije tukaliona kama ni jambo la juu juu, mimi naomba sana tulishughulikie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, naomba niungane na wenzangu waliozungumzia asubuhi kuhusu kuongezeka kwa bajeti ya maji. Ninaomba sana asilimia tatu ni ndogo sana na tunaambiwa kwamba imepungua kwa sababu ya kukamilika ule mradi wa Kahama – Shinyanga, vijiji 54 labda na watu wale wachache wa pale Shinyanga kwa kweli ni vijiji vichache sana. Kwa hiyo, ninaomba sana, Serikali mara nyingi ina ukoko, tafuteni fedha nyingine ili kuongeza bajeti ya maji. Kila mtu hapa akisimama anaomba maji, sasa kama hatutakuwa tumelichukulia hili *seriously* itakuwa vigumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata pale Dar es Salaam, mimi siishi Dar es Salaam lakini nafika Dar es Salaam na watu wa Dar es Salaam bila shaka watakubaliana na mimi, maji hayatoshelezi kabisa. Lakini kuna bwawa lile la Kidunda kupitia *MCC*, halikupewa fedha. Maana yake ni kwamba sisi wenyewe lazima tujikakamue kama nchi. Ninaomba sana Serikali iongeze bajeti ya maji ili tuweze kujitosheleza kwa mahitaji makubwa sana yaliyopo. Wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam na wanawake wote nchini wakiwemo wa Mkoa wa Mbeya, wanahitaji sana maji kwa sababu wao ndio wanaoteka maji, ninaomba sana tuwasaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hotuba ya Waziri wa Fedha kwa asilimia mia, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamuita anayefuata, niseme tu kwamba majadiliano haya yanafuatiliwa na Watanzania wengi na si kila mmoja anaelewa ni nini hasa kinafanyika humu Bungeni. Kinachofanyika humu Bungeni, ni majadiliano ya Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na hoja ya Serikali iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha Alhamisi wiki iliyopita kuhusu mambo makubwa mawili. Moja, ni kujadili hali ya uchumi wa Taifa kwa mwaka 2007 na mwelekeo wa mpango wa maendeleo kwa mwaka 2008/2009. Lakini la pili, ni kujadili mapato na matumizi au kwa maneno mengine bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Basi baada ya maelezo hayo, naomba nimuite Mheshimiwa Castol Ligallama na Profesa Raphael Mwalyosi ajiandae.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda nimpongeze Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mkulo na Manaibu Mawaziri wake, Mheshimiwa Jeremiah Sumari na Mheshimiwa Omar Mzee, kwa kutuletea bajeti hii ambayo tunaijadili kwa wiki nzima hii.

Mimi mchango wangu utajikita zaidi kwenye kilimo, hususan nitaongelea kilimo cha wakulima wadogo wadogo hasa wa miwa.

Kabla sijaendelea, naomba ni-*declare interest,* mimi ni Mwenyekiti wa Bodi ya Sukari Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa miwa, wametoa mchango mkubwa sana tangu viwanda vyetu vibinafsishwe miaka kumi iliyopita. Katika viwanda vitano tulivyonavyo, viwanda vya Morogoro vya Kilombero na Mtibwa, ndivyo vyenye wakulima wa nje, vile vya *TPC* Moshi, hatuna wakulima wa nje yaani *out growers,* Kagera hatuna wakulima wa nje. Lakini Morogoro, Mtibwa na Kilombero, tuna wakulima wapatao 14,000. Kilombero ina wakulima wa nje 8,000, Mtibwa wana wakulima wa nje 6,000. Wakulima hawa ukiwachukulia katika familia za Kiafrika labda wana *support* familia ya watu sita. Kwa hiyo, takribani watu 84,000 wanakuwa wanategemea kilimo hiki cha miwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima hawa wana kilio cha muda wa miaka mitano. Wametulilia na sisi Wabunge wao tumepeleka Serikalini na napenda leo nitoe kilio chao hapa ili Waziri atakapojumuisha aeleze tuwaambie nini wakulima hao. Pamoja na mchango wao mkubwa katika uchumi wa Taifa hili na kutekeleza programu ya MKUKUTA kwa dhati, wakulima hawa wana tatizo la kutozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani katika gharama za uzalishaji. Amekopa, amepanda miwa yake, miwa imefikia umri wa kuvunwa pale anapokata gharama zile anazomlipa mkataji, Serikali inakuja inatoza asilimia 20 ya gharama zile kama *VAT*. Anapopakia kwenye lori kwa kutumia mashine za kupakilia ambazo wamenunua wao wenyewe, Serikali inatoza tena asilimia 20 ya gharama zile anazomlipa yule mwenye mashine ya kupakia ambayo ni ya Chama chao. Anaposafirisha kwenda kiwandani kwa kutumia gari, Serikali inatoza tena asilimia 20 ya gharama zile za *transportation* kufikisha miwa ile kiwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali hiyo hiyo katika jedwali la pili la Sheria ya *VAT* ya mwaka 1997, nafikiri inasema kwamba zao hili la miwa limesamehewa *VAT*. Sasa kama limesamehewa *VAT* na wakati huo huo hawa wanatozwa *VAT* na wakulima hao ni kama wakulima wa mahindi, hawaweki kumbukumbu ni wakulima wa kawaida hawa. Wana mashamba ya eka tatu, nne ila ni wengi, ndiyo maana unaona *acrage* ni kubwa kwa sababu wako wengi. Kwa hiyo, unaweza kufikiri pale wanapata hela sana, hawapati hela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mtalaamu wa kuandika miradi, ukifanya mchanganuo wale watu kitu wanachokitoa pale ni *negligible*. Kama wanaandika mradi, unaweza kusema siyo *viable*. Nitatoa mfano, kwa shamba liliko kilomita 10 kutoka kiwandani, ukiondoa gharama za kulihudumia shamba hili kwa kulima yaani kuna kulima, kukatua *harrow*, kuweka ile *ridges* na kununua mbegu na kupanda halafu unakuja kuongeza tena usimamizi, unaongeza gharama za kuhudumia miwa yenyewe lazima ufanye palizi, uweke mbolea uje gharama za uvunaji mwisho wa siku utakuta kwamba mkulima katika tani moja anapata shilingi 3050/= na wakati huo Serikali kwa sababu imeweka tozo ya uvunaji, ya upakiaji na ya usafirishaji, Serikali yenyewe

inachukua shilingi 2200/=. Kwa hiyo, mkulima angenufaika kama angepata Sh.2200/= na ile Sh.3050/= angekuwa na afueni kidogo.

Sasa huyu mtu analima kilomita 10 kutoka kwenye kiwanda, ukichukua yule anayelima kilomita 20, mapato yake utakuta sasa *VAT* inachukua shilingi 2514/= mkulima huyu anachukua shilingi 693/= kwa kila tani. Sasa unaona *VAT* inachukua zaidi. Ukichukua yule anayelima kilomita 30 kwa miaka miwili ya kwanza anapata *negative*, hapati kitu kwa miaka miwili kwa sababu amekopa atalipa mikopo basi yeye mwenyewe ataishia kuishi tu. Sasa kilimo gani, MKUKUTA gani huu tunataka kuwafanyia hawa wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hawa wamelia kilio chao na katika uzalishaji, wamejitahidi sana, hawa wakulima wadogo wadogo, wanashindana na mwekezaji. Ukiangalia kuanzia mwaka 2004/2005, kiwanda cha Kilombero kinazalisha miwa *metric tones* 622,000, hawa wakulima wadogo wanazalisha tani 588,000. Mwaka 2006, Kilombero wamezalisha tani 525,000 wakulima wetu waka-*surpass* wamezalisha 696,000 *metric tones,* wakawashinda wenye viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2006/2007, kiwanda cha Kilombero, kimezalisha tani 508 wakulima wetu pale kwa sababu ya ukame walizalisha tani 481, wale wenzetu wanamwagilia lakini wakulima wetu wanalima tu kinamna ngumu. Mwaka jana 2007/2008 Kilombero imezalisha tani 614,00 wakati wakulima wetu tani 668,000 sasa tunataka tuwakatisha tamaa hawa wakulima? Mtibwa vile vile karibu nusu kwa nusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, asilimia 52 ya miwa inayopelekwa kiwandani, inazalishwa na wakulima hawa wadogo wadogo. Sasa kwa kuwatoza zile tozo za *VAT,* mkulima wa kawaida, mkulima ambaye hana kumbukumbu kwa sababu *VAT* inatakiwa sijui upeleke kumbukumbu za *returns,* huyu ni mkulima mdogo kama yule wa mahindi hana mahali anapopeleka kumbukumbu, lakini yule mkulima wa kiwanda yeye ana-*keep record* mwisho wa siku anapeleka *TRA* ana- *recoup* zile gharama, anarudishiwa kama *input tax,* gharama zote zile za kukata miwa, za kupakia miwa na kusomba miwa, yeye 100% anazirudisha kwake. Sasa huyu mkulima wetu atajikomboa lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi Wabunge na vyama vya wakulima hao wadogo wadogo, tunapendekeza Serikali ifute mara moja Kodi hii ya Ongezeko la Thamani ili tumsaidie mkulima huyu ambaye hapati kitu chochote. Unakusanya kodi sawa kodi lazima ukusanye lakini lazima kuwe na raha. Tumeondoa Kodi ya Maendeleo kwa sababu ilikuwa inawanyanyasa watu walikuwa hawana cha kulipa bali walikuwa wanajikamua kwa kuuza kuku na mali zao. Hii nayo ni kodi kama ya nyanyaso na ya kusikilizia, nilivyokuwa naiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema ya kusikilizia kwa nini? Imekuja miaka minne, mitano iliyopita huko nyuma haikuwepo, kodi ya kusikilizia. Mtoza kodi atasema hebu tuweke kodi hii tuone kama kutakuwa na nini. *TRA* inapata mapato, wanaandika ripoti

yao kwamba wao Morogoro wamekusanya kiasi fulani, wanasifiwa, lakini wale watu umewaacha na hali mbaya, haiwasaidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoza kodi ya *VAT* kwenye gharama za kukata na kupakia na kusomba miwa kwenda kiwandani ni sawa na kutoza *VAT* kwenye zao la miwa kwa mlango nyuma. Kwa sababu Serikali hiyo hiyo imesema zao hili ni *VAT exempted***,** Serikali hiyo hiyo kwa huduma zile ambazo ni za uzalishaji inazotoza kodi ya *VAT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu ifahamike zao la miwa ni tofauti na mazao mengine, ukichukua zao la pamba, kahawa, chai ambayo yote yamepewa msamaha wa tozo la *VAT,* hayo mazao ukishavuna kitu kinachofuata labda ni ku-*grade* na kuuza. Zao la miwa ni tofauti, pamoja na kwamba kule *VAT* imechukuliwa kwenye usafirishaji, ukataji na upakiaji ile miwa haijawa na *value* bado mpaka inapokwenda kwenye kiwanda inachukuliwa inapimwa kiwango cha sukari kilichokuwa ndani ya miwa ile ndiyo *basis* ya bei, kiwango hicho cha sukari kinaitwa *renderment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kuwa umebeba miwa kutoka shambani ukapeleka kiwandani lakini *content* ya sukari ikawa ndogo lakini *VAT* imeshachukua hela yake. Wewe mkulima hutapata hela kwa sababu wakipima sukari yako mle kwenye miwa ni ndogo. *Renderment* yako inaweza kuwa 5% lakini mwingine akawa na 10% yule atapata hela nyingi. Hiyo ndiyo *basis* ya *charge.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunawaambia watu wa *VAT,* tumekaa kwenye mkutano, tukawaeleza wenzetu kwamba waangalie kwa sababu tunachouza pale ni utamu wa sukari siyo bua lile la muwa kutoka shambani, kwa hiyo, wanapoanza kuchukua kodi kutoka shambani, wanawaonea hawa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo la VAT la asilimia 20 inayochukuliwa nalo linatozwa kwa huyu mwenye kiwanda. Anakusanya *VAT* kwa niaba ya wakulima lakini yeya ana-*recoup.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumefanya nini baada ya kuchukua malalamiko ya wakulima wetu? Tukakutana kwenye mkutano tarehe 11.1.2008, tukaita wenzetu, wadau wote wa miwa, Wizara ya Kilimo, Bodi ya Sukari, Wabunge wa Mkoa wa Morogoro, Naibu Waziri wa Fedha wakati huo na sasa ndiyo Waziri mwenyewe, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, *Commissioner* wa *Domestic and Tax Revenue,* Mkurugenzi wa *Fiscal Policy* wote tukakaa, tukajadili na kupeana mkakati kwamba sasa turudi tutafute wataalamu wa kodi waandike andiko. Andiko ni hili hapa na liliwasilishwa kwenye Wizara ya Fedha tarehe 15/2/2008. Tunategemea sasa Waziri atakapofanya majumuisho, atueleze wakulima hawa tuwaeleze nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine baada ya kuachana na hilo ni kwamba nchi jirani, nyingine zinapata matatizo kama hayo, mwekezaji aliyewekeza Malawi kwenye kilimo cha miwa ndiyo huyu huyu aliyewekeza Tanzania Kilombero (Ilovo). Kule

anachofanya anakusanya *VAT* kama *input tax* anai-*claim* kama anavyo-*claim* ya kwake anawapa wakulima hela zao zile walizotumia kukata, kupakia na kusomba. Kwa hiyo, kama tutatumia *system* hiyo nafikiri hakutakuwa na tatizo na wakulima hawa watakuwa wameneemeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda kuchangia ni kwamba Jumamosi tulikuwa na semina hapa. Semina iliendeshwa na Shirika *SEKAB*. Shirika la *SEKAB* limeanzisha kilimo cha miwa Bagamoyo kwa ajili ya kutengeneza nishati ya *ethanol*. Mimi nilikuwa nafikiri kwamba kama tutaboresha mazingira ya kilimo cha miwa, vijana wengi walioko Dar es Salaam watahamasika kwa sababu pale Bagamoyo ni karibu na Dar es Salaam. Wale wanakusudia kulima miwa Rufiji kwa ajili ya kutengeneza *ethanol* na kuzalisha umeme. Basi vijana wengi ambao ni nguvu kazi inayokaa bure Dar es Salaam, vijiweni, wanaweza kuvutika kujiunga na kilimo hiki. Lakini hawawezi kuvutika kama mazingira yenyewe ni haya ya kukatakata *VAT* kwenye gharama za uzalishaji. Kwa hiyo, tukiweka mazingira safi, tutakuwa tumesaidia hata hawa vijana wetu ambao ni nguvu kazi inayongojea ajira kila siku pale Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kuchangia ni kuhusu mikopo ambayo tunaweza kupata kutokana na nchi sasa kukopesheka. Napendekeza kwamba mikopo hiyo iwe kwenye miundombinu tu ya barabara kwa sababu nchi yetu itaingia kwenye uzalishaji mzuri baada ya kuwa imeongezwa Mikoa (sasa iko Mikoa nane) ambayo imepewa jukumu la kuzalisha chakula nchini, Mkoa wa Morogoro ukiwa mojawapo. Sasa ukiwa na fursa za barabara, mazao ni rahisi kwenda kwenye soko na tunaweza tukapiga hatua haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza mikopo ambayo itapatikana kwa kuweka *sovereign bonds,* ielekezwe zaidi kwenye miundombinu na miundombinu hiyo iletwe hapa Bungeni kwamba ni wapi na wapi ili tukubaliane sisi wote kwamba kunakuwa na *network,* mgawanyo wa nchi nzima kufuatana na fursa za mahali ambapo kilimo cha namna fulani kinafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Castor Ligallama kwa mchango wako ulioutoa. Sasa namuita Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Festus Limbu.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba mapema kabisa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia kwa sababu kwa jinsi bajeti ya safari hii ilivyoandikwa, ni tofauti kabisa na nyingine za nyuma. Mimi binafsi, naona ina mwelekeo tofauti ambapo kadri tunavyozidi kuendelea, itatufikisha mahali pazuri. Ndiyo maana ninaiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado nitakuwa na mambo mawili, matatu ya kuchangia kwa lengo la kuboresha vizuri zaidi na kutaka ufafanuzi wa hapa na pale.

Mchango wangu, kwa sehemu kubwa, utajikita kidogo kwenye mambo ya mazingira, kwa sababu mimi ni mtu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze kuchangia kwenye suala la hali ya uchumi wa Taifa, kipengele kinachohusu Hifadhi ya Mazingira, kipo kwenye ukurasa wa 31, kifungu namba 58 na 59 ambapo tunaelezwa kuwa Serikali itaendelea, naomba kunukuu kifungu cha 58 kinasema:-

*"…kutekeleza Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na vyanzo vya maji, kwa kufanya uperembaji, underline ni yangu, wa utekelezaji wa mkakati huo katika Mikoa ya Mbeya, Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Lindi, Tabora, Kagera, Singida, Iringa, Manyara, Kigoma, Mwanza, Ruvuma na Morogoro".*

Jumla ni Mikoa 15. Kwa hiyo, katika Mikoa 15 wamefanya uperembaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuzungumzia hapa ni kwamba, maana ya kuperemba, ni ku-*monitor*, ndiyo maana ya kuperemba. Huwezi ku-*monitor* kitu kusipokuwa na *base line information* au *base line data,* una-*compare* mwaka fulani na *base line year* kwamba mazingira ya wakati ule yalikuwa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika Mikoa 15 iliyozungumziwa na hiyo mingine inayokuja, sijaona ripoti inayoonyesha hali ya mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji katika Tanzania. Sijawahi kuona hiyo ripoti inayosema katika Mkoa wangu wa Iringa, mazingira ya mwaka huu tunaoanzia kuperemba, *base line data* inasema vyanzo vya maji vimeharibika kwa kiasi hiki, mmomonyoko wa ardhi katika Mkoa ule, uko hivi na maeneo ni haya na ramani inaonyesha mazingira ya mahali pa kuanzia ipo. Unaangalia mabadiliko kila baada ya mwaka mmoja na kuendelea, hiyo ndiyo inaitwa *monitoring*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijawahi kuona ripoti kama hiyo, kama ipo basi tuonyeshwe na kama haipo basi suala zima la kusema wanafanya uperembaji hakuna kitu kama hicho. *Data* ile na kitu wanachotupa hakina tija. Haina tija kwa sababu haina msingi wa kulinganisha. Kwa hiyo, tunafanya kazi ya bure, tunatwanga maji kwenye kinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitaomba kwa sababu limezungumzwa kama kisera hivi, wakionyesha hiyo *base line data,* nitashukuru na nitaondoa hiyo hoja lakini kama hakuna, basi uperembaji unaoendeshwa hauna tija na hauna maana na hautuletei faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni msingi na malengo ya uchumi na maendeleo ya jamii katika kipindi cha muda wa kati. Katika ukurasa wa 40, kifungu 74(iii) kinasema:-

*"Ukuaji wa shughuli za kiuchumi za kilimo (mazao, mifugo, uwindaji na misitu) unategemewa kuongezeka kutokana na kuboreshwa kwa miundombinu vijijini…"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, msingi wetu ni kilimo, ufugaji pamoja na mambo ya misitu na uwindaji. Vitu hivi tukivifanyia kazi na kuboresha miundombinu kwenye vijiji, vitakuwa msingi wa kutuletea maendeleo, tuna-*jump, in spring board* kwa kutumia vitu hivi, tunaweza ku-*move forward.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuainisha msingi huu unaozungumziwa hapa na suala zima la ongezeko kubwa la watu hapa nchini la asilimia 2.9 *per annum* ambapo ipo kwenye kifungu cha 77, ukurasa wa 44.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kuhusiana na kutumia vitu hivi kama vigezo, sipingi lakini ninachosema, tumejifunza kutokana na kujengwa kwa Daraja la Mkapa maana tunazungumzia kuboresha miundombinu. Tulipojenga Daraja la Mkapa, wote tunajua madhara yaliyotokea Kusini mwa Tanzani kwenye misitu, uharibifu wa misitu, kuvuna ovyo magogo na kuyasafirisha bila tija na Serikali haikupata faida yoyote, lakini rasilimali zetu zimekwenda. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unapofungua njia hizi kwenye vijiji bila kuwa na mikakati, itakuletea matatizo kweli kwenye rasilimali hizo za misitu na mali za asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichotaka kusema mimi ni kwamba hata kwenye uwindaji tumekuwa tukihoji hapa, uwindaji huu ukishaingiza miundombinu mpaka vijijini na mpaka kwenye mapori makubwa, unasogeza wawindaji haramu wanaenda kuvuna rasilimali zetu bila utaratibu wowote, hii italeta shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeangalia upanuzi wa kilimo kutokana na wingi wa watu. Kilimo kinapanuka, tunavunja mapori na maeneo makubwa tunayaweka chini ya kilimo, tunaharibu bioanuai ingawaje tunahitaji kula, lakini hakuna utaratibu wa kuainisha wingi wa watu na mahitaji ya watu hao kwa ajili ya kilimo na makazi na mahitaji mengineo ya rasilimali tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba je, kama kweli tunataka kuboresha miundombinu vijijini na tutumie misitu, ardhi, mifugo na uwindaji kama *spring board* ya kutuletea maendeleo zaidi, huko tunakokwenda tumejiandaa vipi kuhakikisha kwamba yaliyotokea Kusini mwa Tanzania na suala la magogo hayatokei kwenye maeneo mengine ambayo tutayafungua? Sasa nitataka kupata maelezo hayo, tumejiandaa vipi na tutaweka mikakati gani, ni kama *regulatory impact assessment,* usiweke tu sheria, tutatumia hiki ku-*harvest resources*, lakini tumeweka mikakati gani kuhakikisha kwamba tunazuia uharibifu ambao hautakiwi utokee?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Makadirio ya Mapato na Matumizi, nataka nianze kuzungumzia suala la Motopoa. Kwanza, napongeza jinsi Wizara ilivyoona umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwa kupunguza ukataji kuni na kutumia mkaa na

pengine hata mafuta ya taa. Sasa walichokizungumza pale wame-*recommend* Motopoa, utumiaji wa gesi na wamepunguza kodi kule kwenye Motopoa, wamepunguza kodi kwenye mitungi ya gesi na gesi yenyewe na kwenye magunia na kadhalika na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Motopoa nimeambiwa na nimethibitisha kuwa kweli itakuwa rahisi kununua lita moja ya mafuta ya Motopoa lakini ili kupika mlo mmoja mzuri wa maharage kwa mfano, unaweza ukahitaji lita tano ili maharage yaive. Kwa hiyo, ukinunua lita tano za Motopoa wakati ungetumia nusu lita ya mafuta ya taa pengine hakuna tofauti yoyote. Kwa hiyo, si kweli kwamba kwa kutumia mafuta ya Motopoa tuta-*save* mazingira kwa sababu watu wengi wataenda kutumia Motopoa badala ya kukata kuni na mkaa, si kweli. Labda watoe maelezo mengine, lakini tusitumie kigezo cha kutumia Motopoa kama tuta-*save* mazingira, siyo kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani nishati mbadala ni Motopoa tu? Kwa nini limechukuliwa hilo na gesi, kwa nini hatukuangalia vitu vingine? Mimi ninakotoka Ludewa tuna makaa ya mawe na utaratibu wa kupunguza makali ya makaa ya mawe upo. Mkaa ule umekaa pale *idle.* Hata Mbinga kuna mkaa mwingi. Kwa nini hatutumii mkaa ule na teknolojia tunayo, tukatengeneza mkaa uwe na *calorific value* kidogo tukatumia badala ya kutumia kuni na mkaa? Kwa nini tumeng'ang'ania Motopoa? Nina wasiwasi labda hii ni kampuni ya mtu binafsi au tuna-*promote* biashara ya mtu binafsi hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani tumechambua kati ya *sources* nyingi tulizonazo, ni hii tu ndiyo tumeona tui-*recommend? Why only this one?* Wananchi wa kule vijijini kweli itafika hii Motopoa na mitungi ya gesi watanunua wapi na wabebe vipi wakati hakuna magari? Watakuwa wanabeba kichwani mtungi wa gesi kwenda kupikia nyumbani? *It is impossible!* Kwa hiyo, tunapoweka unafuu wa kodi kwenye Motopoa, haisaidii mazingira hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kidogo mambo ya Ludewa kabla sijakaa chini maana wapiga kura wangu hawatanielewa.

Kwanza, nimesoma kwamba katika mwaka 2008/2009, Serikali itaweka mkazo pamoja na mambo mengine kuhifadhi mazingira katika maeneo tengefu. Kando kando ya Ziwa Nyasa, ni eneo tengefu, tumevua samaki wamekwisha. Kwa hiyo, wananchi kule hawana kitoweo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti uliofanywa mwaka jana, unaonyesha katikati ya Ziwa kuna samaki. Tuka-*recommend* kwamba ili sasa kuwapata wale samaki, tutumie ndoana, lakini tunahitaji boti ya kwenda kule. Kwa hiyo, kulikuwa na utaratibu tuwape wananchi wale boti moja na *engine* kwa ajili ya kutoa mafunzo *on sustainable fishery*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliahidiwa boti na aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, alipokuwa Waziri wa Wizara hiyo kwamba tutapewa boti kwenye bajeti hii. Mimi nitapenda kujua wenzangu wanaohusika na uvuvi sasa hiyo boti iko wapi? Hela wamezipata au ilikuwa danganya toto?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kwenye suala la barabara, tumesikia kwenye matangazo huenda wakaanza kuzalisha *sponge iron* kule Liganga. Sasa hili ni suala la uchumi hapa nchini na wataendelea kufanya utaratibu wa kuzalisha chuma cha pua pale, lakini hakuna miundombinu. Hivi mitambo mizito itakayopelekwa kule ku-*blast* chuma kile na kwa ajili ya kujenga kiwanda, itapita kwenye tope! Wizara ya Miundombinu na Serikali, kwa nini hawaweki kipaumbele kwenye barabara angalau ya kutoka Mundindi pale Liganga kuja Mkiu na kwenda Njombe ili mali hizo zipitishwe kutoka itakapokuwa inazalishwa na vifaa vinavyotakiwa kwa ujenzi vipelekwe kule? Tunangoja mpaka mwekezaji aanze kazi, lakini hakuna barabara, biashara ya wapi hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho ni *trunk road* ya kutoka Njombe kupitia Itoni inaenda mpaka Manda, ni barabara kuu ya Kitaifa, barabara ile imesahauliwa kabisa. Lakini barabara nyingi zinajengwa katika Mikoa mingine, barabara ya kwenda Manda mnadharau sana kama kwamba watu wanaoishi Ludewa hawastahili *rrunk road?* Naomba barabara hii itengenezwe kwa sababu masika kule hatupiti. Naomba Mheshimiwa Waziri mnapopanga mipango yenu kwenye bajeti mkumbuke na watu wa Ludewa ni watu wa Tanzania hapa sio watu wa Malawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Professa Raphael Mwalyosi. Pamoja na mambo mengine amezungumzia habari ya kuperemba kwamba ni *monitoring*. Kwa Wagogo hapa Dodoma kuperemba ni kuwinda. Sasa sijui Mheshimiwa Waziri Seif Khatib labda akija kupata nafasi siku za mbele ya safari huko atatueleza kupelemba ni nini hasa.

Sasa namwita Mheshimiwa Dr. Festus Limbu atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassamy.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani nyingi sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kulihutubia Bunge lako Tukufu. Nianze mapema kabisa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu nifanye masahihisho kidogo ambayo yamekuwepo kwa muda mrefu sana. Kwenye kitabu cha orodha ya Wabunge, jimbo la Magu limekuwa likiitwa Jimbo la Magu Mjini. Magu Mjini ni Kata. Kwa hiyo, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Magu, sio Mbunge wa Jimbo la Magu Mjini. Magu Mjini ni Kata na kuna Diwani pale. Kama kuna maelezo mengine labda nitaomba nipewe kwa sababu kosa hili niliwahi kupeleka malalamiko kwamba hili libadilishwe lakini naona bado inakuja hivyo hivyo. Nashukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri na wasaidizi wake, Naibu Mawaziri pamoja na Katibu Mkuu pamoja na wataalamu wote kwa kazi nzuri walioifanya. Naungana na Wabunge wenzangu waliopongeza bajeti hii na mpango wa

maendeleo jinsi ulivyoandaliwa. Kwa kweli ukiusoma unasomeka vizuri, *logic* ina-*flow* vizuri na kwa kweli wamefanya kazi nzuri, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kumteua Profesa Benno Ndullu kuwa Gavana wa Benki Kuu. Professa Benno Ndullu namfahamu muda mrefu, uzalendo wake hautiliwi mashaka. Halafu katika Bara la Afrika katika Wachumi bora watano yeye anaweza akawa namba moja.

Kwa hiyo, nampongeza sana na namshukuru kwamba amekubali kuacha kazi nyingine alizokuwanazo na ambazo angeweza kuzipata, akakubali kuja kulitumikia Taifa lake. Alipochaguliwa kuwa Naibu Gavana, mimi niliwaambia marafiki zangu, *now here comes the Governor*. Nampongeza Rais na nakushukuru sana Professa kwa kukubali jukumu hilo. Naamini Benki Kuu iko kwenye mikono salama na *inshallah* timu yake ni nzuri, naiamini na naitumainia kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukipitisha sheria nyingi mbalimbali hapa Bungeni, lakini tunapopitisha sheria mbalimbali kama Wabunge na Rais kuridhia kwamba amekubali hiyo iwe sheria, kunakuwa hakuna uhakika kwamba sheria hiyo itatekelezwa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Rais akishaidhinisha, akishaweka sahihi kwamba imekuwa sheria, tunaomba Waziri wa Fedha asaini *certificate of financial implications.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila sheria ina *financial implications*. Hatuwezi kuwa tunapitisha sheria lakini fedha zake zinatengwa baada ya miaka mitano au sita, sheria inatungwa leo, lakini utekelezaji wake unafanyika baada ya miaka mitatu au minne kwa sababu hakuna fedha. Kwa hiyo, tunaomba Waziri wa Fedha itakapopitishwa sheria aji-*commit* kwa kusaini *certificate of financial implications* kwamba fedha zipo za kutekeleza sheria hiyo. Vinginevyo, sheria tutakazokuwa tunatunga zitakuwa zinalala kwenye ma-*shelf* na makabati bila ya kutekelezwa ambayo sio makusudi ya shughuli tunayofanya hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze mambo ya jumla yafuatayo: Kwanza, naomba ni-*declare interest* kwamba mimi ni Mwenyekiti wa Bodi ya Pamba Tanzania. Naomba niipongeze sana Serikali kwa kutenga ruzuku kwa mara ya kwanza katika pembejeo ya pamba kwa maana ya viuadudu. Katika bajeti tunayoimaliza, Serikali ilitenga Shilingi bilioni 1.47 kwa ajili ya viuadudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali, kwa kweli na wakulima wamenufaika sana na pamoja na sababu nyingine mwaka huu wamelima pamba sio kawaida. Pamba mwaka huu imeongezeka zaidi ya mara mbili ya ile waliyolima mwaka 2007. Kwa hiyo, naamini *multiplier effect* ya hii ruzuku itakwenda mpaka kwenye mambo mengine na itachangia kwa kiasi kikubwa katika kuwaletea wakulima wa pamba maisha bora. Ni matarajio yangu kwamba ruzuku hii itaongezwa mwaka huu ili wakulima wa pamba waweze kupunguziwa gharama na kuweza kulima kwa wingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri wa Madiwani. Mheshimiwa Blandes na Waheshimiwa Wabunge wengine wamesema Madiwani tuwaangalie, wanafanya kazi kubwa sana ya kusukuma maendeleo. Lakini wanatembea kwa mabasi, baiskeli au wanatembea kwa pikipiki za kuazima. Tunashindwa nini kuwaangalia hawa watendaji katika kuhamasisha maendeleo? *WEO* ana pikipiki, Katibu Tarafa ana pikipiki, Diwani inabidi aombe *lift* na ndiye mhamasishaji mkubwa wa maendeleo katika Kata. Naomba Madiwani wafikiriwe wapewe mikopo ya magari madogo kama Suzuki na ambayo yana msamaha wa kodi. Hapo natoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini katika Bunge lililopita alijibu swali langu kuhusu umeme wa kutoka Magu kwenda Mahaha. Wananchi wa jimbo langu, hasa wa eneo hilo, walifurahi kwa sababu hicho kitu hakijawahi kuwepo toka nchi iumbwe, na walisema kwamba kama umeme utapita kama Waziri alivyoahidi, basi CCM itaendelea kudumu. Mheshimiwa Ngeleja - Waziri wa Nishati na Madini, nakupongeza sana na kwenye jibu lile ulisema kwamba tayari tathmini ilishafanyika, ni shilingi bilioni 3.7. Mradi ule ulikuwa umetathminiwa gharama yake ni bilioni 3.7 naamini kwamba bajeti hii itatenga hizi fedha na utekelezaji wake utaanza na wananchi kwa kweli wameanza kusubiri umeme huu kwa hamu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye mfumo wa bajeti. Bajeti yetu ina vipengele vikubwa vitatu. Kuna mishahara kwa maana ya *PE* halafu kuna *OC* kwa maana ya *other charges* halafu kuna *development*. Napenda niipongeze Wizara ya Fedha, Serikali na tujipongeze wenyewe kwamba sasa tumepunguza utegemezi kutoka asilimia 42 mpaka 34. Huu ni ushindi mkubwa na ni lazima wote tuushangilie kwa sababu tunapunguza utegemezi. Maana yake sasa tunaweza tukalipia mishahara yetu, tunaweza tukalipia na matumizi mengine kwa maana ya *other charges* na kiasi kidogo kinakwenda kwenye maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo langu liko kwenye *OC,* kwenye mishahara sina matatizo. Ukiangalia *OC* vizuri kuna maeneo ambayo bado yangeweza kuboreshwa ama kupunguzwa ili fedha zile ziende kwenye maendeleo. Kwenye *OC* bado kuna mianya mingi ambapo fedha zinaweza zikapunguzwa zikaenda kwenye maendeleo.

Lakini pia kwenye maendeleo bado kuna matumizi ambayo yanaweza yakapangiliwa tena upya ili kuwe na *impact* ya kutosha katika kuleta maendeleo ya wananchi. Hizi trilioni 7.2 ambazo zimepangwa kama bajeti ya mwaka huu, zinaweza zikatupa *impact* zaidi kama tukipangilia *OC* yetu vizuri na *development.* Bajeti yetu ingepangiliwa vizuri. Kuna maeneo ambayo siwezi kuyataja hapa lakini ukipitia bajeti hii haraka haraka na kwa makini utaona ni maeneo gani yanaweza yakarekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha nyingi tunazotumia, karibu zote za ndani au asilimia kubwa tunatumia kwenye *recurrent expenditure*. Hii ni sawa sawa na kutumia fedha zetu nyingi kwenye *software* kuliko kwenye *hardware*. Tunatumia fedha zetu wenyewe kwenye *software* zaidi kuliko kwenye *hardware.* Kwenye *hardware* tunategemea wafadhili ndio watulipie. Hii ina hatari zake. Tungenunua pia *hardware.* Wanaofahamu kompyuta wanaelewa nina maana gani. *Software* tunazilundika, lakini

lazima uwe na kompyuta na kadhalika. Fedha zetu nyingi tunapeleka kwenye *software* Mheshimiwa Mwenyekiti na hii ni hatari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende sasa kwenye viashiria ama vigezo vya uchumi mpana kwa maana ya *macro-economic variables*. Kiashiria cha kwanza ni pato la Taifa, yaani *GDP*. Ukuaji wa *GDP* wa asilimia saba hautoshi. Nchi yetu ni tajiri, ina maliasili nyingi na sidhani kwamba asilimia saba zinatosha japokuwa tunasema asilimia nane na kuendelea hadi asilimia 10 ili tuweze kuondoa umaskini, asilimia saba hazitoshi. Nchi yetu ina utajiri mkubwa na *we are a sleeping giant* kwa kweli. Tanzania ni *sleeping giant,* hatujaweka mipango yetu sawa sawa kwa ajili ya kuamka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007 Pato la Taifa kwa kila Mtanzania ilikuwa ni Sh. 548,000/=. Tuko milioni 38, pato hilo ukiligawanya unapata laki tano kwa kila Mtanzania kwa mwaka. Lakini idadi ya watu ni kubwa sana, wengi wao wako *redundant.* Nchi zote zilizoendelea zimeendelea kwa kupunguza kasi ya ukuaji wa idadi ya watu.

Kwa mfano, China ilikuwa unazaa mtoto mmoja, basi. Sasa hivi ndio wanaongeza kidogo. Nchi ya Denmark *population* yake ni milioni 5.5. Milioni 5.5 nchi ya Denmark wakigawana Pato la Taifa kila mtu anakuwa tajiri na kazi zinawatosha. Sasa tuna changamoto, tusipoangalia kutekeleza sera ya idadi ya watu, ambao sikuona kwenye maelezo ya Waziri kwamba sera ya idadi ya watu inatekelezwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie sasa uchumi unakua wapi. Uchumi unakua kwenye maeneo ambayo sio waliko wananchi wengi masikini. Unakuwa zaidi kwenye madini ambako Watanzania wengi hawaguswi na kuwa zaidi kwenye umeme na gesi ambako Watanzania hawapo, inakuwa zaidi kwenye mawasiliano na labda kwenye mawasiliano kwa sababu hata kijijini kwangu wananipigia simu kwa hiyo imesaidia kidogo. Lakini hii *impact* ya ukuaji wa uchumi kwa mfano kwenye madini inatusaidiaje katika kurekebisha uchumi wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye kitabu cha Mpango wa Uchumi ambapo kumekuwa na *graph,* hata bidhaa tunazouza nchi za nje tunazozalisha hizi ambazo sio asilia kwa maana ya mazao, ukuaji wake unakwenda chini na haya mengine ambayo sio *traditional* ndiyo yanaongezeka ambapo watu wengi hawapo. Naomba tupange *priority* zetu vizuri na maeneo ambayo yanachangia kwenye uchumi kwa wingi, basi yaende kuchangia kwa maendeleo ya wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili ni mfumuko wa bei *(inflation).* Mfumuko wa bei maana yake ni kwamba una fedha nyingi kuliko bidhaa. Una fedha nyingi zinafukuza bidhaa chache na chanzo chake kinaweza kuwa cha ndani au nje.

Mfumuko wa bei unaweza ukapikwa ndani ya nchi ama unatoka nje. Kukabiliana na mfumuko wa bei unaweza ukafanya mambo mawili yafuatayo, ama yote mawili. Upunguze fedha kwenye mzunguko ama uongeze bidhaa na huduma, ama ufanye vyote viwili. Ili ushughulike na chanzo cha nje, inabidi upunguze ama uepukane na bidhaa

husika zinazoingia nchini, ama u-*caution* madhara yake. Kama mtu anaporuka *poll-vote* akianguka kwenye mchanga, zamani tulikuwa tunaanguka kwenye mchanga, lakini siku hizi unakuta kuna godoro la kunesa ili ukianguka usiumie. Kwa hiyo, mfumuko wa bei unaotoka nje, inabidi uwe *cautioned* ili kupunguza madhara kwenye uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari za *inflation* kwenye bajeti: Mwaka 2005 *inflation* ilikuwa asilimia tano, mwaka huu. *Inflation* ni asilimia 10. Hii bajeti ya trilioni 7.2 maana yake ni nini? Ni kwamba uwezo wake wa kununua umepungua kwa nusu japokuwa imeongezeka trillion saba ilikuwa trillion sita mwaka 2007 lakini *inflation* ime-*double*. Sementi mfuko mmoja mwaka 2005 ilikuwa unanunua kwa Sh. 10,000/= Magu. Sasa hivi ni Sh. 20,000/=. Bati lilikuwa linauzwa Sh. 7,500/=, sasa hivi ni Sh. 15,000/=.

**MWENYEKITI:** Dr. nakumbushwa hapa.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Nilikuwa naangalia saa Mheshimiwa, naomba dakika moja nimalizie kwa sababu…

**MWENYEKITI:** Ni kengele ya pili Mheshimiwa.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana kwa mchango wako Dr. Festus Limbu. Mheshimiwa Khadija Salum Ally-Qassamy, na ili nisiweke viporo atafuatiwa na Mussa Azan Zungu.

**MHE. KHADIJA SALUM ALLY-QASSAMY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia leo hii nikaweza kusimama mbele ya Bunge lako na Tukufu kuweza kuchangia hoja hii ya bajeti iliyokuwepo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, napenda kwanza ku-*declare interest* kwamb mimi ni mfanyabiashara, tena ni mdau katika mafuta. Mimi naona bajeti hii haijamsaidia mwananchi wa chini. Bajeti imemsaidia mwananchi wa kati na mwenye kipato cha juu. Kwa sababu Serikali imeondoa kodi ya mafuta ya moto poa, lami, gesi asilia, *pampers* na mengine mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza, kweli vitu hivi vitamsaidia mwananchi wa chini? Kutokana na hali za vijijini pengine hata haya mafuta poa, gesi asilia au *pampers* hawaijui. Ukiangalia katika majiko haya yanayotumia motopoa kwanza majiko yale ni madogo, hayawezi yakachukua familia za Kitanzania ambao ina watu wengi. Majiko yale yanatumia mafuta poa ambayo lita moja inauzwa Sh. 10,000/=. Sasa tujiulize kweli mwananchi wa kijijini ataweza kuyatumia mafuta hayo kwa lita moja Sh. 10,000/=?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda katika gesi asilia, Watanzania asilimia 80 ni masikini ambao nyumba zao ni nyasi na makuti, kweli gesi hii wataweza kuitumia? Mitungi ya gesi inauzwa sio chini ya laki moja na kuendelea. Kweli Mtanzania mwenye

hali ya chini ataweza kutumia gesi hiyo? Si tunajidanganya! Mtanzania kima chake cha chini kutumia ni dola moja. Sasa leo *pampers* moja inauzwa Sh. 300/= mpaka 400/= sasa kweli Mtanzania ataacha kuwatafutia watoto wake chakula aende akanunue *pampers*. Kwa hivyo, nahisi kuwa mambo haya bado hatujamsaidia Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani kwamba mafuta ya aina zote dizeli, petroli pamoja na mafuta ya taa yapunguzwe bei kutokana na hali halisi ilivyo. Mafuta ya taa yanatozwa kodi kwa lita Sh. 59.1, mafuta ya petroli yanatozwa Sh. 545/= kwa lita na mafuta ya dizeli yanatozwa Sh. 520/= kwa lita, kuna ubaya gani kupunguza Sh. 250/= ili tuweze kumsaidia mwananchi? Mimi ninavyohisi ni kwamba tunawapandisha *chart* wafanyabiashara kwa sababu mfanyabiashara unapompa sifa ukawa unasimama kila mtu anachangia kwamba duniani kote hali ni hii, kwa hiyo, kwa mfanyabiashara anapiga kigelegele kwa sababu atafanya vile anavyoona yeye kwake ni sawa. Serikali kwa sababu wanaona ni biashara huria na wao hawakulisemea jambo hili, basi mfanyabiashara ataona kwamba Serikali imeridhika, kwa hiyo, itakuwa inaendelea kufanya kila lile ambalo mfanyabiashara analiona kwake liko sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyochangia bajeti ya mwaka 2007/2008 tukasema kama mafuta yatakuja ku-*cost* Serikali na hivyo ndivyo ilivyotokea. Mafuta tangu mwaka 2007/2008 yamepanda kwa kasi kikubwa sana. Kutokana na hali hiyo, Serikali ikiendelea kunyamaza kimya mfanyabiashara yeye kazi yake anachotaka ni faida tu. Kwa hiyo, ataendelea kuweza kupandisha bei kwa sababu wafanyabiashara wengine hawana imani na wananchi wa Tanzania, wataendelea kupandisha kodi ili wananchi wa Tanzania washindwe hata kupata mlo mmoja kwa siku na hii itakuja kutu-*cost.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo, mimi naisihi Serikali kwamba bora kinga kuliko tiba. Tutakuja kuona hasara mbele yake kwa sababu kila mtu unapokuwa hukikemei kitu, maana yake unawaruhusu watu wafanye vile ambavyo wanaona kwao ni sawa. Kwa hiyo, naisihi Serikali kupunguza Sh. 250/= angalau ipatikane afueni katika kima hiki cha mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nachangia kuhusu biashara ya Zanzibar. Kama inavyojulikana na mara nyingi tunapiga makelele kuhusu bandari ya Zanzibar kwamba ni mbovu. Wafanyabiashara ni wengi na kuna meli kubwa sana haziwezi kusimama Zanzibar kutokana na bandari ni mbovu.

Kwa hiyo, mizigo mingi inashukia Dar es Salaam. Kutokana na mizigo, kwa mfano, magari yakishuka pale yanakuwa yameandikwa *transit* kwenda Zanzibar, cha kusikitisha nchi ni moja, Zanzibar ni Jamhuri ya Muungano, lakini magari yale yanaposimama pale kwa kusubiri kusafirishwa haijafika safari yake inalipishwa kodi na huku ukiritimba ule ule ukiendelea, peleka barua huku peleka barua kule mpaka uhakikishe mwezi au miezi miwili gari hata hujailipia ushuru unailipia kodi karibu Sh. 2,000,000/= au Sh. 3,000,000/=. Kwa kweli nahisi Serikali ya Muungano haiwatendei haki wafanyabiashara wa Zanzibar. Kwa hiyo, naomba kuiuliza Serikali, kwa nini tumefunga *ASCUDA++?* Kwa sababu tupunguze usumbufu, lakini bado usumbufu

unaendelea, wafanyabiashara wa Zanzibar wanaendelea kuteseka. Kwa hiyo, naiomba Serikali iendelee kuitazama hali hii kwa karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine linawahusu wafanyabiashara wanawake wa Tanzania Bara pamoja na wafanyabiashara wengine. Serikali mara nyingi inatakiwa iwaonee huruma wananchi wake na iwape *priority* ili wananchi waweze kujiondolea umasikini. Lakini naona Serikali inawapa *priority* sana wafanyabiashara kutoka nje.

Tuchukulie kama ndugu zetu Wachina, kwa Dar es Salaam wako wengi sana. Wao wanapewa *priority* kubwa! Mfanyabiashara tuseme kama mwanamke hana mtaji, anakwenda kukopa Benki Sh. 10,000,000.= ukii-*convert* katika dola unapata sio chini ya dola 8,000 na kidogo hiyo hiyo ununue tiketi, hiyo hiyo iwe ndio usafiri na ukifika pale huwezi kununua kitu kwenye kiwanda kwa sababu *quantity* yako ni ndogo.

Kwa hiyo, unanunua katika masoko ambayo wenzetu kule ndio wananunua raia wao. Ukifika hapa, Wachina ambao wamepewa fursa, unakuja wewe kulingana nao kiasi kwamba biashara ile ile wao wanaiuza kwa bei ya chini. Mwananchi wa Tanzania unakuwa hujamsaidia.

Kwa hiyo, ina maana umasikini unaongezeka, fedha anashindwa kuzilipa inabakia mwananchi kujiingiza katika mambo yasiyokuwa na maana na Taifa letu kuzidi kuongezeka umasikini wakati wenzetu kutoka nchi za nje wanakuwa matajiri. Kwa hiyo, naiomba Serikali, wenzetu wa nje wanakuwa raia wao ndio wanawapa leseni, mtu yoyote akija, yeye anafanya kazi kwa mujibu wa leseni ya yule raia wa nchi ile.

Kwa hiyo, tunaomba na sisi tuangalie tena sheria zetu pamoja na utandawazi, lakini tuhakikishe kwamba katika biashara tunawapa *priority* wananchi wetu ili na wao waondokane na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni kero sana hasa kwa bandari yetu ya Dar es Salaam. Bandari ya Dar es Salaam ina *priority* kubwa kutokana na kwamba tumezungukwa na nchi ambazo hazina bahari. Kwa hiyo, watu wengi wanakuja kufanya biashara na sisi. Lakini cha kusikitisha, mazingira ya pale ni mabaya, usumbufu ni mkubwa hata wafanyabiashara wa kawaida wa Dar es Salaam, mizigo inachukua sio chini ya miezi miwili haijatoka. Halafu tunapiga kelele kusema kama kuna mkanganyiko wa makontena, wakati sisi wenyewe ndio tunasababisha kutokana na usumbufu, mzunguko, ukiritimba na kuchelewesha kutoa mizigo bandarini.

Kwa hiyo, kutokana na hali hiyo, naiomba Serikali iangalie kwa kina, upatikane angalau wepesi mizigo ipate kutoka haraka haraka na ile bandari iwe na nafasi angalau mpaka tujipange katika kufanya miundombinu ambayo itaweza kusiaidia Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, naiomba Serikali ya Muungano iangalie sana katika suala la Tume ya Pamoja ya Zanzibar ambayo ile Tume ya Fedha, tangu Agosti, 2006 mpaka leo tunaambiwa mazungumzo bado yanaendelea.

Sisi tunaamini kwamba kima hicho kama watu wangekaa wakapanga vizuri, basi ingeisaidia Zanzibar. Zanzibar imezidi kuwa maskini hata pale *Airport,* ni aibu. Ukienda pale *Airport* barabara yake ni aibu kubwa, yaani pale wanakuja watalii wengi. Kwa kweli ni jambo la aibu na la kusikitisha. Naamini kama kweli Serikali ya Muungano ina nia njema na Zanzibar, basi isaidie katika mambo ya kupatikana hizo fedha ili tuhakikishe na sisi angalau ile nchi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa hayo sina zaidi. Ahsante, nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. MUSA ZUNGU AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza na mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo ambalo Serikali limeamua kufanya katika kipindi hiki cha Bajeti ni kuanzisha Tume ya Mipango. Tume hii ya mipango kwa nchi nyingine inaitwa *National Strategic Centres*, ambayo ndiyo inayopanga vipaumbele vya matakwa na mahitaji ya nchi. Ndicho chombo ambacho kinapanga sera na ndicho kinafuatwa na kinaongoza hizi Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi kila Wizara inaogelea kivyake. Kila Waziri anayewekwa katika Wizara fulani mara nyingi huwa anakuja na ya kwake, hakuna kitu ambacho kinamwongoza. Kuna Waziri mmoja alikuja hapa alivuruvuruga masuala ya elimu na akatoatoa mambo mengi tu. Kaondoka yeye, kaingia Waziri mwingine akarudisha yale mambo yaliyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya yanatokana na sababu ile *National Strategic Centre* ambayo ni Tume ambayo inatakiwa itoe mwelekezo na dira, inakuwa haipo au ikiwepo inakuwa haina nguvu. Kwa hiyo, naipongeza Serikali, lakini pia naipongeza Tume ya Mipango. Ingepata jina lingine kubwa kabisa, kufanya jina hili liwe ndiyo dira na ndiyo ambayo itakuwa inatoa maelekezo Hazina. Sasa hivi vipaumbele vinatolewa Hazina. Bajeti nyingi za Wizara zinakatwa na utakuta watu wa Hazina ndiyo wanaopanga vipaumbele na *interest* za kitaifa. Kwa hiyo, nafikiri kwamba Tume hii sasa iwe na uwezo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tuna wawekezaji wanakuja. Hii Tume ndiyo inatakiwa ipange sera na maslahi ya wafanyakazi watakao ajira na wawekezaji kutoka nje mwanzo kabisa wanapokuja. Kwa mfano, mimi sioni sababu kwanini sasa hivi tusiweke kima cha chini cha mshahara kuwaeleza wawekezaji kabla hatujafika hapa, unapokuja Tanzania kima cha chini ni Dola 300. Inakuwepo katika sera na inakuwepo katika dira ya kitaifa. Kwa hiyo, unaweza kuwalipa Dola 300, karibu! Huwezi, rudi kwenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume hii nayo vilevile lazima iwe na kitengo cha sayansi na teknolojia. Lazima Tume hii au *centre* hii ya *strategy* iwe na dira na namna gani nchi yetu itakuwa kwa miaka 20 inayokuja kwa masuala ya nishati. Lazima tuwe na chombo ambacho chombo hiki kitakuwa na mwongozo wa kuzishauri Wizara ni namna

gani tutatumia nishati zetu kwa miaka 20 inayokuja, ni namna gani tutakuwa na idadi ya watu gani baada ya miaka 20 kuanzia sasa hivi. Kwa hiyo, Tume hii inatakiwa iwe na mipango hiyo ya kuiwekea dira Serikali na kuweza kukabili hali halisi itakavyokuwa baada ya miaka 20 kuanzia sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia sana Tume kwa sababu ndiyo ninavyoiona, mimi ndicho kitakachokuwa chombo cha kutuokoa na chombo cha kutuongoza. Sera zetu nyingi sana zimeshapitwa na wakati. Kwa hiyo, chombo hiki sasa kifanye kazi za ku-*revisit* sera hizi na kutoa mtizamo mpya ili taifa letu liweze kwenda mbele. Tumezungumzia hapa kuhusu wakulima wa jatrofa. Lakini kwa vile hatuna chombo ambacho kinatoa mwongozo wa maslahi ya kitaifa, hizi jetrofa zitalimwa hapa na zitachukuliwa kwenda kuwa *processed* katika nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuwe na mpango wa kuyalazimisha makampuni haya ambayo yakilima mazao haya, mitambo yake na viwanda vyake viwekezwe hapa nchini ili tuweze kuongeza ajira za Watanzania. Sasa haya yatapatikana kwenye *National Strategic Centre,* chombo ambacho kinatoa vipaumbele na kinasimamia maslahi ya taifa. Sasa hivi ukienda kwenye kila Wizara, kila mtu anaibuka na lake. Sasa hujui kila mtu akiiibuka na lake ana mtizamo gani na maslahi ya kitaifa. Lakini chombo kama hiki kitakuwa sasa kabla hata hawa Makatibu Wakuu, Mawaziri Viongozi wa juu wanapigwa msasa kwenye chombo hiki kwanza halafu ndiyo wanapelekwa wakahudumiwe wananchi wa taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye taarifa ya Bajeti ya mwaka huu halikuzungumziwa suala la ku-*export* gesi ambayo tunayo. Nimejaribu kuliulizia nikaambiwa ushauri uliotolewa ni kwa gesi yetu sasa hivi itumike kwa kutengeneza mbolea na itumike kwa manufaa ya hapa nchini. Lakini tungepata majibu *deposit* ya gesi ambayo tunayo sasa hivi ni ngapi?

Gesi hii kama tukiamua ku-*export* itatupatia mapato shilingi ngapi kwa taifa na itachukua muda gani gesi hii kwisha? Sasa chombo hiki ndicho kinachotakiwa kitoe majibu haya. Wakati mwingine tukichelewa kuanza kuzalisha gesi hii na dunia inavyobadilika kisayansi na kiteknolojia, kuna hatari baada ya miaka 20 ijayo gesi hii ikawa haina faida tena katika soko la dunia. Kuna *eco-solutions*, kuna watu sasa hivi wanafanya tafiti mbalimbali kuondokana na nishati hii ya petroli na gesi.

Kwa hiyo, nafikiri kuna umuhimu Serikali itupe majibu kwa *deposit* za gesi ambazo tunazo nchini na manufaa ya gesi hii ambayo tutakuwanayo wakati tutakapoanza ku-*export*. Kuna nchi zinauza gesi na wala hawana mafuta. Hebu tuambiwe mipango ya sasa hivi ya Serikali ya namna gani ya kuweza ku-*distribute* gesi ndani ya nchi na nje ya nchi. Mikakati ya Serikali ya siku za mbele ya kuweza ku-*supply* gesi kwenye nchi za jirani ili tuweze kupata mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi zinatuonea wivu kwa hizi maliasili tulizonazo. Wasiwasi wangu mimi na *partners,* sio wote ambao wanataka kutuona tunajitegemea. Inawezekana ushauri mwingine wa sisi kutokuuza gesi hii unatolewa kwa

sababu bado wanataka kutukandamiza na bado wanataka kutuweka chini ya miguu yao. Kwa hiyo, chombo kama hiki cha *National Strategic Centre* ndicho kinafanya utafiti na kuishauri Serikali vipaumbele vya namna gani vya ku-*export* gesi, kwanini tu-*export*? Inawezekana labda *deposits* zetu sio nyingi kama hatuwezi kuuza gesi nje. Lakini kama kuna utafiti wa kuonyesha *deposit* zetu zina *cubic* fulani za ujazo na zinaturuhusu ku-*export* tuanze mikakati ya kuuza gesi nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni maamuzi. Mimi nashukuru namjua Mheshimiwa Pinda kwamba ni mtu wa kazi. Tuwe sasa na maamuzi ya kugharamia miradi yetu. Hivi tukisema Bajeti hii tunatoa trilioni moja tunaipeleka kuzalisha gesi na kuiuza nje, faida gani tutakayoipata katika kipindi cha miezi tisa? Kwa hiyo, tuwe na utamaduni wa kukubali miradi yetu. Tunapoteza mapato mengi sana kwenye madini kwa sababu sisi tunachangia mgodi na ardhi hatuchangii pesa. Lakini tukiwa na utamaduni wa kugharamia migodi hii, kuchangia migodi hii na hawa *partiners* mapato ya Serikali yatakwenda juu kiasi cha kuweza kuchangia pato letu la taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna mipango mingi tu ya viwanja. Dar es Salaam kama itakuwa na *planning* nzuri, hatuna haja ya kuupanua mji wa Dar es Salaam na kuweka viwanja vingi nje ya Dar es Salaam na kuwafanya watu wa Dar es Salaam wakashindwa kulima hata mihogo sasa hivi. Tunatakiwa tuwe na *strategies* za mji wa Dar es Salaam. Mji wa Dar es Salaam haujajaa, Magomeni, Ilala, Gerezani, Kuna mpango wa Serikali wa kushiriki na wananchi wenyewe wakachangia maeneo yao tukajenga maghorofa ambayo yatamsaidia mwenye nyumba kupata *flat* zake tatu na huyo mwekezaji akaweza na yeye kufanya biashara katika maeneo hayo, hatutakwenda Bunju tena. Kwa hiyo, naomba kupendekeza hilo suala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni *National House.* Kuna mpango katika Mkoa wa Dar es Salaam sasa hivi ambao siku zote naupigania. Mimi sipingani na *NHC* kujenga majengo mapya katika mji wa Dar es Salaam na hasa katikati ya Mji. Malengo ya *NHC* ilikuwa ni kuwakomboa Watanzania wanyonge kuweza kuishi katika makazi bora na salama na yenye ustaarabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoanza kuingia ubia kwa mpangaji aliyekaa miaka 40 au 35, unamdanganya kuwa ndiye mtu wa kwanza kumpa nafasi ya kujenga na hawezi, maana kuna watu wamezaliwa kupanga na wengine kujenga. Lakini wengi tumezaliwa kupanga. Hata mimi napanga mpaka leo. Unapomwambia mpangaji baada ya miaka 35 funga virago ondoka unaleta tabaka za matajiri katikati ya Mji. Ushauri wangu kwa *NHC* ni kwamba, jengeni nyumba, ingieni mkataba na wabia lakini katika Mkataba mnaweka *provision* ya hizi ghorofa tatu, hawa wanyonge tunawarudisha kwa kodi yao ile ile. Kitu gani kinashindikana? Lakini kila mikataba, mikono yetu iko nyuma; *yes, yes*! Kila kitu tunawakubalia tu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine utakuta hizi nyumba sasa tunazirudisha kwa milango ya nyuma kwa matajiri wale wale tuliowanyang'anya. Utakuta mstaafu ameshaitumikia Serikali miaka 35 ana kijumba chake pale cha *National Housing*, pensheni yake ni ndogo, amelipa kodi miaka 35, kwanini nyumba hizi wasipewe? Hata

kama utasema hatuwapi tena, sababu wameshazigharamia, tuseme tunawauzia kwa bei ndogo na kuzimilikisha. Tunawasahau!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu ameshatumikia Serikali miaka 40, badala yake anashindwa kulipa kodi ya miezi mitatu, anafunga virago anatupwa nje. Je, tuulize *NHC* ki-*apartment* kile kodi waliokusanya haiwezi ikajenga hata nyumba tatu kama zile. Hata nchi za kibepari wana *system* ya *mortgage*. Unalipa kodi miaka 10 au 15 baada ta hapo allah wa saala nyumba hii ni ya kwako unakaa wewe na watoto wako. Mimi naomba tungepata jibu kwa hili. Kuzikarabati wanashindwa, maji machafu ndiyo mtindo mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye barabara ya Uhuru. Barabara hii, lile eneo lililotengenezwa linaitwa la *Bush*, lile eneo baya ni la Zungu. Masikini ya Mungu mimi jamani! Tena nimeshaiomba huu mwaka mzima hii barabara kwamba ichukueni. Hata kujibiwa sijibiwi jamani! Niambieni, Zungu, haiwezekani bwana, kaeni na barabara yenu. Jibu tu, huu ni mwaka mzima tangu mwaka 2007 mpaka mwaka huu naililia barabara ya Uhuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu unapita siku zote, hata wewe mwenyewe huoni Mheshimiwa *PM*? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vyanzo vyetu vya mapato, tumeambiwa tusikusanye tutapewa ruzuku. Sisi tulikuwa tunakusanya zaidi ya bilioni tatu kwa mwaka kwenye leseni, tumenyang'anywa. Sasa na ruzuku inakuja imepungua. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nakuomba uichukue hii, kesho unipe majibu. Mwaka 2005/2006 zilikuja sahihi, 2007 zilikuja kidogo ilipungua, 2007/2008 makisio tumepewa Sh. 1,700,000,000/= badala ya Shilingi bilioni 2.7. Bilioni moja imeingia mitini, imekwenda wapi? Mwaka 2008/2009 shilingi bilioni 1.5 imeshuka kutoka kwenye shilingi bilioni 2.7 mpaka shilingi bilioni 1.5, tutaendelea vipi na watu wetu kwa hali kama hii? Tunaomba na Mheshimiwa Waziri Mkuu mturudishie kwa Dar es Salaam vyanzo hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Zungu. Kama nilivyosema mwanzo, sasa namwita *Senate* Paul Kimiti na jirani yake Hamza Mwenegoha ajiandae.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi ili na mimi nichangie kidogo kuhusiana na Bajeti hii. Waheshimiwa Wabunge msishangae tunapoitwa Maseneta, sisi ndiyo wazee tuliobaki ndani ya Bunge hili. Nimekuwa Mbunge tangu mwaka 1980 na nipo hapa na bado ninadunda, nitawashinda watakaokuja wengine huku. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie Bajeti ambayo naiunga mkono vizuri, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na watumishi wote ambao wameisaidia kuandaa Bajeti hii. Lakini pia nimpongeze Ndugu Kitilya wa *TRA* kwa kazi nzuri kweli anayoifanya na pia nimpongeze Ndugu Ludovick Uttoh - *CAG* wetu kwa kazi nzuri anayolinda kwa kidogo tunachokipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote mnakumbuka juu ya Ma-*auditor* wa zamani. Ukisikia *Auditor* anakuja utajificha. Nilikuwa na mwenzangu anaitwa Ndugu Sanga wakati nafundisha Ukiliguru na yeye alikuwa anafundisha Tengeru. Tumetoka Marekani, tulipofika tu Dar es Salaam tukaambiwa *Auditor* anamtafuta huyo kijana anaitwa Sanga. Alikuwa ni Mwalimu anakusanya fedha za maziwa pale shuleni na kumbe alikuwa ametumia fedha hizo. Alipofika Tengeru hakuwa na uwezo wa kurudisha fedha hizo, aliposikia *Auditor* amefika, alikwenda akajinyonga. Alijinyonga kwa sababu *Auditor* wa wakati huo alikuwa hana utani. Ukisikia *Auditor* anakuja ni kweli *Auditor*. *Auditor* wa siku hizi unamwandalia hata mahali pa kulala, atafanya kazi kweli iliyokusudiwa kufanywa? Hawezi! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba *CAG* afanye angalau *a crush programme* tupate Ma-*auditors* wa kutusaidia. Hiki kidogo tunachopata kilindwe ili kisaidie maendeleo ya Watanzania. Nataka niipongeze Serikali kwa dhati kabisa ya kwamba safari hii kwa kweli wamejitahidi. Bajeti imekuja nzuri na imeanza kujibu Ilani yetu ya Uchaguzi.

Ilani ya Uchaguzi ina maeneo mengi, ukitaka kujua Bajeti inajibu, nenda kwenye Bajeti, angalia maagizo tuliyoyatoa, kitu gani bado na kwa sababu zipi? Mimi nitatoa mfano. Nimefuatilia suala zima la barabara nikakuta kwa bahati nzuri mwaka huu *MCC* wanaingia. Inaonekana katika Ilani, asilimia 80 ya barabara zilizotajwa katika Ilani zitatekelezwa. Mungu akupe nini? Huo ni mwanzo mzuri. Lakini bado naogopa kwa sababu kama sio *MCC* na sisi tunaogopa kukopa, hizi barabara zisingejengwa hata kidogo. Ndiyo maana nataka niungane na wenzangu, Mheshimiwa Kaboyonga, amezungumzia sana kwa nguvu ya kwamba tusiogope kukopa kwa maendeleo ya nchi yetu. Kama tunataka maendeleo, tusiogope, tukope tu! Lakini tuogope kukopa kwa fedha ambazo zinatumika vibaya. Hiyo kabisa nitaipinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia Bajeti ya Mwaka huu, nikakuta barabara ya Tunduma -Sumbawanga imepewa shilingi bilioni 10, za *MCC* na bilioni mbili ni fedha zetu wenyewe. Nikasema ni mwanzo mzuri na nasema Mheshimiwa Waziri Mkuu umeanza vizuri kwa sababu kero kubwa ya Rukwa kuacha yote, ni barabara na viongozi wanapokwenda Mkoani afadhali uzungumzie mengine. Ukikosa kuzungumzia kama umeandaa nini kwa barabara, utapata shida sana. Kwa hiyo, huu ni mwanzo, lakini nadhani tutaelezana zitatumika kwa utaratibu upi. Hiyo ndiyo kazi mojawapo kwa sababu ajenda yetu kubwa ndiyo hiyo ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nataka niwakumbushe, mwaka 1937 wakati wa enzi za ukoloni nilisoma kwenye *Hansard* ya *Legislative Council* (Baraza la Kutunga Sheria) wakati huo ambalo zaidi lilikuwa linaongozwa na *Governor*. Waliiombea barabara ya kutoka Mbeya mpaka Rungwe Tukuyu 7,000 *Pounds* itengenezwe kwa lami. Walitoa sababu gani?

Walisema kwamba lazima tuimarishe barabara hiyo kwa sababu ndiyo uzalishaji wa chakula utoke huko kiende Chunya. Hayo ni maelezo waliyoyatoa. Chunya ndiyo ilikuwa sehemu ya migodi mikubwa *Lupa mine*, Saza *Mine* na Makongorosi.

Makongorosi *actually* ni jina la kiingereza ilikuwa *Mine which was making loss* wakaiita Makongorosi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, limeshakuwa jina na limeshajulikana na watu wamelizoea, lakini ilikuwa ni *mine* ambayo ilikuwa inafanya hasara sana. *It was making loss*! Makongorosi mpaka leo inaendelea hivyo. Sasa kwanini waliamua? Waliamua kwa sababu wale wachimbaji wa madini walitegemea wapate chakula na kwa sababu barabara kutoka Mbeya mpaka Tukuyu wakati huo kwa Profesa Mwandosya mnafahamu ilikuwa ni mbaya kwa ajili ya mvua zinazonyesha kila wakati. Wakasema iwekwe lami. Wali-*value* chakula, wakaagiza 7,000 *Pounds* zianze kutengwa iwekwe lami. Kati ya barabara za kwanza kuwa na lami ni pamoja na hiyo. Walikuwa na sababu. Leo miaka arobaini na ngapi ya uhuru tunashindwa hata kilomita moja ya kwenda Sumbawanga. Tumekosa nini tena kwenye chakula ambapo tungeweza kulisha nchi hii! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema kwa uchungu kwa sababu tumechoka. *We are tired! It is now too much!* Hatutaki tena kuzungumza, tunataka matendo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niingie kwenye kilimo. Mwaka 2007 nakumbuka na wewe utakumbuka, nilisema kwa uchungu kwamba wakati mwingine sijui hawa watu wanaoagiza mbolea wanatoka wapi? Kwanini tunakubali watupe bei zao ambazo sio za kweli na tunaingia gharama kubwa sana kuongeza ruzuku na wakati bila hata ruzuku tungeweza kupata mbolea kwa bei ya chini? Nikatoa mfano ya kwamba mimi mwenyewe nilitaka niwe naagiza mbolea, lakini nikaambiwa hukopesheki. *You are not credit wealth* Kimiti. Pamoja na mbwembwe zangu mimi Kimiti kweli nimekuwa kiongozi miaka yote hii sikopesheki, nitatoroka nitakwenda wapi? Nikakwama.

Mwaka huu nimeanza, tena kwa taarifa yenu nilikuwa nimepata kampuni mmoja kutoka Marekani inaagiza mbolea kutoka Ukraine. Walinitumia *order* na ni mwezi Aprili walisema tutaleta mbolea ya *urea* kwa dola 350 kwa tani *C.I.F.* Dar es Salaam. *Carriage Insurance and Freight* Dar es Salaam na *payable* pale, mradi tufungue *L.C.* ikifika tunamlipa ili isiwe ya kitapeli. Ukifanya hesabu zako ni karibu Sh.19,000/= au Sh. 20,000/- kwa mfuko mmoja. Tumezubaa, tumechelewa, miezi miwili baadaye imefika dola 900 mpaka 1000. Kila unapochelewa mambo yanabadilika. Ninataka niiombe Serikali tuwe *very fast* katika *action* zetu tusiwe tunachelewa, *speed* iongezeke tufanye kazi kama tupo kwenye vita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mmoja niliwahi kukumbuka kwamba tulipokuwa na Kamati ya kusimamia maendeleo kivita ilikuwa inaitwa KAMKUKI wote mnakumbuka. Kwa sababu hali ya uchumi sio nzuri, hali ya chakula sio nzuri hatuwezi kuendelea, tukachukua mambo yetu kama siku zote, hapana! Ni kosa kubwa! Lazima tubadilike katika utendaji wetu wa kazi.

Ndiyo maana nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, kiongozi wetu wa Serikali maamuzi mengine tuwe tunachukua haraka tusichelewe. Kipindi hiki sio kizuri, kila hatua unayochukua lazima uende *fast,* la sivyo, tutakwama. Mimi ni Mtaalam wa

Kilimo ni *Agricultural Economist* na nina wanafunzi wangu wapo hapa. Mheshimiwa Dr. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, yule Mheshimiwa Martha Umbullah wote wanafunzi wangu. Nilikuwa nawafundisha *Agricultural Economics*. Hao nimewateua kwa sababu walikuwa katika Chuo Maalum wanachukua *Diploma in Homes Economics* na kule wanaume hawapo. Tumeelewana? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani sasa masuala ya ambayo lazima tuyaangalie hivi sasa ni kuangalia nini tufanye ili tuondokane na baadhi ya matatizo tuliyokuwa nayo. La kwanza, nakubaliana na wenzangu walivyozungumza ya kwamba lazima wigo wa kodi tuuongeze. Tusitegemee hawa hawa wa kila siku, lazima tuongeze wigo wa kodi na hiyo inawezekana. Mambo ya kupunguza kodi, mambo ya ushuru kwa ajili ya mazao mbalimbali kwa ajili ya shunguli za kilimo, hiyo naungana na wenzangu kwamba hatuna ujanja. Lakini kuna mengine ningeomba kabisa, hivi kweli Serikali inashindwa kutoa shilingi bilioni tano kutengeneza ndege zetu za Serikali? Mnataka viongozi wetu wapate ajali? Wameomba bilioni tano lakini hata senti tano haikutolewa. Tupate maelezo, kwanini tunakataa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Shirika la Ndege la Tanzania linadaiwa na lina madeni karibuni bilioni nne tulipokuwa na wenzetu wa Afrika Kusini. Mnataka kweli ndege zetu zikienda *South Africa* zishikwe huko? Zikikamatwa, hatuna ujanja, mtalipa tu! Afadhali tukubali tulipe mapema. Tumezungumza juu ya Uwanja wa Ndege, tunataka kuupanua, wako watu wa Tabata pale miaka mingapi wanasema wanataka shilingi bilioni 28. Kama hatuna, kwanini tusiamue basi kujenga viwanja vingine kama ni Bagamoyo au Mkurunga au wapi? Mimi nadhani vitu vingine ni vizuri, vitu vingine vikawekewa mkakati kwa sababu mimi naogopa tunaweza tukafikia mahali fulani tukashindwa kutekeleza baadhi ya haya ambayo tulikuwa tumejipangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni hali ya chakula hapa nchini. Hali ya chakula hapa nchini ni mbaya. Nimeangalia katika mahesabu yetu, zimetengwa shilingi bilioni 15 kwa ajili ya kuimarisha *SGR*. Waheshimiwa Wabunge, shilingi bilioni 15 inaweza tu kununua tani 50,000 mpaka 60,000 na hicho chakula ni cha mwezi mmoja kwa kina Azzan Zungu pale Dar es Salaam. Mwezi mmoja tu, kwanza sio ajabu hakitoshi. Mwaka huu tumesema hatutaruhusu watu wauze chakula nje, unataka Mfipa au mtu anayetoka Ludewa anatoka Makete au Njombe apeleke wapi mahindi yake kama *SGR* haiwezi kununua? Ama sivyo tunataka walanguzi ndiyo waendelee kuwanyonya wakulima wetu wawape bei ndogo kwa sababu hawana njia yoyote?

Tunaiomba Serikali ihakikishe safari hii wanajitahidi ili angalau watoe fedha kwa ajili ya kununua mahindi tena mapema iwezekanavyo. Itakuwa ndiyo ukombozi, watapata fedha kwa ajili ya maandalizi ya pembejeo ambayo tunasema safari hii bei itakuwa ni kubwa sana. Sasa usipowawezesha utapata matatizo makubwa sana. Lazima tuwasaidie, ni kazi mojawapo. Tunataka kuhifadhi chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa yako, Mjini Sumbawanga kuna tani karibu 19,000 hatujaziondoa hata kidogo na msimu umeanza. Tutaweka wapi mahindi ya mwaka huu? Naomba utaratibu uandaliwe kwa wote wanaohusika angalau kianze kutoka

au mkubali kitakachokuwa kinanunuliwa kinapelekwa moja kwa moja sehemu mbalimbali zinazotakiwa. Tuwe na *enough stock* ndani ya nchi! Hilo nadhani nataka niwaombeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni kuhusu shule zetu za Sekondari. Shule za Sekondari mimi nimezunguka katika shule zangu zote za Sumbawanga pale Mjini. Wanafunzi wananiuliza hivi, kweli mnasema ulimwengu wa sayansi na teknolojia, shule zote hata maabara hakuna! Mnatupeleka wapi wazee? Wanafunzi wananiuliza, utaratibu ambao nimeutengeneza baada ya kuzungumza nao nasema ulizeni chochote, wote wanaulizia hilo hilo. Mimi nikawaambia tupo katika mkakati wa kuanza kujenga maabara na nina imani kabisa safari hii kama kweli tunataka tuingie katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia lazima tuanze kuwajenga vijana wetu hatua kwa hatua katika shule zetu za sekondari maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, yako mengi tungeweza kuzungumza, tuna nafasi kubwa ya kuzungumza kwenye Wizara nyingine, lakini kwa ufupi ninaiunga mkono hoja hii kwamba ni nzuri, mradi tuisimamie vizuri iweze kufanya jukumu lake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana *Senetor* Paul Kimiti. Kama nilivyosema mwanzo, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamza Mwenegoha na Mheshimiwa Fuya Kimbita ajiandae.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. Kwanza, nitangaze *interest*; mimi ninahusika kabisa na hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi ya Mheshimiwa Dr. Kigoda kwa sababu mimi ni Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Kwa hiyo, yote aliyosema yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachangia sasa hivi kwa sababu yale ambayo ningeweza kuchangia hasa kuhusu Jimbo langu, nisingeweza kuyachangia kwenye hotuba hii. Kwa mantiki hiyo, nitaanza katika mchango wangu kwanza, kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu Waziri wote wawili, Katibu Mkuu na Manaibu Katibu Wakuu wote watatu na wadau wote hasa *TRA* na hapa kwenye *TRA*, lazima niseme ukweli, nampongeza rasmi kabisa Dr. Kijoriga ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya *TRA*, mama shupavu kabisa na hodari huyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na mazungumzo kuhusu mambo ya Jimbo langu, halafu yatakayobakia, muda kama ninao, nitagusa mengine. Naomba nianze na Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetangaza kujenga Bwawa la Kidunda ambalo lingesaidia kupeleka maji Dar es salaam. Bwawa hili liko kwenye Mto Ruvu na linajengwa kwenye Jimbo langu na linajengwa kwenye Kata ambayo mimi ninaishi. Kata nzima ya Selembala ilitegemea kuhamishwa pamoja na Mbunge wao ili Dar es salaam wapate maji. Hatuna matatizo kabisa kwa suala hilo. Tunaheshimu maamuzi ya Serikali

na tumeyakubali. Sasa linalofuata, wamekuja wataalam wa kuangalia mazingira yatakavyoharibika, wamepita. Wakaja tena wengine, nao wanaitwa wanaangalia mazingira. Hawa wameharibu kazi! Hawa ndio wamekwenda wanaweka alama kwenye nyumba na kusema nyumba hii inahama, nyumba hii inahama, nyumba hii inahama. Wananchi wa Kata hii wamesimamishiwa maendeleo wasijenge, wasilime kwa sababu Serikali itawahamisha na tulikuwa na matumaini tunahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunataka tujue ukubwa wa Bwawa na jinsi litakavyorudi nyuma, hakuna anayetupa jibu. Tulikuwa tunataka tujue tunahamia wapi? Kijiji cha Kiburumo kilipata msaada wa *TASAF* kujenga zahanati, Halmashauri. Kwa busara kabisa, walisimamisha malipo ya mwisho ya zahanati kwa sababu wanasema zahanati itahama. Sasa ina maana gani kuleta malipo ya mwisho na kumalizia zahanati hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia kwenye *MCC*, hamna kitu. Naomba Serikali mtupe jibu, tuendelee kufanya shughuli za maendeleo au tuendelee kudumaa kama Kata? Maana hatujui nini la kufanya! Je, Serikali itajenga Bwawa lile katika muda wa miaka miwili/mitatu ijayo ama hapana? Kwa sababu wananchi hawa lazima wapate jibu. Hapa ninamwomba Mheshimiwa Waziri ama Naibu Waziri katika kipindi hiki cha bajeti tuandamane yeye na mimi, twende wakatoe jibu! Wananchi hawa wawe katika hali ya uelewa, wajue nini cha kufanya kuhusu Bwawa la Kidunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nigusie sekta ya nishati na madini. Naomba safari hii nianze na shukrani kwamba Serikali imejitahidi sasa kuanza kuelekea kutuletea umeme kutoka Morogoro mpaka kwenye kitongoji cha Kangazi ambacho kiko kwenye Kata ya Kisemu, kwenye Tarafa ya Matombo. Tunashukuru kweli kweli! Lakini, tunasema, hapo ulipomalizia, Wilaya ya Morogoro Vijijini inahamia kwenye Tarafa ya Mvuha. Kata ya Mvuha ni kilomita 16. Tunaomba basi angalau msogeze umeme hapo penye Makao Makuu ya Wilaya. Tunategemea ukifika hapo, utakwenda vile vile Dutumi, Mngazi na Kisaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetaja Kisaki makusudi, kwa sababu wakati wa Kampeni za Mheshimiwa Rais za kugombea Urais katika Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete alifika Kisaki Stesheni na aliahidi kwamba atajitahidi kwa uwezo wake wote ile jenereta kubwa sana ambayo iko pale Kisaki Stesheni iweze kusaidia kugawa umeme kwa wananchi kwa malipo. Viongozi wa *TAZARA* waliposikia hili, wameondoa ile jenereta kubwa, wameleta jenereta ndogo. Huku ni kuhujumu.

Mimi nasema hii ni hujuma ya makusudi ya uongozi. Sasa watu hawa wananiuliza, katika utendaji wa namna hii, Je, *TAZARA* inataka sisi tusaidie kulinda reli kama wao hawataki kutusaidia hata kutupa umeme kwa malipo! Wameondoa jenereta, wameipeleka Dar es Salaam. Nami nimefuatilia jenereta ile, inakaa tu Dar es salaam. Sasa hii maana yake nini? Naomba Wizara ya Nishati na Madini na Miundombinu, tafadhali wafuatilie suala hili, walirudishe lile!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye Wizara ya Miundombinu, kuhusu barabara. Hii ni ahadi ya Rais wakati wa kampeni. Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba barabara ya Morogoro mpaka Kisaki Stesheni itakuwa barabara ya changarawe na ya kupitika wakati wote. Barabara ya Ubena – Ngerengere – Tunyunguo – Kiganila – Mvuha, nayo pia itakuwa barabara ya kiwango cha changarawe. Lakini, aliahidi kwa sababu alivukia chini Mto Ruvu wakati huo ulikuwa umekauka, tuliweza kumvusha chini, akasema hapa nilipovukia, litajengwa daraja ili kurahisisha utaratibu huu wa kuweza kuunganisha barabara hii. Mpaka kesho! Sasa imekuwa ndoto. Bahati nzuri, Naibu Waziri wa Miundombinu aliyekuwepo, amefika na nimemwomba Naibu Waziri ambaye yupo sasa, siyo tu afike, twende wote nikamwonyeshe ili naye ajue nini maana ya hiyo dhahama, ili ahadi hii itekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna swali la Bandari Kavu. Tunajidanganya Dar es Salaam tukafikiri tunaweza kutengeneza Bandari Kavu pale tu kwa kusogeza watu. Mimi nafikiri siyo Bandari Kavu. Dar es Salaam pamejaa. Msianze kusukuma watu zaidi Kurasini kule.

Hebu Serikali ifikirie kuhama ije Ruvu pale ambapo treni inapita juu. Itengeneze maeneo makubwa kabisa ya kukabidhi kila nchi ya kutoka jirani zetu wawe na eneo la kuweka mali zao na iwe tayari imekwishatengeneza na kupima na ardhi, iwalipe wananchi wenyewe ili tukabidhi watu hawa itengenezwe pale Bandari Kavu kubwa kabisa. Tutakuwa tumevutia wamiliki wote, wafanyabiasdhara wote wa nchi za jirani kuja kuwekeza wao wenyewe. Lakini, tuking’ang’ania Dar es Salaam kutengeneza Bandari Kavu, mwisho wake tunakuja tunaweka Bandari Kavu hata barabarani, tunahatarisha watu kugongwa. Mimi nitashauri Serikali iwe hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile kuna tatizo la uwekezaji. Katika nchi hii, mwekezaji ambaye ana pesa, anakuja mara moja, anasema nataka kuwekeza kwenye kilimo, hakuna mahali pa kumpa. Tuna mapori mengi, siyo mahali pa kuwekeza. Mahali pa kuwekeza tayari patayarishwe, pamekwishapimwa, kuna hati, huyu mwekezaji anaonyeshwa tu eneo ni hili, hati ni hii, toa pesa. Utaona wawekezaji wanawekeza. Lakini wangapi wamekuja hapa, wamekwenda *Mozambique*! Wamehama wamekwenda hata Kigali, sisi tuko hapa tunangojea wawekezaji kwa sababu mlolongo wetu wa kumpa mtu ardhi ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie benki. Nashukuru sana Serikali imeongeza mtaji kwa *Tanzania Investment Bank* ili sasa iweze kujikokota ikawa Benki yenye nguvu. Lakini, imesahau chombo kimoja na mali yake yenyewe, hii ni Twiga *Bankcorp*. Hii ni Taasisi ya Fedha, ikiongezewa mtaji, itakuwa ni Benki ambayo inaweza kuisaidia Serikali katika kazi zake.

Ni Benki nzuri, wanajitahidi wale vijana, lakini hawana ruhusa ya kufanya kazi kama Benki. Hapa naomba Serikali iangalie vizuri hawa, waongeze Benki. Hata kama tukiwa na pesa kiasi gani, nyingi kiasi gani kwenye Benki za biashara, bila ya Serikali kuwa na Benki ya Kilimo ni kazi bure. Kilimo hakiwezi kuinuka na kwenda hata kidogo,

lazima tuwe na Benki ya Kilimo. Benki ya Kilimo ndiyo inayoweza kumpima mkulima anayelima kwa jembe, mkulima anayelima kwa nguvu ya wanyama na mkulima anayelimia trekta, kumkopesha kiasi gani, sio benki aina nyingine yoyote. Benki ya aina nyingine yoyote itamkopesha mfanyabiashara hata kama wa kupika vitumbua, siyo mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kuzungumzia *Internal Auditors*. Hawa *Internal Auditors* wanamsaidia sana *Auditor General*. Lakini, wanatawaliwa na nani? Hawana chombo! *Internal Auditor* yeye anatawaliwa na yule Mkuu wa Taasisi, sasa huyu huyu anatakiwa amkague huyu Mkuu wa Taasisi, lakini huyu huyu ndiye anayemtawala huyu *Internal Auditor*. Haiwezekani hata kidogo! Mtoto hawezi kumkagua baba, haiji! Akiambiwa alale wakati wa usingizi hata kama ni saa mbili usiku, atalala tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, *Internal Auditor* kama hakutengenezewa chombo akawa huru, awe anamu-*audit* huyu ambaye ameambiwa utakwenda kufanya shirika fulani, wakati wote atatoa mahesabu kufuatana na utashi wa bosi wake, ama Katibu Mkuu, ama Mkurugenzi. Hii naomba Serikali iangalie kweli kweli. Kama inawezekana kwa muda huu, basi *Internal Auditors* wapeleke kwa *Auditor General* wawe ndio chini yao na iwe ndiko wanakojibu.

Mheshimiwa Mwenyekitii, kwa hiyo, hawatakuwa waajiriwa wa taasisi au Wizara. Ni chombo muhimu sana, lakini tunadhani ni watu wadogo tu wapo tu hapo, hapana. Wapo hapo wanajitahidi kufanya kazi zao kwa dhati kabisa, lakini wanatawaliwa na watu walioajiri. Nami nikimwajiri mtu, halafu akini-*audit*, akisema nimefanya makosa, nitamwona hana adabu, namfukuza. Hili lazima tuangalie kweli kweli! Ni kitu muhimu kabisa watu hawa wawe na chombo chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema ile hotuba ya Mwenyekiti wangu, ilitosheleza, nami nichangie mambo yangu jimboni. Nakushukuru sana. Naunga mkono hoja! *(Makofi)*

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii jioni ya leo. Awali ya yote, niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na neema, pamoja na misukosuko midogo ya kiuchumi tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao wameendelea kutoa pongezi kwa bajeti nzuri ambayo ina mwelekeo kwa maana ya matumaini mapya ambayo tunaendelea kuwa nayo. Tunaweza tukalaumu sana, lakini ni rahisi sana kukosoa kwa kuangalia wachezaji kwenye mpira pale uwanjani ukiwa nje. Lakini ukiwa wewe mwenyewe unacheza, kidogo ni vigumu pia. Tunahitaji tufanye bidii, ndiyo na mabadiliko mengine, lakini tusiwe tunalaumiana kupita kiasi na labda tusijilinganishe na hizi nchi nyingine ambazo zilishaendelea miaka mingi mno. Unafika kwenye nchi nyingine, unaangalia jengo fulani la kiutawala, unaambiwa hili jengo lina umri wa miaka 900. Leo hii Tanzania miaka 47 tu ya uhuru, tunataka tulingane na hao

ambao miaka 900 walishaendelea. Kwa hiyo, ninasema tusijilaumu, lakini tujikosoe pale ambapo tunaona tumefanya makosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wameishazungumzia kwa mapana mengi, sasa na sisi wengine tunakuja dakika hizi za mwisho, tuendelee kugusiagusia yale machache. Ningeomba nijielekeze tu kwa mtiririko ufuatao kwa kuamini kwamba ili tuweze kufikia yale tunayoyazungumzia au kumletea Mtanzania maendeleo tunayotarajia, elimu ni kipaumbele kama kilivyowekwa kwenye bajeti yetu. Bila kuwaelimisha wananchi wetu vizuri, haya maendeleo tunayotaka kuwaletea hayatakuwa na maana kwao, nikimaanisha lazima tuweke msisitizo mzuri sana kuanzia *kindergarten*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo lingine katika elimu zetu, tusiende mno kwenye haya masomo ya *theory* zaidi, *practical* au masomo ya kisayansi ni muhimu zaidi. Tukiwa tunazalisha mno wasomi kwa ajili ya vyeti tu, tutakuja kuwa na Vihiyo! Leo hii sio ajabu ukamkuta *Engineer* ame-*graduate*, lakini mtu aliyetoka *Technical School* anaweza akafanya vizuri zaidi yake katika mambo ya *practical site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika elimu yetu tujielekeze elimu ipi ambayo itatufaa. Tunazungumzia mchakato wa kuwa na viwanda nchini kwetu. Hivi viwanda kama hatujawafundisha watu wetu mambo ya kisayansi jinsi ya kufanya hizo kazi na kuhudumia viwanda, nani atakuja kufanya kazi humu? Ndio mwanzo wa kulalamika kwamba kuna ajira zinazochukuliwa na jirani zetu. Lakini ni sisi wenyewe tupange mipango mizuri katika elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi tunawatakia mema zaidi, lakini afya zao lazima tuzijali. Tumekuwa tunazungumza hapa kwamba afya ni jambo la msingi, afya ya mama na mtoto. Lakini lazima tuzidishe huduma kwa wananchi wetu kwa upande wa afya. Nishukuru kwamba zipo harakati za kuanzisha zahanati katika ngazi ya kijiji. Lakini zahanati hizi lazima tujitahidi zipate huduma. Kwenye Kata zetu tuwe angalau na vituo vya afya ambako mwananchi halazimiki kusafiri kwenda mbali zaidi katika kupata huduma za afya. Nashukuru kwamba katika huu ugonjwa mbaya wa UKIMWI, nimesikia kwamba yale mambo ya *RFA* sasa zile hayapo, zile pesa zitakuwa zinakwenda moja kwa moja Mikoani ambako natumaini zitakuwa zinafika kwa walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu dhana ya kufa kufaana ilikuwepo hapo, natumaini kuna watu wengine labda walikuwa wakiombea hata dawa isipatikane kuhusu UKIMWI kwa sababu wamejengea majumba, wamenunulia magari kwa kisingizio hicho hicho cha UKIMWI.

Mimi ningeomba tu kwamba tuwe na moyo wa kumgeukia Mwenyezi Mungu na kutambua kwamba aliyeathirika siyo sehemu ya kupatia kula na tuwe na kiasi sisi binadamu. Kama tunakula kwenye sinia, hukushiba, kulamba vidole hautaweza kushiba zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la miundombinu. Miundombinu ni kitu muhimu mno! Wenzangu wote wamezungumzia barabara kutoka kona zote za nchi hii.

Huu uchumi tunaotaka upae, hautapaa kama miundombinu yetu ni mibovu. Miundombinu kwenye viwanja vya ndege, barabara, usafiri wa maji, miundombinu kwa ujumla wake ni muhimu mno.

Nami wakati naanza, nimesema naipongeza hii bajeti kwa sababu hata miundombinu imepewa kipaumbele. Kwa wananchi wangu wa Hai wanakumbuka ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa pale Bomang'ombe, kuwekea barabara ya Kwasadala – Masama lami kwa maana ya kwenda kwenye Mlima Kilimanjaro ili kupanua wigo au vyanzo vingine vipya zaidi vya mapato. Kwa hili naipongeza sana Serikali na ndio narudi kusema kwamba huduma ya miundombinu ni muhimu mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili na amani iendelee kuwepo, baada ya mambo mengine niliyozungumzia hapo juu yawe mazuri na utawala bora. Utawala bora una nafasi yake muhimu sana. Mwenzangu pale alisema kuna kupima *happiness*, kwa nini watu wanakuwa na hasira na vitu vingine.

Mimi nadhani dhana ya utawala bora ikieleweka vizuri na tukajituma vizuri kwa vitendo kwa maana ya utawala bora kuwajali wananchi na kuwahudumia inavyofaa na baada ya uchumi na mambo mengine kuwa mazuri, haya mambo ya hasira hayatakuwepo. Kwa hiyo, ningeomba sana suala la utawala bora tulizingatie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna kile kitu ambacho tunasema ni uti wa mgongo. Tangu sisi wengine tunakuakua tulisikia kwamba kilimo ni uti wa mgongo. Sasa uti wa mgongo huu hafifu. Ningeomba tuweke jitihada kwenye kilimo cha mazao na ufugaji. Tukiweka jitihada za kutosha, hapo kweli tutaweza kumkomboa huyu Mtanzania kwa maana ya kuwa na *mechanization* kwenye kilimo, tuachane na hiki tunachosema ni jembe la mkono miaka nenda rudi. Hata na Maksai labda na yenyewe ni kwa sababu tu ya umaskini wetu. Hii Maksai ya kukokota jembe la ng'ombe nacho ni kilimo duni. Tungeweka matrekta, tukaanzisha vikundi ambavyo kutakuwepo na watu wachache ambao wataweza kukopesheka kwenye kata zetu, wakaweza kukopeshwa yale matrekta, wakawakodishia wakulima wenzao, baada ya mavuno wakaja kulipa. Hapo tutakuwa tunamkomboa mwananchi.

Lakini, tusiishie tu kuzungumza. Natumaini katika Wizara ambazo zina wasomi, mojawapo ni Wizara ya Kilimo. Pale wapo Madokta wengi sana, *degree* ziko nyingi, amebeba mpaka mtu analemewa. Lakini, ni kwenye meza. Tuwape fursa hawa watu. Ndio maana pale tunaposema sasa tuanzishe Benki za Kisekta, Benki za Kilimo, Benki za Ujenzi ili wale wanao-*graduate SUA* waweze kukopeshwa na wakaweza sasa ku-*apply* ile *theory* waliyokuwa wanaipata shuleni *to the practical side of it*.

Lakini, tusizungumzie kwamba tunaleta wawekezaji kutoka nje, waje wawekeze kwenye kilimo. Eh, jamani kila kitu tuwape tu! Haitawezekana! Sisi Watanzania lazima tujiamini tunaweza. Kuna baadhi ya mataifa yetu hapa Afrika sasa hivi yameweza kuonyesha kwamba Afrika tunaweza na kweli Afrika tunaweza. Tuwawezeshe hawa wazalendo wetu wanaosoma na tukionea aibu hili, tutakuja kujuta. Historia itakuja kutusuta! Tutakuta tumekabidhi kila kitu ndani ya nchi yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hicho kilimo ili kiwe na tija zaidi, lazima tuwe na viwanda *(Agro-processing)* ili ku-*add value* katika haya mazao yetu ili huyu mkulima wetu azidi kupata bei nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri kuna watu tumezungumza nao pale Uingereza wanaitwa *Fair Trade*, wanasema wako tayari kununua mazao yanayotoka katika nchi masikini tukiwepo sisi kwa hayo mazao tunayolima kidogo kidogo. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tukashawishi wananchi wetu kwenye majimbo yetu tunakotoka. Hilo soko lipo pale Uingereza, maana Uingereza asilimia kubwa ya chakula chake wanaagiza kutoka nje. Wako tayari kununua hivi vyakula. Ukienda hata kwenye *supermarket* zao utakuta vyakula vinatoka nchi mbali mbali, wanaviita *organic* ambavyo ndivyo vyakula ambavyo tunavilima hapa. Kwa hiyo, ningeomba tujitahidi kwenye kilimo na kwenda kuwashawishi wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kilimo tunawanyanyasa wananchi wetu. Pale Hai, miaka ambayo tunabarikiwa kuvuna mahindi kwa wingi, unakuta nchi jirani ya Kenya kuna soko zuri, lakini tunawazuia wale wananchi kuuza. Tukiwazuia kuuza, bado kuna panya *route* ambako wananchi wanalazimika kwenda kuhonga wale walinzi wetu mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwa nini mpaka tumlazimishe mwananchi akahonge? Kwa nini usiwekwe utaratibu wa kulipa kiasi fualani? Sasa hivi hali ya chakula duniani, kweli ni mbaya. Lakini nazungumzia hii hali huenda isiendelee. Hali ikiwa ni nzuri, tusiendelee kuwabana wananchi wetu. Kama kuna uwezekano mwananchi kuuza chakula nje ya nchi kwa bei nzuri zaidi, tukaweza kukiagiza kwa bei rahisi, mimi nadhani ingekuwa ni jambo la neema ili na hiki kilimo kiweze kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbolea ya ruzuku tulisema ingekuwa angalau Sh. 40,000/= au Sh. 50,000/=. Lakini, ime-*shoot*, imefikia mpaka Sh. 100,000/=. Tuna maswali mengi sana tunaulizwa na wananchi wetu, lakini sasa majibu tuyatoe wapi! Kwa hiyo, ni suala ambalo tungelizungumzia vizuri na kuliangalia kwa maana ya kuwa na viwanda vyetu vya mbolea. Namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyotembelea pale Minjingu, ile mbolea mimi mwenyewe nimejaribu kuitumia na inafaa na inasaidia sana ardhi. Kwa hiyo, ningeomba izidi kusambazwa nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Utalii, ukizungumza na watu wanaofahamu utalii wanakwambia Tanzania tumegusa sehemu ndogo sana ya utalii. Tuna vivutio vingi hatujavisema, hatujajitangaza. Ukienda kwenye baadhi ya nchi nyingine, hawajui Tanzania iko wapi! Hapo mimi ningeomba balozi zetu zitumike na mahali pengine pale ambako kuna *opportunity* kubwa zaidi za kibiashara, tukafungue huko balozi ndogo, tuweze kujitangaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye utalii, ningependekeza tuanzishe Mfuko wa Utalii. Mfuko huo wa Utalii utakuwa unawawezesha wananchi kwenda kuyasema yale

wanayodhania kwamba yanaweza kuwa vivutio kwa wageni wetu ili kuweza kuanza kuvitangaza vile vivutio na kuweza kuongeza tija zaidi katika hayo maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba tunaelewa wazi kwamba Mlima Kilimanjaro ndio kivutio kimojawapo kinachoingiza mapato mengi katika Sekta ya Utalii. Lakini bado hatujautumia ule Mlima vizuri. Kuna utalii wa *Non-Summit Tourism of Mount Kilimanjaro*, inawezekana; *Echo Tourism,* inawezekana. Kwa hiyo, huo Mlima bado hatujautumia. Naomba sana tuongeze jitihada katika kuutumia ule Mlima. Hilo nitakuja kuongea na Waziri wa Utalii, anieleze kile kilio chetu kimeishia wapi kwamba tuwe tunapata gawio rasmi zile Halmashauri zinazozunguka Mlima ili wale wananachi wawe na moyo wa kuendelea kuutunza ule Mlima. Vinginevyo, tukiwakatisha tamaa, ule Mlima utunzaji wake utakuwa ni mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kuwa na uchumi mkubwa, lazima tujipange vizuri. Tulikuwa na mambo ya madini hapa, wawekezaji wameshakuja, wameshaifahamu Tanzania kwenye madini. Sasa tuongeze, *fifty fifty,* tuwe na mikataba ambayo tumeshaitayarisha kabla *(Blue Prints),* mwekezaji kutoka nje akija hapa, akae akijua anakuja kuwekeza na kwenye taratibu zipi. Hataki, aondoke zake! Tumeshafahamika kwenye hiyo sekta. Kwa hiyo, naomba hapo tusioneane aibu, tuwaeleze wazi, mtu awe anajua kwamba anakuja kuwekeza kwenye sehemu ya aina gani. Kwa hiyo, naomba tuwe na Mabenki hayo ya Kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni sikitiko kuhusu suala la mafuta. Tunaondoa ule ushuru! Ndio mwanzo wa kuja kupata haya mafuta ya ajabu ajabu yenye kuleta kansa hapa nchini. Hawa wananchi wetu tuwatunze! Lakini alizeti inazalishwa sana Singida na sehemu nyingine hata kule kwetu Kilimanjaro tunalima alizeti siku hizi. Ningeomba ule ushuru urudi tena pale pale au uongezwe zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kufikia Dira ya Maendeleo ya mwaka 2020/2025, lazima tufanye bidii zaidi na sisi wananchi wa Tanzania tuwe *serious.* Yale mambo ambayo siyo ya msingi tuachane nayo. Tunatumia hela nyingi sana kwenye sherehe, maharusi, misiba. Tunafanya misiba siku hizi ya kifahari. Tuachane nayo! Ukienda India, Wakenya wanaosoma India, ni zaidi ya 10,000, Watanzania ni wachache. Tuchangiane katika kwenda kusomesha watoto wetu au kwenda kutibu watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusije tukawasahau wastaafu. Watu wameijenga nchi hii, wameitumikia katika hali ngumu sana. Sasa tuwakumbuke wastaafu wetu ili waweze kupata kima kizuri na kima cha chini cha mshahara, tukiongeze jamani. Wale Madiwani wetu tusiwasahau na watendaji wa vijiji. Lakini, wananchi tuwakumbuke. Ukali wa maisha upo wala siyo siri, ukali wa maisha ni mkubwa mno.

Nilipanda *lift* moja pale Dar es Salaam, nikakuta Bwana mmoja anayeongoza *lift* ananifahamu kama mimi ni Mbunge. Akaniambia Mheshimiwa mnatupeleka wapi? Kopo dogo la mkaa sasa hivi Sh. 1,500, huchemshii maharage, ukapikia ugali wala ukachemshia chai, vipi? Kwa hiyo, naomba tuwakumbuke. Tuangalie ile mianya yote ambayo inapoteza pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nawashukuru wananchi wangu wa Hai na ninazidi kuomba Mwenyezi Mungu nchi yetu iendelee kubarikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kimbita. Nasema tu kwamba, baada ya Mheshimiwa Janet Kahama kuzungumza, nitatoa fursa ili Mheshimiwa Waziri wa Fedha atoe maelezo machache kuhusu utofauti wa takwimu kati ya hotuba yake na kile kitabu cha *Volume One*. Kwa hiyo, tumekubaliana na Mheshimiwa Janet Kahama kwamba atatumia muda mfupi kidogo.

**MHE. JANETH B. KAHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ingawa ni dakika kumi, lakini nitajitahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpa pongezi nyingi sana Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, kwa kuchaguliwa kuwa Waziri Mkuu. Pia, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara hii, Waziri, na watalaam wake kwa kazi yao nzuri ambayo wamekwishaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kwenye maeneo mawili, ambayo ni uwekezaji wa wanawake na pia, katika utegemezi wa Tanzania. Mambo ya uwekezaji, wanawake yamepewa kipaumbele katika hotuba ya Waziri ambayo itakuwa katika uwezeshaji wa wanawake.

Baada ya hapo, naomba kutoa ushauri kidogo katika eneo hilo la uwekezaji. Wanawake wafikiriwe eneo la *SACCOS* ambalo sasa hivi ni ukombozi kwa wanawake wengi Tanzania. Liwekwe fungu la fedha kama inawezekana, la kuwatosha kuwasaidia, kutoka katika Wizara hii. Lakini pia *SACCOS* nyingi zifikiriwe kupewa mikopo zaidi ili kuendeleza uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba Wizara ifikirie kutenga kitengo maalum *dedicated windows* au s*pecial windows* kwa ajili ya kupitia Benki ya Rasilimali *(TIB)* ambayo mpaka sasa hivi imekwishapata mtaji wa shilingi milioni 50 ili hii iwezeshe kuwasaidia wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia naomba iharakishe sana kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Wanawake *(The Women Development Bank)*. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nimeona amezungumzia Benki ya *TIB* na *Postal Bank,* lakini hakuna mahali alipoizungumzia Benki ya Maendeleo ya Wanawake. Inanitia hofu sana, sijui Benki hii itaongelewa katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto au itazungumziwa wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sana wakati wa majumuisho yake aweze kutueleza kuhusu benki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba vikundi vya wanawake wajasiriamali, wasaidiwe kuunda angalau kampuni kubwa ya pamoja *(A Holding Cooperation)* kama vile *NICO* ambayo itawawezesha hawa wanawake waweze kuanzisha makampuni ya biashara mengi, wasaidiwe kuweza kuweka hisa hapa nchini ili kupata faida yao zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikundi hivi pia visaidiwe kuanzisha kampuni ya ubia ya mauzo ambayo ni kitu muhimu sana. Wajasiriamali hawa huwa wana matatizo sana, wanafanya biashara nyingi, lakini kwa bahati mbaya hawana soko la kuweza kuwasaidia popote pale. Kwa kipindi kilichopita, hata wakati wa saba saba huwa kuna sehemu moja tu iliyotengwa kwa ajili ya kuuza vitu vyao. Serikali ingeangalia katika eneo hili katika Mikoa yote angalau ya nchi yetu ya Tanzania waweze kupata maeneo mbalimbali ya kufanyia biashara zao za uhakika. *(Makofi)*

Lingine ambalo nilitaka kuzungumzia ni kuhusu barabara, lakini acha niendelee katika utegemezi kama nilivyosema. Utengemezi upo katika maeneo ya aina tatu. Utegemezi wa bajeti, utegemezi wa kujitakia na utegemezi wa kutegemeana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia utegemezi wa bajeti, Mheshimiwa Waziri yeye mwenyewe amekwishasema kuwa mpaka sasa amechukua jitihada tayari kuhakikisha kuwa anapunguza utegemezi kutoka asilimia 42 mpaka asilimia 34 jambo ambalo kwa kweli wanastahili kupewa pongezi sana. Utegemezi wa kujitakia ni ule utegemezi ambao una kasumba wa kutawaliwa, lakini pia kwa upande mwingine inatokana na sisi wenyewe kutokuwa makini katika mipango yetu ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, wananchi wengi hupendelea sana kununua vitu vinavyotoka nje ya nchi badala ya kununua vitu vyetu vinavyotengenezwa hapa Tanzania. Kasumba hiyo ni mbaya kwa sababu inaumiza sana viwanda vyetu nchini Tanzania, lakini pia inapunguza ajira kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kero kubwa sana ninayonipata mimi mwenyewe kuona samani za nchi hii zinaletwa kutoka nchi za nje kama vile Singapore, Malaysia, China na kadhalika ambapo samani za nchi hii kama vile *furniture* zinatengenezwa kwa miti ya mininga na miti mingine ambayo ina ubora zaidi inayopatikana hapa nchini. Jambo hili mimi sijalielewa hata kidogo, maana hata Serikali yenyewe imeanza kununua *furniture* nyingi kutoka nje ambapo wangeweza kutumia *furniture* za hapa nyumbani zinazodumu. Naiomba Serikali iangalie katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa katika hili ni kuboresha utengenezaji wa *furniture* zetu. Vijana wetu wanaweza wakafundisha na wakawa makini katika kutengeneza *furniture* nzuri. Tuna vikundi vingi sana, vingine viko Arusha, Dar es Salaam, Dodoma na kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Dodoma Veyula, kwa *Sister* Rosalia, kuna *furniture* nzuri ambazo zimetengenezwa katika kiwango cha kimataifa, ni vyema Serikali ingeliangalia jambo hili na wao wenyewe waonyeshe mfano wa kununua vitu vinavyotengenezwa hapa nchini kuliko kuagiza kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuleta samani kutoka nje vinagharamia fedha za kigeni nyingi sana, lakini pia vina bei kubwa sana, halafu havina ubora hata kidogo. Kwa hiyo, ningeomba Serikali iliangalie jambo hili na wananchi wenzangu Watanzania tuelewe jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapunguza pia umaarufu wa khanga. Hili jambo mimi linaniumiza sana. Khanga zinatengenezwa Tanzania na zinapendwa na watu wengi Afrika Mashariki, kusini mwa Afrika, kama Lesotho, Swaziland lakini bado unaona khanga nyingi zinaingia kutoka India, China na Japan. Mimi sijaelewa jambo hili hata kidogo na tukumbuke khanga ni fahari ya Tanzania, hakuna nchi nyingine duniani inatumia khanga tangu mwanzo isipokuwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatutakuwa thabiti kuangalia utegemezi wa namna hii tutakwisha. Ni lazima tuweke bidii na umakini kwa kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri. Utegemezi unaokubaliana katika nchi za ulimwengu, ni ule utegemezi unaoendana na kukubaliana *inter independence*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sina muda, jambo muhimu lingine nililotaka kuzungumzia ni kuhusu wastaafu wetu. Wastaafu wetu wamepata shida sana na hasa wale waliofanya kazi *East African Community* na wengine ambao wamefanya kazi Serikalini. Kwa nini isifike wakati sasa Serikali iamue kufanya mashirika ya *PPF*, *NSSR* yakashinikizwa kushirikiana ili kusaidia wastaafu hawa walipwe pesa zao mara moja tufunge kitabu hicho tuendelee na kuangalia shughuli za maendeleo ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia kwamba barabara zinaleta kero sana katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mama Janeth Kahama na tunakushukuru sana kwa muda uliotupatia. Moja kwa moja naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi ili atoe ufafanuzi ambao anataka kuutoa.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi, nitatumia muda mfupi sana ili kufafanua yaliyojitokeza jana na ambayo ndiyo yameandikwa katika magazeti yote ya leo na yale mengine yote ambayo hayakuandikwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka niwapongeze Waheshimiwa wale watatu waliozungumzia zile takwimu katika vitabu vile. Hii inaonyesha kwamba wenzetu ni makini na wanasoma kila kitu. Hilo kwa kweli kwa upande wa Serikali ni jambo la kupongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nataka kulizungumzia ni ile hotuba niliyoisoma hapa Bungeni. Ile hotuba iliidhinishwa na Serikali masaa mawili kabla sijaisoma humu ndani. Kwa hiyo ni *official document* ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vitabu vyote vinne vilichapishwa mwezi Mei kwa sababu isingeweza kuchapishwa mwishoni mwa Juni, kwa sababu ni vingi sana na wakati huu hotuba zote zinachapishwa kati ya Mei mpaka naingia hapa Bungeni kuja kusoma hotuba maamuzi mengi yamefanyika. Mojawapo ni kwamba kama mnavyofahamu sasa hivi Afrika Mashariki bajeti zote kwa nchi tatu zinasomwa siku moja, kwa hiyo, kuna *pre-budget,* kikao cha Mawaziri wa Fedha wa Uganda, Kenya na Tanzania ambao ni lazima mkubaliane maeneo fulani fulani ili yanaposomwa kusije kukawa na tofauti kati ya nchi moja na nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kikao hiki kilifanyika tarehe 2 Juni, na kwa sababu wenzetu Kenya walituomba kwa sababu ya matatizo waliyoyapata, ilibidi wachukue muda mrefu kukamilisha bajeti yao. Hiyo ni sababu mojawapo ambayo ilichelewesha na ilibidi kikao kifanyike tarehe 2 Juni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine baada ya vitabu vile kuchapishwa kumekuwepo na maamuzi mengine katika ngazi mbalimbali za Serikali ambazo kwa namna fulani ama zimeongeza mapato mahali fulani au zimepunguza gharama mahali fulani na hilo ni lazima litasababisha takwimu ambazo zilichapishwa mwezi wa Mei zitofautiane na zile zilizosomwa mwezi Juni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo ni kubwa, mwaka huu kwa sababu zinazoeleweka, wahisani walichelewa kidogo kuthibitisha kila Mhisani amechangia *General Budget Support* anayechangia *basket Fund* na anayechangia miradi. Wamethibitisha karibu na mwishoni mwa mwezi wa Juni kwa sababu hotuba yangu mimi imechukua hali halisi ya kila kilichoidhinishwa na wafadhili mpaka natoa bajeti, vitabu vile havikuwa na tarakimu nyingine ambazo zimeidhinishwa mwishoni mwa mwezi wa tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo pia ni zuri, ni kwamba thamani ya *NMB* imeongezeka sana kuliko ilivyothaminiwa mwanzoni mwa mwaka huu. Kwa hiyo, utakuta fedha ambazo Serikali itazipata siyo zile ambazo kiongozi wa Upinzani - Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed alizungumzia, lakini bado ni zaidi kuliko zile ambazo tulikuwa tumekusudia kwamba tutazipata mwanzoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka shilingi bilioni 42 tukafika shilingi bilioni 58. Mpaka mwishoni ushauri wa wataalamu kwamba bei nzuri ambayo tunaweza tukauza hisa kwa wananchi ni shilingi 600 kwa hisa ambazo zinatoa shilingi bilioni 60 baada ya kukata makato ya wale waliotufanyia tathmini. Hiyo nayo katika vitabu vile mtakuta

kuna shilingi bilioni 58, lakini *figure* hasa mpaka mwishoni nakuja kutoa hotuba hapa ni shilingi bilioni 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mapendekezo mengine ambayo yalitolewa katika vikao vya juu vya Serikali ambayo na yenyewe hayakuwepo katika vitabu hivi vilivyochapishwa mwezi Mei. Mapendekezo yale ilibidi yaingizwe baadaye. Mimi nimeyasoma kwenye hotuba yangu ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kawaida, hatutegemei kwamba kila kinacholetwa Bungeni kitakubaliwa na Wabunge jinsi kilivyo. Humu ndani Upinzani wametoa mapendekezo, Kamati ya Fedha na Uchumi na Wabunge wengine wakati wa kuchangia wametoa mapendekezo, baadhi ya mapendekezo yale yakikubaliwa yatabadilisha sura nzima, yataelezewa siku ya kutoa majumuisho ya bajeti yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka kuelezea kwamba kwanza, nawasifu wenzetu waliochanganua zile *figures*, wanaonekana kwamba ni makini na ni watu ambao wanasoma. Kwa hiyo, tunaomba mwendelee kufanya hivyo na Serikali ni wasikivu kama Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi alivyosema. Pale ambapo kuna kitu cha kufaa kwa wananchi tutakisikiliza na tunakifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wenyewe tulishagundua kwamba kila wakati ambapo maamuzi yamefanyika tofauti na tarakimu zilizopo kwenye vitabu, tumeshaanda *addendum* zitasambazwa na mtaziona kwamba zitakuja kuoana na hotuba niliyoisoma.

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wa Spika!

**MWENYEKITI:** Wasilisha.

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO:** Nilikuwa naomba kutoa hoja kwamba tuongeze muda ili Mheshimiwa Waziri wa Fedha aweze kumalizia kutoa maelezo yake kwa kipindi cha nusu saa.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Nimeshamaliza *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mwongozo hauhitajiki tena kwa vile Mheshimiwa Waziri wa Fedha amekwishamaliza.

Mimi nina mambo machache hapa kwenye meza yangu. Nashukuru sana kwa mawasilisho ambayo yametolewa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha nimemwona, hata Mzee John Cheyo amefurahi sana.

Waheshimiwa Wabunge, kuna funguo hapa kama kuna Mbunge yeyote aliyepoteza funguo yake itakuwa hapa meza kuu.

Waheshimiwa Wabunge, kesho wachangiaji watakaochangia ni Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na wengine mtafuatia.

Mwisho kabisa, Mheshimiwa Profesa Mwalyosi aliongelea neno kuperemba mara kwa mara. Tafsiri ambayo nimeipata kwa Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib anasema, Kiswahili halisi ni kumwangalia mtu kwa tahadhari kubwa ili baadaye uweze kuchukua hatua endapo atatenda tendo baya kwako.

Waheshimiwa Wabunge, tafsiri hii hata mimi inaniingia akilini maana hata kwenye Kigogo inakaa sawasawa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, naahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 jioni Bunge liliahirishwa hadi Jumatano, Tarehe 19 Juni 2008 Saa 3.00 Asubuhi)*